# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA
## MWAKA WA FEDHA 2023/24



MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI
MACHI 2025

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT
ISO 9001:2015 Certified

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Mahakama, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma, Simu: 255(026)2161200, Baruapepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

**Kumb. Na. CGA.319/421/01** **27 Machi 2025**

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu,
S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
11400 Chamwino,
**40400 DODOMA.**

**RE: KUWASILISHA TAARIFA KUU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA 2023/24**

Nina furaha kuwasilisha Taarifa yangu ya Jumla ya Mwaka kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Taarifa hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi na kupendekeza hatua za kuboresha, ambazo zinalenga kukuza uwajibikaji katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.

Nawasilisha.

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

## KUHUSU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

**Mamlaka**

Mamlaka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

**Dira**

Kuwa Taasisi yenye Kuaminika na ya Kisasa katika Ukaguzi wa Umma inayotoa Huduma za Ukaguzi za Viwango vya Juu zinazoimarisha Imani kwa Umma.

**Dhima**

Kutoa huduma za Ukaguzi zenye Kiwango cha Juu kwa njia za Kisasa zenye Kuimarisha Uwajibikaji na Uwazi katika Usimamizi wa Rasilimali za Umma.

**Kauli Mbiu**

Kuwa Taasisi yenye kuaminika na ya Kisasa katika ukaguzi wa umma

## Misingi ya Maadili

**Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo:** Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo

**Kufanya kazi kwa uadilifu:** Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadilina sheria katika utoajiwa huduma za ukaguzi

**Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo:** Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi staiki

**Kufanya kazi kwa utaalam:** Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora

**Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi** Tunahimiza, kuvumbua na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwaajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

**Kufanya kazi kwa ushirikiano:** Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje

# YALIYOMO


ORODHA YA MAJEDWALI .......... iv

ORODHA YA VIAMBATISHO .......... vii

VIFUPISHO .......... viii

SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI. xi

MUHTASARI .......... xiii

SURA YA KWANZA .......... 1

UTANGULIZI WA JUMLA .......... 2

SURA YA PILI .......... 5

HATI ZA UKAGUZI .......... 6

SURA YA TATU .......... 10

UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAGUZI ZILIZOPITA .......... 11

SURA YA NNE .......... 13

UTENDAJI WA FEDHA, MATUMIZI, NA USIMAMIZI WA BAJETI .......... 14

SURA YA TANO .......... 25

USIMAMIZI WA UNUNUZI .......... 26

SURA YA SITA .......... 33

USIMAMIZI WA MIKATABA NA HALI HALISI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI .......... 34

SURA YA SABA .......... 45

UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA MRADI WA BWAWA LA UMEME WA MAJI LA JULIUS NYERERE .......... 46

SURA YA NANE .......... 52

UKAGUZI WA KIUFUNDI WA USAMBAZAJI UMEME VIJIJINI .......... 53

SURA YA TISA .......... 59

UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA MINARA YA MAWASILIANO .......... 60

SURA YA KUMI .......... 71

UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UDHIBITI NA UFUATILIAJI WA TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA KATIKA SEKTA ZA UJENZI NA MADINI .......... 72

SURA YA KUMI NA MOJA .......... 79

UKAGUZI WA KIUFUNDI KWENYE UTEKELEZAJI WA MIRADI YA USAMBAZAJI MAJI VIJIJINI CHINI YA WAKALA WA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI .......... 80

SURA YA KUMI NA MBILI .......................................................... 89

UKAGUZI WA KIUFUNDI KWENYE UJENZI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU YA MAJITAKA MAENEO YA MIJINI .................................................. 90

SURA YA KUMI NA TATU .......................................................... 94

UKAGUZI WA KIUFUNDI KWENYE MRADI WA UJENZI WA BWAWA LA KIDUNDA .......................................................... 95

SURA YA KUMI NA NNE .......................................................... 100

UKAGUZI WA KIUFUNDI KWENYE UKARABATI NA UJENZI WA SOKO JIPYA LA KARIAKOO, SOKO KUU LA MWANZA, NA STENDI YA MABASI YA NYAMHONGOLO .......................................................... 101

SURA YA KUMI NA TANO .......................................................... 107

UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UFUNGAJI NA MATENGENEZO YA ALAMA ZA BARABARA NA TAA ZA KUONGOZA MAGARI .................................. 108

SURA YA KUMI NA SITA .......................................................... 114

UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UBORA WA USANIFU WA KAZI ZA BARABARA .. 115

SURA YA KUMI NA SABA .......................................................... 123

UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA DARAJA LA KIGONGO - BUSISI ..... 124

SURA YA KUMI NA NANE .......................................................... 130

UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA DARAJA LA PANGANI NA BARABARA ZAKE .......................................................... 131

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na. 1: Idadi ya miradi iliyokaguliwa kisekta 2023/24 .................... 3
Jedwali Na. 2: Ukaguzi wa kiufundi uliofanyika mwaka wa fedha 2023/24..... 3
Jedwali Na. 3: Muhtasari wa hati za ukaguzi 2023/24 ............................. 7
Jedwali Na. 4: Mwenendo wa hati za ukaguzi ...................................... 8
Jedwali Na. 5: Hitimisho la uzingatiwaji wa sheria ya ununuzi ................... 8
Jedwali Na. 6: Hitimisho la uzingatiwaji wa sheria za bajeti ..................... 9
Jedwali Na. 7: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita......11
Jedwali Na. 8: Uchambuzi wa utendaji wa kifedha kisekta ......................14
Jedwali Na. 9: Fedha za miradi zilizokopwa na kutorejeshwa ...................15
Jedwali Na. 10: Malipo ya kazi yaliyofanywa pasipo vipimo vya kazi ...........16
Jedwali Na. 11: Watu waliothiriwa na miradi kutolipwa fidia ...................17
Jedwali Na. 12: Malipo kwa fedha taslimu kutofanyika kwa usahihi ............19
Jedwali Na. 13: Matumizi yasiyo na viambatisho..................................20
Jedwali Na. 14: Kuchelewa kuwasilisha kodi ya zuio ..............................21
Jedwali Na. 15: Miradi iliyokosa fedha kwa kutofaulu ulipaji unaohusisha matokeo ..........................................................................23
Jedwali Na. 16: Ununuzi uliopangwa ambao haujatekelezwa....................26
Jedwali Na. 17: Gharama za ziada kwa miradi ....................................28
Jedwali Na. 18: Kazi za ziada ambazo hazikuidhinishwa na bodi za zabuni ...29
Jedwali Na. 19: Bidhaa za Ujenzi Zilizonunuliwa kutoka kwa Wazabuni Wasioidhinishwa ..............................................................31
Jedwali Na. 20: Ununuzi uliofanywa nje ya Mfumo wa Kielekitroni wa Ununuzi wa Umma .........................................................................32
Jedwali Na. 21: Mikataba Iliyosainiwa bila Kuhakikiwa ...........................34
Jedwali Na. 22: Miradi na riba iliyolipwa kutokana na kuchelewesha malipo ya wakandarasi ...................................................................36
Jedwali Na. 23: Malipo ya awali yasiyokuwa na dhamana ........................37
Jedwali Na. 24: Madai ya muda mrefu ya wakandarasi ...........................38
Jedwali Na. 25: Miundombinu ya miradi iliyokamilika lakini haikuwa inatumika ......................................................................................42
Jedwali Na. 26: Ongezeko la gharama za kazi katika Vipande vya 1 hadi 6 ...54
Jedwali Na. 27: Ruzuku zilizotolewa kwa kata ambazo tayari zilishafikiwa na huduma ......................................................................61

Jedwali Na. 28: Ruzuku kwa maeneo ambayo awali hayakuwa na huduma za mawasiliano ........................................................................62
Jedwali Na. 29: Tofauti kati ya ruzuku zilizotengwa na zilizotolewa ...........63
Jedwali Na. 30: Kata ambazo zilishafikiwa na huduma za mtandao lakini zilipewa ruzuku ..................................................................64
Jedwali Na. 31: Madai ya fidia yasiyodaiwa........................................66
Jedwali Na. 32: Malipo ya awali yaliyofanywa bila dhamana ya benki .........67
Jedwali Na. 33: Miradi ya minara ya mawasiliano iliyotekelezwa bila ya mikataba...................................................................67
Jedwali Na. 34: Miradi iliyothibitika kuwa hewani lakini haikufikia viwango..68
Jedwali Na. 35: Maeneo ya kazi yaliyokamilika bila kufanyiwa vipimo vya kuthibitisha ubora ..........................................................70
Jedwali Na. 36: Muda wa usanifu wa miradi na miaka ya kuanzia ..............82
Jedwali Na. 37: Gharama za ziada zilizotumika kukamilisha miradi baada ya kusitisha mikataba ..........................................................83
Jedwali Na. 38: Mikataba iliyositishwa na kiwango cha fedha kilichotakiwa kukatwa kama fidia ........................................................85
Jedwali Na. 39: Mchanganuo wa ongezeko la gharama katika miradi ..........86
Jedwali Na. 40: Malipo yaliyolipwa kwa kazi ambazo hazikufanywa............92
Jedwali Na. 41: Ucheleweshaji wa malipo kwa mkandarasi na mshauri elekezi ..........................................................................96
Jedwali Na. 42: Malipo kwa mabadiliko ya kazi ambayo hayakuidhinishwa....97
Jedwali Na. 43: Hali ya malipo ya fidia ya ardhi kwa bwawa la kidunda.......98
Jedwali Na. 44: Mchanganuo wa gharama za fidia baada ya kurudia tahthmini ..........................................................................98
Jedwali Na. 45: Ongezeko la gharama kutokana na kutofanya uchunguzi wa hali ya uchakavu ........................................................... 102
Jedwali Na. 46: Ongezeko la gharama kutokana na usanifu hafifu kwenye ujenzi wa soko la mwanza ........................................................ 103
Jedwali Na. 47: Nondo zilizolipwa bila ya kubainisha uzito na unene kwa kila aina ya nondo ............................................................. 104
Jedwali Na. 48: Makutano ya barabara yanayoongozwa na askari wa usalama barabarani.............................................................. 108
Jedwali Na. 49: Hali ya idadi inayohitajika ya alama za barabarani.......... 110
Jedwali Na. 50: Uchambuzi wa wizi wa alama za barabara .................... 112
Jedwali Na. 51: Athari za uratibu duni baina ya wadau wa miradi........... 116
Jedwali Na. 52: Uchambuzi wa usanifu wa uwezo wa barabara kuhimili mizigo ........................................................................... 117

Jedwali Na. 53: Athari za utafiti na usanifu wa miundombinu ya maji....... 119
Jedwali Na. 54: Athari za uchunguzi hafifu wa udongo na vifaa............... 121
Jedwali Na. 55: Marekebisho ya bei kwa vifaa vipya ............................ 126
Jedwali Na. 56: Malipo ya kazi zilizopimwa...................................... 127
Jedwali Na. 57: Adhabu kwa mabadiliko ya wafanyakazi waandamizi........ 128
Jedwali Na. 58: Muda wa kutolewa kkataba kuanzia tarehe za mwisho za uwasilishaji wa zabuni............................................................ 133
Jedwali Na. 59: Marekebisho ya bei kutokana na kuchelewa kumshirikisha mkandarasi ................................................................... 133
Jedwali Na. 60: Hali ya matumizi ya fedha za mkopo........................... 134
Jedwali Na. 61: Kiasi kinachodaiwa kutokana na kuchelewa hati za malipo 135

# ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. I: Hati za Ukaguzi Zilizotolewa Mwaka wa Fedha 2023/2024 .................................................................................. 137
Kiambatisho Na. II: Fedha Zilizotumika Kinyume na Maelekezo ya Mradi .... 158
Kiambatisho Na. III: Shughuli Zilizowekwa kwenye Bajeti Kutofanyika....... 160
Kiambatisho Na. IV: Orodha ya Miradi Iliyoathiriwa na Ucheleweshaji wa Utoaji wa Fedha ...................................................................... 161
Kiambatisho Na. V: Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo bila Kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira ................................................................. 162
Kiambatisho Na. VI: Taarifa ya Mkataba wa Miradi ya Barabara kwa ajili ya Ufungaji na Matengenezo ya Alama za Barabarani.............................. 163
Kiambatisho Na. VII: Taarifa za Miradi ya Barabara Iliyokaguliwa............. 165
Kiambatisho Na. VIII: Muhtasari wa Mkataba wa Mradi.......................... 167
Kiambatisho Na. IX: Sababu za kuongeza muda na idadi ya siku zilizoongezwa .................................................................................. 167
Kiambatisho Na. X: Kiwango cha Malipo Yaliyocheleweshwa Kulipa Hati ya Malipo ya Mkandarasi ............................................................... 168
Kiambatisho Na. XI: Malipo ya Ziada kwa Wafanyakazi wa Washauri ......... 169
Kiambatisho Na. XII: Takwimu za Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Pangani na Barabara Zake .................................................................... 170

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ADF | Mfuko wa Maendeleo ya Afrika |
| AfDB | Benki ya Maendeleo Afrika |
| AUWSA | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha |
| BoQ | Makadirio ya Gharama za Ujenzi |
| BRT | Mradi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka |
| CDC | Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani |
| DAWASA | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam |
| DIT | Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam |
| DLI | Viashiria vya Ugawaji wa Fedha |
| EASTRIP | Mradi wa Kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki |
| EIA | Tathmini ya Athari za Mazingira |
| EPforR II | Programu ya Matokeo Makubwa Sasa katika Elimu Awamu ya II |
| ESIA | Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii |
| ESPJ | Mradi wa Uwezeshaji Kupitia Ujuzi |
| GAVI | Shirika la Kimataifa Linalohusika na Utaratibu wa Chanjo |
| GCC | Masharti ya Jumla ya Mkataba |
| GoT | Serikali ya Tanzania |
| GPSA | Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini |
| HEET | Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi |
| ICT | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| IDA | Jumuiya ya Maendeleo ya Kimataifa |
| IFAD | Mfuko wa Kimataifa wa Maedeleo ya Kilimo |
| IFRS | Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha |
| IMF | Shirika la Fedha la Kimataifa |
| INTOSAI | Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi |
| IPC | Madai ya Malipo ya Wakandarasi na Washauri Elekezi |
| IPSAS | Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma |
| ISA | Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu |
| ISO | Shirika la Kimataifa la Kuweka Viwango |
| ISSAIs | Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi |
| JICA | Shirika la Maendeleo la Japani |
| JNHPP | Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere |
| KfW | Benki ya Maendeleo ya Ujerumani |
| KOICA | Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea |
| LANES | Mradi wa Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu |
| LGAs | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| MDAs | Wizara, Idara, na Wakala |

| | |
|---|---|
| MoEST | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia |
| MoF | Wizara ya Fedha |
| MoH | Wizara ya Afya |
| MoU | Hati ya Makubaliano |
| MoW | Wizara ya Maji |
| MWAUWASA | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza |
| NAO | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi |
| NBS | Ofisi ya Taifa ya Takwimu |
| NEMC | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira |
| NeST | Mfumo Mpya wa Kielekitroni wa Ununuzi wa Umma |
| NGOs | Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| NIRC | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji |
| NM-AIST | Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela |
| NUFFIC | Shirika la Uholanzi la Kuendeleza na Kueneza Elimu ya Kimataifa |
| OPEC | Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta |
| PAA | Eneo la Utekelezaji wa Mradi |
| PAP | Watu Wanaoathiriwa na Mradi |
| PERFAR | Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI |
| PMA | Tathmini ya Usimamizi wa Miradi |
| PMU | Kitengo cha Ununuzi na Ugavi |
| Po-RALG | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PPC | Tume ya Ununuzi wa Umma |
| PPF | Mfumo wa Ununuzi wa Umma |
| PPP | Ushirikiano wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi |
| PPR | Kanuni za Ununuzi wa Umma |
| PPRA | Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma |
| PSSN II | Mtandao wa Usalama wa Jamii wa Uzalishaji Awamu ya II |
| REA | Wakala wa Nishaji Vijijini |
| REF | Mfuko wa Nishati Vijijini |
| RISE | Kituo cha Miundombinu ya Maji na Nishati Endelevu kwa Matumizi ya Baadaye |
| RUWASA | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini |
| SACCOs | Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika |
| SCC | Masharti Maalumu ya Mkataba |
| SEQUIP | Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari |
| SGR | Mradi wa Reli ya Kisasa |
| SIDA | Shirika la Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa la Uswidi |
| SRWSSP | Programu ya Usambazaji wa Huduma za Maji Safi Vijijini |
| TANAPA | Shirika la Hifadhi za Taifa |
| TANePS | Mfumo wa Kielekitroni wa Ununuzi wa Umma |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |

| | |
|---|---|
| TANIPAC | Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania |
| TANROADS | Wakala wa Barabara Tanzania |
| TARURA | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini |
| TASAF III | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya III |
| TAZARA | Shirika la Reli Tanzania na Zambia |
| TBS | Ofisi ya Taifa ya Takwimu |
| TCCL | Shirika la Mawasiliano Tanzania |
| TCRA | Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania |
| TCU | Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania |
| TECU | Kitengo cha Ushauri cha Uhandisi cha Wakala wa Barabara Tanzania |
| TFCS | Mfumo wa Uuzaji Tiketi na Ukusanyaji wa Nauli |
| TFRS1 | Kiwango cha Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha cha Tanzania Namba 1 |
| TMA | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania |
| TPDC | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TRC | Shirika la Reli Tanzania |
| TSMP II | Mpango Kabambe wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Nchini Awamu ya II |
| TSSP | Programu ya Msaada wa Sekta ya Usafiri |
| TTCL | Shirika la Simu Tanzania |
| Sh. | Shilingi ya Tanzania |
| UNDP | Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa |
| URT | Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania |
| USAID | Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa |
| USD | Dola ya Marekani |
| UVIKO 19 | Ugonjwa wa Virusi vya Korona |
| VAT | Kodi ya Ongezeko la Thamani |
| WASH | Mradi wa Huduma za Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni |
| WSDP | Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji |

## SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI



Nina furaha kuwasilisha Ripoti ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioisha tarehe 30 Juni 2024. Ripoti hii inatoa tathmini ya kina kuhusu taarifa za matumizi ya fedha, ufanisi wa utekelezaji na kiufundi kwa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na taasisi za umma. Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Ukaguzi wa Umma (ISSAI) ikijumuisha ukaguzi wa taarifa 332 za fedha na kaguzi 12 za kiufundi katika sekta muhimu, ikiwa ni pamoja na sekta ya nishati, usafirishaji, maji, mawasiliano, na ujenzi.

Napenda kuipongeza Serikali, chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kujitolea kwake bila kuchoka kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma. Pia, ninatoa shukrani kwa watekelizaji wa miradi na taasisi zinazosimamia kwa ushirikiano wao na utoa taarifa muhimu zilizosaidia katika kuandaa ripoti hii.

Matokeo na mapendekezo yaliyoainishwa katika ripoti hii ni ya manufaa katika kuimarisha utawala bora, kuongeza uwajibikaji, na kuboresha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma katika utekeleza miradi. Pamaja na kwamba utekelezaji wa miradi mingi unaonyesha mwenendo mzuri wa usimamizi wa fedha na kiutendaji, ukaguzi ulibaini mapungufu kadhaa yanayohitaji kushughulikiwa. Ikiwa ni pamoja na kasoro katika ununuzi, upungufu katika matumizi ya bajeti, ucheleweshaji katika kutekeleza miradi, na udhaifu katika usimamizi unaathiri matokeo ya jumla ya miradi.

Kinacholeta wasiwasi ni kurudiarudia kwa mapendekezo ya ukaguzi ambayo hayakushughulikiwa kikamilifu, usimamizi usioridhisha wa mikataba, na matumizi ya fedha katika baadhi ya miradi. Upotevu wa fedha unaojirudia, ucheleweshaji wa malipo ya fidia kwa waathirika wa miradi, na mapungufu katika kuzingatia athari za kimazingira zinahitaji hatua madhubuti za usimamizi unaorithisha.

Ninawasihi watekelezaji wa miradi, na taasisi zinazoshughulikia usimamizi wa miradi kuchukua hatua madhubuti katika kushughulikia mapungufu yaliyobainika na kuhakikisha kuwa fedha za miradi zinatumika kwa ufanisi na

manufaa ya taifa. Pia, ninalishauri Bunge na wadau wengine kutumia taarifa iliyo katika ripoti hii ili kuimarisha mifumo ya usimamizi, na kudumisha uwazi katika utekelezaji wa miradi.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kutekeleza jukumu lake la ukaguzi kwa viwango vya juu zaidi vya utaalamu na uhuru, kuhakikisha kwamba rasilimali za umma zinatumiwa kwa ufanisi na kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mwisho, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa kwa utaalamu wao na kujitolea katika kutekeleza jukumu hili la kikatiba.

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# MUHTASARI

Taarifa hii inaelezea matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na taasisi za umma nchini Tanzania kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Ukaguzi huu ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi wa Umma (ISSAI) na ulijumuisha ukaguzi wa fedha na uzingatiaji wa sheria kwa miradi 332 pamoja na ukaguzi wa kiufundi kwa miradi 12 katika sekta mbalimbali, zikiwemo nishati, usafirishaji, maji, mawasiliano, na ujenzi.

Ukaguzi wa miradi 332 ulifanywa kwa kutumia mbinu mseto inayojumuisha ukaguzi wa fedha na ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria ili kuhakikisha uwazi na usimamizi bora wa rasilimali za umma. Ukaguzi huu uliangazia uandaaji wa taarifa za fedha, uzingatiaji wa kanuni na sheria, pamoja na ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa ndani. Aidha, ukaguzi wa kiufundi wa miradi 12 ulifanyika kwa kutumia mbinu ya ukaguzi wa wakati halisi (real-time audit) ili kutathmini ufanisi na tija ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa kuwa ukaguzi wa kiufundi hauzingatii viwango vya ukaguzi wa fedha, hakuna hati ya ukaguzi zilizotolewa kwa ukaguzi huu.

## A. UKAGUZI WA FEDHA NA UKAGUZI WA UZINGATIAJI WA SHERIA

### Hati za Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, kati ya miradi 332 iliyokaguliwa, miradi 331 (sawa na 99.7%) iilipata hati isiyo na mashaka, ikionesha ufuataji mzuri wa viwango vya utoaji wa taarifa za kifedha. Hata hivyo, hati yenye shaka ilitolewa kwa mradi wa Mfuko wa Afya unaotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, kutokana na upungufu wa nyaraka za uthibitisho na malipo yasiyothibitishwa. Hili linaonesha kwamba bado kuna changamoto katika usimamizi wa fedha katika mfuko huu.

### Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Miaka ya Iliyopita

Katika mwaka huu wa fedha 2023/24 kulikuwa na jumla ya mapendekezo 3,083 ya ukaguzi wa miaka iliyopita, ambapo kati ya hayo, mapendekezo 1,394 (sawa na 45%) yaliyotekelezwa kikamilifu. Mapendekezo 789 yalikuwa katika hatua ya utekelezaji, huku mapendekezo 477 hayakuwa yametekelezwa kabisa. Kuendelea kucheleweshа utekelezaji wa mapendekezo haya kunaongeza hatari za kifedha, kiutendaji, na za kisheria, jambo linaloashiria udhaifu wa muda mrefu katika usimamizi wa taasisi hizi katika kutekeleza mapendekezo.

## Usimamizi wa Fedha na wa Matumizi

Katika mwaka wa fedha uliokaguliwa, jumla ya Shilingi trilioni 8.44 zilikuwepo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kiasi hiki kinajumuisha bakaa ya miaka iliyopita na fedha zilizopokelewa ndani ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi trilioni 5.93 zilitumika, huku Shilingi trilioni 2.50 zilikua hazijatumika hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024.

Tathmini ya utendaji wa kifedha ilibaini changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na fedha za mradi kiasi cha Shilingi milioni 635.44 zilizokopwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia bila kurejeshwa. Pia, malipo ya Shilingi milioni 892.92 yalifanywa bila ya kazi iliyokamilika kuthibitishwa na mhandisi mshauri. Katika ukaguzi, nilibaini pia kuwa malipo ya jumla ya Shilingi bilioni 2.01 yalifanyika kwa njia ya fedha taslimu kinyume na taratibu. Vilevile, malipo ya fidia kwa Watu Walioathiriwa na Miradi (PAPs) kiasi cha Shilingi bilioni 24.75 bado hazijalipwa, hali inayosababisha ucheleweshaji wa miradi na ongezeko la gharama za utekelezaji.

## Usimamizi wa Bajeti

Nilibaini mapungufu katika usimamizi wa bajeti, ikiwa ni pamoja na shughuli zilizobajetiwa zenye thamani ya Shilingi bilioni 428.46 hazikutekelezwa. Aidha, kucheleweshwa kwa utoaji wa fedha kiasi cha Shilingi bilioni 427.36 kutokana na changamoto za ndani kuliathiri utekelezaji wa miradi.

Vilevile, miradi haikufanikisha Utoaji wa Fedha unaohusiana na matokeo (Disbursement Linked Results – DLRs), jambo lililosababisha kiasi cha Shilingi bilioni 141.76 kutotolewa, hali iliyochelewesha utekelezaji wa miradi na utoaji wa matokeo yaliyotarajiwa.

## Usimamizi wa Ununuzi

Nilibaini changamoto kubwa katika uzingatiaji wa taratibu za ununuzi, ikiwa ni pamoja na manunuzi yenye thamani ya Sh. 4.49 bilioni yaliyofanyika nje ya Mfumo wa kitaifa wa Ununuzi Kielektroniki (NeST). Aidha, manunuzi kutoka kwa wasambazaji wasioidhinishwa yalifikia Shilingi bilioni 3.1, hali inayodhoofisha uwazi na uwajibikaji. Vilevile, kulikuwa na manunuzi yenye thamani ya Shilingi bilioni 133.24 yaliyokuwa katika mpango wa mwaka wa manunuzi lakini hayakutekelezwa, jambo lililosababisha ucheleweshaji wa utoaji wa huduma na maendeleo ya miundombinu.

### Usimamizi wa Mikataba na Maendeleo ya Miradi

Mikataba yenye thamani ya Shilingi bilioni 13.45 ilisainiwa bila kupitia uhakiki wa kisheria, hali inayoongeza hatari za kisheria na kifedha. Pia, kulikua riba ya Shilingi bilioni 1.29 iliyotokana na ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi. Aidha, malipo ya awali yenye jumla ya Shilingi bilioni 13.79 yalifanyika bila dhamana, jambo linaloongeza hatari za kifedha kwa serikali ikiwemo upotevu wa fedha hizo iwapo mkandarasi atashindwa kutekeleza wajibu wake.

Vive vile, shule za msingi 35 na shule za sekondari 148 zilijengwa kwenye ardhi isiyopimwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 125.14, hali inayoweza kusababisha migogoro ya ardhi na changamoto za uendelevu wa miradi.

## B. Ukaguzi wa Kiufundi

Nilifanya ukaguzi 12 za kiufundi. Matokeo ya kaguzi za kiufundi yametolewa kama ifuatavyo:

### Mradi wa Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP)

Ukaguzi wa kiufundi wa Mradi wa Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) umebaini mapungufu katika mpango, usimamizi wa mkataba, na utekelezaji wa wajibu wa kijamii wa kampuni.

Mradi huu haukuwa na Mpango wa dharura wa kuzuia na kukabiliana na maafa kwa jamii zilizo kando ya bwawa, hali ambayo inafanya wakazi wa maeneo hayo kuwa katika mazingira hatarishi.Vilevile, katika usimamizi wa mikataba TANESCO liliajiri kampuni ya kisheria bila kupata idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, jambo ambalo lilisababisha uwakilishi dhaifu wa kisheria katika kesi ya Bodi ya Usuluhishi wa Migogoro ya Mikataba. Aidha, jumla ya Shilingi milioni 752.87 zililipwa kwa kampuni hiyo bila kukata kodi ya zuio ya Shilingi milioni 143.94. Aidha, fidia ya ucheleweshaji ya Shilingi bilioni 327.93 haikukatwa kutoka kwa mkandarasi, jambo lililopunguza uwajibikaji wa kimkataba.

### Miradi ya Umeme Vijijini

REA alishindwa kufanya utafiti wa mahitaji umeme kama inavyotakiwa na badala yake ilitegemea takwimu zilizopitwa na wakati, hali iliyosababisha makadirio yasiyo sahihi ya mahitaji ya umeme. Pia, kulikuwako na ongezeko la gharama ya Shilingi bilioni 15.34 kutokana na maandalizi hafifu ya mchanganuo wa bei za vipande vya 1 hadi 6.

Vilevile, transfoma zenye uwezo mdogo kuliko zilizoainishwa kwenye upembuzi yakinifu zilinunuliwa na kufungwa bila kufanya tathmini ya mahitaji ya umeme, hali inayoweza kusababisha upungufu wa miundombinu na matatizo ya kukatika kwa umeme. Pia, kulikuwa na mabadiliko nje ya wigo wa mradi, yaliyosababisha kupelekwa kwa umeme katika vijiji ambavyo awali havikuwa vimeorodheshwa kwenye mkataba.

### Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano

Ukaguzi wa kiufundi wa ujenzi wa minara ya mawasiliano chini ya Mfuko wa Ufikiaji Huduma za Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umebaini mapungufu katika upangaji, ununuzi, usimamizi wa mikataba, na uhakikisho wa ubora. Nilibaini kuwa UCSAF ilitumia Shilingi bilioni 4.28 kwa kujenga minara ya mawasiliano katika maeneo ambayo tayari yalikuwa na huduma hiyo na Shilingi bilioni 5.76 katika maeneo ambayo awali hayakuwa yameainishwa kuwa na uhitaji wa minara. Pia, UCSAF ilitoa ruzuku ya Shilingi bilioni 7.17 zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa bila maelezo ya kutosha. Aidha, fidia ya Shilingi bilioni 3.80 kwa ucheleweshaji wa miradi haikudaiwa, hali iliyopunguza uwajibikaji na ufanisi wa utekelezaji wa mradi.

Vilevile, 42% ya maeneo yaliyokamilika hayakufanyiwa vipimo vya awali vya kukubalika kwa matumizi. Aidha, kati ya maeneo yaliyopimwa, 46% yalishindwa kufikia viwango vya chini vya upatikanaji wa simu na kiwango cha mafanikio ya mawasiliano, hali inayohatarisha ufanisi wa mradi na manufaa yake kwa wananchi.

### Udhibiti na Ufuatiliaji wa Tathmini ya Athari za Mazingira

Ukaguzi wa kiufundi wa usimamizi na ufuatiliaji wa Tathmini za Athari za Mazingira (EIA) na Mipango ya Usimamizi wa Mazingira (EMP) uliofanywa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) katika sekta ya ujenzi na madini umebaini mapungufu katika uzingatiaji wa sheria, ufuatiliaji, na utekelezaji wa masharti ya mazingira.

NEMC ilishindwa kufuatilia kwa ufanisi taratibu za usajili na upitishaji wa tathmini za mazingira, ambapo miradi mikubwa kama Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka na Daraja la John Pombe Magufuli ilianza kutekelezwa bila vyeti vya tathmini ya athari za mazingira, hali ambayo ilisababisha hatari za kimazingira ambazo hazikufanyiwa tathmini wala kuwekwa mikakati ya udhibiti.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa katika miradi mitano kati ya minane iliyokaguliwa, kulikuwa na upungufu wa takwimu za awali za mazingira, ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa uchambuzi wa metali nzito katika ubora wa maji katika Mgodi

wa Almasi wa Williamson na Mradi wa Mtandao Mpya wa Maji jijini Arusha. Hali hii ilihatarisha uwezo wa kufuatilia athari za mazingira na kupanga hatua za kudhibiti madhara.

Mchakato wa mapitio ya tathmini za athari za mazingira nao ulibainika kuwa na mapungufu, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa uhakiki wa kina wa maeneo ya miradi, ushirikishwaji mdogo wa wadau, pamoja na hatua dhaifu za kupunguza athari za mazingira, hali iliyoongeza hatari ya uharibifu wa mazingira.

Zaidi ya hayo, ufuatiliaji wa mazingira baada ya kutolewa kwa vyeti vya EIA haukuwa wa kutosha, ambapo NEMC lilishindwa kuthibitisha utekelezaji wa hatua za kudhibiti uchafuzi wa mazingira, kufuatilia usimamizi wa taka ngumu na hatarishi, au kuhakikisha kuwa tathmini za mazingira za kila mwaka zinafanyika kama inavyotakiwa. Matokeo yake ni kuwepo kwa kumwagika kwa mafuta na udhibiti hafifu wa mmomonyoko wa udongo katika maeneo kadhaa ya miradi.

Vilevile, udhibiti na ufuatiliaji wa mipango ya kufunga miradi haukuwa wa kuridhisha, kwani hakuna mradi wa ujenzi uliokuwa na mkakati rasmi wa kuondoa miundombinu baada ya mradi kukamilika. Aidha, urejeshaji wa mazingira kwa awamu katika miradi ya uchimbaji madini ulikuwa umecheleweshwa au haukutekelezwa ipasavyo, hali iliyoongeza hatari ya uharibifu wa mazingira wa muda mrefu.

### Usambazaji wa Maji Vijijini chini ya RUWASA

Ukaguzi wa kiufundi wa Wakala wa Usambazaji wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RUWASA) umebaini mapungufu katika upangaji wa miradi, ununuzi, usimamizi wa mikataba, na uhakikisho wa ubora, hali iliyohatarisha ufanisi na uendelevu wa miradi ya maji vijijini.

Katika ukaguzi, nimebaini tathmini ya vyanzo vya maji haikufanyika kwa kina, ambapo ukaguzi wa mara moja tu haukuweza kubaini athari ya mabadiliko ya msimu katika ubora na upatikanaji wa maji. Matokeo yake, miradi ya Morong'anya na Kemondo-Maruku ilitegemea mbinu zisizofaa za uchujaji wa maji, huku miradi ya Kigwa-Uyui na Igogo-Igurubi ikitegemea miundombinu ya mabomba ambayo haikusanifiwa kwa ajili ya upanuzi wa huduma, hali inayosababisha hatari ya muda mrefu kwa upatikanaji wa maji. Aidha, kujumuisha kipindi cha utekelezaji wa mradi ndani ya miaka 20 ya miradi kulipunguza muda wa matumizi ya miundombinu hiyo kabla ya kuhitaji ukarabati mkubwa.

Aidha, mikataba 14 kati ya 15 iliingiwa bila kufanyika kwa uhakiki wa kina wa makandarasi, jambo lililosababisha ucheleweshaji wa hadi miaka mitano na gharama za ziada za Shilingi bilioni 1.17 kutokana na kuvunjwa kwa mikataba.

Pia, ushindani usioridhisha katika zabuni ya mradi wa Morong'anya ulisababisha gharama zisizotarajiwa za Shilingi bilioni 1.26 kutokana na upungufu wa vipengele muhimu katika makadirio ya gharama za ujenzi.

Udhaifu katika usimamizi wa mikataba ulisababisha hasara ya Shilingi milioni 493.08 kutokana na uvunjaji wa mikataba usiozingatia taratibu, pamoja na ongezeko la gharama la Shilingi bilioni 4.04 kutokana na mapungufu katika usanifu wa miradi. Aidha, ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi ulisababisha riba ya Shilingi milioni 711.79, jambo lililoongeza mzigo wa kifedha kwenye miradi husika.

Vilevile, matatizo ya usimamizi wa ubora, yakiwemo ufungaji usiofaa wa mabomba, ujazaji udongo usiotosha, na matumizi ya malighafi zisizofaa kwa ajili ya kujaza udongo, yameongeza uwezekano wa kuwa na miundombinu dhaifu ya maji. Hali hii inahitaji maboresho ya haraka katika usimamizi, upangaji, na uzingatiaji wa viwango vya kiufundi ili kuhakikisha ufanisi na uendelevu wa miradi ya maji vijijini.

### Ujenzi na Matengenezo ya Miundombinu ya Majitaka na Usafi wa Mazingira

Ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya maji taka na usafi wa mazingira inayotekelezwa chini ya Wizara ya Maji na Mamlaka za Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira (WSSAs) umebaini mapungufu katika upangaji wa miradi, ununuzi, usimamizi wa mikataba, na uangalizi wa fedha.

Ubunifu wa kituo cha kutibu maji taka cha Mbezi Beach haukuzingatia viwango vya mazingira. Mradi uliweka kiwango cha taka kinachoruhusiwa katika majitaka yaliyochujwa (Chemical Oxygen Demand) kuwa 125 mg/L ambacho kinazidi kiwango kinachoruhusiwa cha 60 mg/L kwa asilimia 108.33. Hali hii inahatarisha uchafuzi wa vyanzo vya maji, jambo linaloweza kuwa na athari mbaya kwa mazingira.

Tathmini zisizokamilika za upembuzi yakinifu zilisababisha agizo la mabadiliko ya kazi (variation order) lenye thamani ya Shilingi bilioni 1.66 kwa miradi ya maji taka ya Area C na Area D jijini Dodoma kwa ajili ya nyumba ambazo awali hazikujumuishwa. Hali hii imeongeza hatari ya kujaa kwa mifumo ya maji taka kutokana na ukuaji wa mahitaji ambao haukuzingatiwa katika usanifu wa awali.

Aidha, malipo ya ziada ya Shilingi bilioni 1.60 yalilipwa kwa miradi ya Ilemela na Babati kwa kazi ambazo hazikufanyika, kutokana na kuthibitishwa kimakosa kwa kazi zisizotekelezwa. Aidha, ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi katika miradi mitano ulisababisha gharama ya riba ya Shilingi milioni 273. Miradi ya Babati na Dodoma ndiyo iliyokuwa na ucheleweshaji mkubwa wa utekelezaji, ikiwa na wastani wa siku 252 na 161 za kuchelewa, mtawalia. Ucheleweshaji huu ulitokana kuchelewa kupata fedha kutoka Wizara ya Fedha.

### Mradi wa Bwawa la Kidunda

Ukaguzi huu ulilenga kutathmini ufanisi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) katika upangaji, usanifu, na utekelezaji wa Mradi wa Bwawa la Kidunda ili kukidhi mahitaji ya maji na kuboresha huduma za usafi wa mazingira.

Nilibaini kuwa hakukuwa na ujumuishaji wa mabwawa ya kuzuia mashapo katika usanifu wa mradi, hali ambayo imeongeza hatari ya mkusanyiko wa mchanga, kupungua kwa uwezo wa hifadhi ya maji, na kuongezeka kwa gharama za matengenezo. Upungufu huu ulitokana na utafiti wa awali wa upembuzi yakinifu usio wa kina.

Pia, nilibaini ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi kwa kati ya siku 16 hadi 299, hali ambayo inaweza kusababisha malipo ya riba yasiyo ya lazima. Aidha, mabadiliko ya kazi yasiyoidhinishwa yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.57 yalibainika katika Hati ya Malipo (IPC) Na. 5 kutokana na udhaifu katika ufuatiliaji wa gharama na taratibu za uthibitishaji.

Vilevile, DAWASA ililipa fidia ya ziada ya Shilingi bilioni 4.02 baada ya kufanya tathmini upya. Hii ilionesha kuwa jumla ya Shilingi bilioni 9.07 zililipwa kama fidia, na kusababisha ongezeko la gharama la Shilingi bilioni 5.24, kwani bajeti ya awali ilikuwa Shilingi bilioni 3.83.

### Ukarabati na Ujenzi wa Masoko na Vituo vya Mabasi

Ukaguzi wa kiufundi wa ukarabati na ujenzi wa Soko la Kariakoo, Soko Kuu la Mwanza, na Kituo cha Mabasi cha Nyamhongolo umebaini mapungufu katika upangaji wa miradi, usanifu, na usimamizi wa mikataba, hali iliyosababisha ongezeko la gharama na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi.

Kutokuwepo kwa tathmini ya kina ya hali ya majengo katika masoko ya Kariakoo na Mwanza kulisababisha kutofafanuliwa kwa wigo wa miradi, hali iliyopelekea mabadiliko yenye thamani ya Shilingi milioni 757.02. Mapungufu katika usanifu wa Soko Kuu la Mwanza yalisababisha kazi za ziada zenye thamani ya Shilingi

bilioni 1.96 kutokana na mahitaji muhimu ya mradi kutokujumuishwa katika hatua za awali.

Pia, malipo ya Shilingi bilioni 9.87 kwa upauaji wa nondo bila kubainisha vipimo vya nondo hizo, hali iliyoongeza hatari ya kupanda kwa gharama zisizo halisi. Aidha, Shilingi milioni 766.90 zililipwa kwa washauri kama gharama za kurejesheka bila nyaraka za uthibitisho, jambo linaloashiria udhaifu katika udhibiti wa fedha.

Ucheleweshaji wa miradi kwa miezi 13 katika Soko la Kariakoo na miezi 44 katika Soko Kuu la Mwanza ulisababisha madai ya washauri wa Shilingi bilioni 1.35 kwa gharama za usimamizi wa muda uliosongezwa. Ucheleweshaji huu ulitokana na idhini zilizocheleweshwa, malipo yaliyokawia, pamoja na ongezeko la wigo wa miradi.

### Ufungaji na Matengenezo ya Alama za Barabarani na Taa za Kuongoza Magari

Ukaguzi wa kiufundi wa ufungaji na matengenezo ya vifaa vya barabarani na ishara za mawasiliano ya barabara uliofanywa kwa TANROADS na TARURA umebaini mapungufu katika upangaji wa miradi, usimamizi wa mikataba, na matengenezo, hali ambayo imeathiri kwa kiasi kikubwa usalama wa barabara na ufanisi wa mfumo wa usafirishaji.

Miundombinu ya alama za barabarani katika makutano muhimu jijini Dar es Salaam imepitwa na wakati, hali iliyosababisha hitaji la udhibiti wa foleni kwa mikono kupitia askari wa usalama barabarani. Aidha, ukosefu wa bajeti ya kutosha umekwamisha juhudi za matengenezo, ambapo Shilingi bilioni 1.8 hutengwa kwa mwaka ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Shilingi bilioni 200.

Pia, nilibaini upungufu wa alama za barabarani, ambapo Barabara ya Bagamoyo ina upungufu wa taa za barabarani kwa 73%, ilhali mistari ya barabarani iliyofifia na ukosefu wa alama za barabara vikiongeza hatari za ajali. Udhibiti wa ubora haukuwa wa kuridhisha, kwani rangi za alama za barabarani hazikupimwa kama inavyotakiwa, hali inayohatarisha uimara wake kwa muda mrefu.

Uharibifu wa vifaa vya barabarani kwenye Barabara ya Tabora-Nzega na barabara za Mji wa serikali Dodoma umesababisha hasara ya Shilingi milioni 170.48, huku udhaifu wa hatua za ulinzi ukichangia ongezeko la wizi wa vifaa hivyo.

## Hitimisho

Ukaguzi wangu umebaini maeneo muhimu yanayohitaji hatua za haraka za usimamizi ili kuboresha uzingatiaji wa kanuni, kuongeza ufanisi wa usimamizi wa miradi, na kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali. Kuimarisha udhibiti wa ndani, kuongeza uratibu kati ya wadau, na kuboresha ufuatiliaji wa miradi nitakuwa muhimu katika kushughulikia changamoto zilizobainika ili kufanikisha malengo ya miradi kwa ufanisi.




# SURA YA KWANZA

## Utangulizi wa Jumla

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha maelezo ya awali kuhusu ukaguzi wa miradi. Ukaguzi huu ulitathmini usimamizi wa fedha, mfumo wa udhibiti, na uzingatiaji wa sheria katika miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Taarifa hii imegawanyika katika sura 18, kila moja ikilenga kipengele mahususi, ikijumuisha utekelezaji wa sheria za ununuzi, usimamizi wa mapato na fedha, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa bajeti, na kaguzi za kiufundi katika miradi ya maendeleo. Aidha, inatoa mapendekezo ya kuboresha utendaji kazi wa taasisi hizi, kuimarisha uwazi na uwajibikaji, na kukuza utawala bora

## 1.2 Mamlaka

Ukaguzi huu ni sehemu ya mamlaka na majukumu ya kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoelezwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418. Lengo lilikuwa kuhakikisha taasisi zinazotekeleza miradi zinafanya kazi kwa ufanisi, kuchangia katika Uchumi, na kutoa huduma bora kwa wananchi.

## 1.3 Madhumuni ya Ukaguzi

Ukaguzi ulilenga kutoa maoni huru iwapo taarifa za fedha zilitayarishwa kwa mujibu wa mfumo unaokubalika wa utoaji taarifa za fedha, kwa kuzingatia mambo yote muhimu. Aidha, ulilenga kutathmini uzingatiaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma katika miradi ya maendeleo, na Sheria ya Bajeti, kanuni na miongozo. Ukaguzi pia ulilenga kutathmini tija na ufanisi wa miradi ya maendeleo katika kusimamia fedha za umma na kutoa huduma kwa wananchi.

## 1.4 Mawanda ya Ukaguzi

Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, aina tatu za ukaguzi zilifanyika kwenye miradi ya maendeleo, ambazo ni ukaguzi wa hesabu, uzingatiaji wa sheria, na ukaguzi wa kiufundi. Taarifa 332[1] za ukaguzi wa fedha zilitolewa zikilenga mifumo ya usimamizi wa fedha, udhibiti, na uandaaji wa taarifa za fedha,

[1] Jumla hiyo haijumuishi taarifa 11 kutoka kwa akaunti za kuhifadhia fedha za miradi (holding accounts) ambayo hutumiwa kuhamishia fedha kwenda kwenye miradi husika. Hakuna shughuli za miradi zinazofanywa kwenye akaunti hizi, hata hivyo maoni ya ukaguzi yaliyotolewa kwenye akaunti za kuhifadhia fedha za miradi ni kwa madhumuni ya kutoa maoni ya ukaguzi kwa wafadhili kuhusu usalama wa fedha hizo.

ambao pia ulitathmini uzingatiaji wa sheria za ununuzi na usimamizi wa bajeti. Aidha, kaguzi 12 za kiufundi zilifanyika katika sekta mbalimbali kwenye miradi ya umeme, maji, ujenzi wa minara ya mawasiliano, ujenzi wa vituo vya mabasi na masoko, na ukaguzi wa mazingira. Mchanganuo wa miradi iliyokaguliwa unaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1** na **Jedwali Na. 2**.

### Jedwali Na. 1: Idadi ya miradi iliyokaguliwa kisekta 2023/24

| Na. | Sekta | Taarifa za Ukaguzi wa Kiufundi | Taarifa za Ukaguzi wa Fedha | Miradi Iliyokaguliwa | Watekeleza Miradi | Jumla ya Taarifa za Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilimo | - | 9 | 7 | 5 | 9 |
| 2 | Elimu | - | 33 | 10 | 23 | 33 |
| 3 | Nishati na Madini | 2 | 15 | 17 | 5 | 17 |
| 4 | Afya | - | 209 | 15 | 192 | 209 |
| 5 | Mawasiliano na Uchukuzi | 5 | 18 | 22 | 9 | 23 |
| 6 | Maji | 3 | 13 | 13 | 11 | 16 |
| 7 | Jamii | - | 11 | 11 | 10 | 11 |
| 8 | Miradi Mingine | 2 | 24 | 26 | 18 | 26 |
| **Jumla** | | **12** | **332** | **121** | **273** | **344** |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi wa fedha, kiufundi, na uzingatiaji sheria kwa mwaka wa fedha ulioshia tarehe 30 Juni 2024*

### Jedwali Na. 2: Ukaguzi wa kiufundi uliofanyika katika mwaka wa fedha 2023/24

| Na. | Sekta | Jina la taarifa ya kiufundi | Mtekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Nishati na Madini | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP) | Shirika la Umeme Tanzania |
| 2 | Nishati na Madini | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Miradi ya Kusambaza Umeme Vijijini | Wakala wa Nishati Vijijini |
| 3 | Mawasiliano na Uchukuzi | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano | Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote |
| 4 | Miradi Mingineyo | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Udhibiti na Ufuatiliaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) na Mipango ya Usimamizi wa Mazingira (EMP) katika Sekta za Ujenzi na Madini | Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira |
| 5 | Maji | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Utekelezaji wa Miradi ya Kusambaza Maji Vijijini chini ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini |
| 6 | Maji | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Majitaka na Usafi wa Mazingira katika Maeneo ya Mijini | Wizara ya Maji, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati, |

| Na. | Sekta | Jina la taarifa ya kiufundi | Mtekelezaji |
|---|---|---|---|
| | | | na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza |
| 7 | Maji | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Ujenzi wa Mabwawa ya Kidunda na Kipera | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam |
| 8 | Miradi Mingine | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Ujenzi wa Masoko na Vituo vya Mabasi chini ya Mradi wa Uendeleezaji wa Miji Mkakati wa Tanzania (TSCP) na Mradi wa Uendelezaji Miji na Manispaa (ULGSP) | Jiji la Dar es Salaam, Jiji la Mwanza, na Manispaa ya Ilemela |
| 9 | Mawasiliano na Uchukuzi | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Ufungaji na Matengenezo ya Alama za barabarani na Taa za Kuongozea Magari | Wakala wa Barabara Tanzania |
| 10 | Mawasiliano na Uchukuzi | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi | Wakala wa Barabara Tanzania |
| 11 | Mawasiliano na Uchukuzi | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Ujenzi wa Daraja la Pangani (urefu wa mita 500) na Barabara za Kuingilia (Sehemu ya Pili: Ujenzi wa Barabara ya Pangani-Bagamoyo) | Wakala wa Barabara Tanzania |
| 12 | Mawasiliano na Uchukuzi | Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Ubora wa Usanifu wa Kazi za Barabara | Wakala wa Barabara Tanzania |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi wa kiufundi kwa mwaka wa fedha ulioshia tarehe 30 Juni 2024*

## 1.5 Mbinu za Ukaguzi

Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI) na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISAs). Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alitumia mbinu mseto za ukaguzi, zikijumuisha kukagua kumbukumbu na nyaraka, kufanya usaili, na kutembelea maeneo ya utekelezaji wa miradi. Ukaguzi pia ulihusisha kupima mifumo ya udhibiti wa ndani ya miradi ya maendeleo na kutathmini utekelezaji wa sheria, kanuni, na sera husika.




# SURA YA PILI

## Hati za Ukaguzi

# HATI ZA UKAGUZI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na taasisi za umma katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Pia, inawasilisha mwenendo wa maoni niliyoyatoa katika taarifa za fedha kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo.

Maoni yaliyotolewa yanatokana na tathmini ya vielelezo vilivyopatikana katika kipindi chote cha ukaguzi, ili kutathmini endapo hesabu zilizingatia mifumo husika ya utayarishaji wa hesabu kama vile Viwango vya Kimataifa vya Hesabu (IFRSs), Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs), na Kiwango cha Taarifa za Fedha Tanzania Na. 1 (TFRS 1) katika mambo yote muhimu. Tathmini hii inazingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) 1200.

## 2.2 Aina za Hati za Ukaguzi

Aina za hati za ukaguzi ni hati inayoridhisha, hati yenye shaka, hati mbaya, na hati ya kushindwa kutoa maoni.

**Hati inayoridhisha** hutolewa wakati mkaguzi anaporidhika kuwa taarifa za fedha zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango na mfumo unaokubalika wa utayarishaji wa hesabu.

**Hati yenye shaka** hutolewa pale taarifa za fedha zinapoonekana zimeandaliwa kwa usahihi isipokuwa kuna suala/masuala ambayo yanaathiri usahihi kamili wa taarifa hizo za fedha. Hali hii inaweza kutokea baada ya mkaguzi kupata vielelezo vya kutosha na kuhitimisha kuwa kosa/makosa kwenye taarifa ya fedha yakiwekwa pamoja yana athari, lakini hayaathiri kwa ujumla usahihi wa taarifa za fedha.

Aidha, hati yenye shaka inaweza kutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kumwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho huo kwa ujumla wake haziathiri maeneo yote ya taarifa za fedha.

**Hati mbaya** hutolewa pale mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo vya kutosha kuthibitisha kuwa taarifa za fedha zina makosa, ambayo yakiwekwa pamoja yana athari kubwa na yanahusisha maeneo mengi katika taarifa za fedha.

**Kushindwa kutoa hati** hutokea pale mkaguzi asipopata uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za hesabu ambazo ni msingi wa kutoa hati. Mkaguzi anaweza kuhitimisha kuwa athari za makosa yanayoweza kuwapo kwenye taarifa za fedha ambazo hazijathibitishwa yanaweza kuwa makubwa na kuathiri sehemu zote za taarifa hizo. Mkaguzi huwa anashindwa kutoa hati katika hali chache sana zinazohusisha shaka, hadi kuhitimisha kuwa athari za makosa yanayoweza kuwapo kwenye hesabu ambazo hazijathibitishwa yanaweza kuwa makubwa na kuathiri maeneo yote ya taarifa hiyo.

## 2.3 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, nilikamilisha kaguzi 344 (kaguzi 332 za taarifa za fedha na kaguzi 12 za kiufundi) za miradi ya maendeleo inayotekelezwa na taasisi za umma[2], ambapo nilitoa hati 332 kwenye kaguzi za taarifa za fedha.

Kati ya hizo, 331 zilikuwa hati zinazoridhisha na moja ilikuwa hati yenye shaka kwenye mradi wa Mfuko wa Afya wa Pamoja uliotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. Hati hiyo ilitokana na uandaaji wa taarifa ya fedha yenye matumizi pungufu kutokana na kukosekana kwa nyaraka za kutosha kwenye malipo, malipo ya posho za kujikimu yasiyothibitshwa, na marekebisho kwenye kitabu cha fedha yasiyothibitishwa. **Jedwali Na. 3** linaonesha hati za ukaguzi zilizotelewa.

**Jedwali Na. 3: Muhtasari wa hati za ukaguzi 2023/24**

| Sekta | Hati zilizotolewa | | |
|---|---|---|---|
| | Hati zinazoridhisha | Hati zenye shaka | Jumla |
| Kilimo | 9 | - | **9** |
| Elimu | 33 | - | **33** |
| Nishati na Madini | 15 | - | **15** |
| Afya | 208 | 1 | **209** |
| Mawasiliano na Uchukuzi | 18 | - | **18** |
| Maji | 13 | - | **13** |
| Jamii | 11 | - | **11** |
| Miradi Mingine | 24 | - | **24** |
| **Jumla** | **331** | **1** | **332** |

***Chanzo:*** *Taarifa za fedha za Mwaka wa Fedha 2023/24*

## 2.4 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

**Jedwali Na. 4** linaonesha mwenendo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa watekelezaji wa miradi kwa miaka mitano mfululizo kuanzia Mwaka wa Fedha

[2] Isipokuwa taasisi moja ya kibinafsi ambayo ilitekeleza mradi mmoja uliofadhiliwa na UNDP

2019/2020 hadi 2023/2024. Ongezeko la hati zinazoridhisha kutoka 99% hadi 99.7% linatokana na uboreshaji katika maandilizi ya taarifa za fedha zinazoendana na Viwango vya Kimataifa vya Hesabu na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha.

**Jedwali Na. 4: Mwenendo wa hati za ukaguzi**

| Mwaka wa Fedha | Hati Zilizotolewa | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | Hati Inayoridhisha | | Hati Yenye Shaka | | |
| | Idadi | % | Idadi | % | |
| **2023/2024** | 331 | 99.7 | 1 | 0.3 | 332 |
| **2022/2023** | 296 | 99 | 3 | 1 | 299 |
| **2021/2022** | 287 | 99 | 3 | 1 | 290 |
| **2020/2021** | 293 | 100 | - | - | 293 |
| **2019/2020** | 275 | 95 | 15 | 5 | 290 |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi za Mwaka wa Fedha 2023/24 na taarifa kuu ya miradi ya maendeleo ya miaka iliyopita*

## 2.5 Hitimisho la Ukaguzi wa Usimamizi wa Bajeti na Ununuzi

Ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2023/24 ulitoa mahitimisho 634 katika maeneo makuu mawili. Maeneo hayo ni utekelezaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma, ambapo nimetoa maoni 319; na sheria na mwongozo wa bajeti, ambapo nimetoa maoni 315.

### 2.5.1 Hitimisho la Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria za Ununuzi

Katika mwaka wa fedha 2023/24, nimetoa mahitimisho 319 kuhusu utekelezaji wa sheria za ununuzi wa umma kwa watekelezaji wa miradi. Kati ya hayo, maoni 195 yanaonesha taasisi zilizingatia kikamilifu sheria za ununuzi huku maoni 124 yanaonesha kulikuwa na dosari katika utekelezaji wa sheria ya ununuzi kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 5**.

**Jedwali Na. 5: Hitimisho la uzingatiwaji wa sheria ya ununuzi**

| Sekta | Uzingatiaji Kikamilifu wa Sheria | Dosari katika Uzingatiaji wa Sheria na Miongozo | Jumla |
|---|---|---|---|
| Kilimo | 4 | 3 | **7** |
| Elimu | 15 | 18 | **33** |
| Nishati na Madini | 13 | 2 | **15** |
| Afya | 122 | 79 | **201** |
| Mawasiliano na Uchukuzi | 12 | 5 | **17** |
| Maji | 6 | 7 | **13** |
| Jamii | 6 | 4 | **10** |
| Miradi Mingine | 17 | 6 | **23** |
| **Jumla** | **195** | **124** | **319** |

***Chanzo:*** *Taarifa za fedha za Mwaka wa Fedha 2023/24*

### 2.5.2 Hitimisho la Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria za Bajeti

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, nimetoa mahitimisho 315 kuhusu uzingatiaji wa sheria na miongozo ya bajeti kwa watekelezaji wa miradi. Kati ya hayo, watekelezaji 246 wa miradi walizingatia sheria na miongozo ya bajeti na watekelezaji 69 walikuwa na dosari katika kuzingatia sheria na miongozo ya bajeti kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 6**.

**Jedwali Na. 6: Hitimisho la uzingatiwaji wa sheria za bajeti**

| Sekta | Uzingatiaji Kikamilifu wa Sheria ya Ununuzi | Dosari katika Uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi | Jumla |
|---|---|---|---|
| Kilimo | 6 | 5 | **11** |
| Elimu | 28 | 5 | **33** |
| Nishati na Madini | 14 | 1 | **15** |
| Afya | 150 | 51 | **201** |
| Mawasiliano na Uchukuzi | 15 | 2 | **17** |
| Maji | 11 | 2 | **13** |
| Jamii | 2 | 0 | **2** |
| Miradi Mingine | 20 | 3 | **23** |
| **Jumla** | **246** | **69** | **315** |

***Chanzo:*** *Taarifa za fedha za Mwaka wa Fedha 2023/24*



# SURA YA TATU

## Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita

# UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAGUZI ZILIZOPITA

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea maendeleo na hatua zilizochukuliwa na maofisa masuuli kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa taasisi husika. Ninatambua juhudi zinazochukuliwa na maofisa masuuli katika kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na kuandaa mipango ya ushughulikiaji wa changamoto zilizoripotiwa.

## 3.2 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita

Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ni muhimu kwa kuwa hukuza uwajibikaji, huchochea uboreshaji, hupunguza hatari, huongeza utendaji kazi kwa ujumla, huweka imani ya wadau, huhakikisha uzingatiaji wa sheria na maadili, huimarisha usimamizi wa rasilimali, na huimarisha utawala bora ndani ya taasisi.

Ufuatiliaji wangu wa utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita ulibaini kuwa katika taarifa 299 za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, kulikuwa na jumla ya mapendekezo 3,083 ya kaguzi zilizopita. Mapendekezo 1,394 (45%) yalitekelezwa kikamilifu; mapendekezo 789 (26%) yalikuwa katika hatua ya utekelezaji ; mapendekezo 477 (15%) yalikuwa hayajatekelezwa; mapendekezo 293 (10%) yalirudiwa; na mapendekezo 130 (4%) yalipitwa na wakati. Hali ya jumla ya utekelezaji wa mapendekezo inaridhisha kwa kiasi fulani. **Jedwali Na. 7 l**inaonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo.

**Jedwali Na. 7: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita**

| Sekta | Jumla ya Mapendekezo | Yaliyotekelezwa | Yanayoendelea Kutekelezwa | Hayakutekelezwa | Yaliyojirudia | Yaliyopitwa na Wakati |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo | 52 | 30 | 18 | - | 2 | 2 |
| Elimu | 487 | 269 | 139 | 14 | 41 | 24 |
| Nishati na Madini | 64 | 27 | 20 | 4 | 9 | 4 |
| Afya | 1858 | 844 | 359 | 409 | 168 | 78 |
| Mawasiliano na Uchukuzi | 182 | 75 | 50 | 19 | 29 | 9 |
| Maji | 230 | 43 | 144 | 21 | 22 | - |
| Jamii | 49 | 18 | 14 | 4 | 5 | 8 |
| Miradi Mingine | 161 | 88 | 45 | 6 | 17 | 5 |
| **Jumla** | **3,083** | **1,394** | **789** | **477** | **293** | **130** |

| Sekta | Jumla ya Mapendekezo | Yaliyotekelezwa | Yanayoendelea Kutekelezwa | Hayakutekelezwa | Yaliyojirudia | Yaliyopitwa na Wakati |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Asilimia (%)** | | **45** | **26** | **15** | **10** | **4** |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi za Mwaka 2023/24*

Kutotekelezwa kwa mapendekezo ya ukaguzi kunaweza kuwa na athari mbaya, zikiwemo kuhatarisha uadilifu kwenye eneo la usimamizi wa fedha; kuongezeka kwa vihatarishi katika utendaji; kudhoofisha ufanisi wa taasisi; kupoteza imani ya wadau wa miradi ya maendeleo; kusababisha migogoro ya kisheria na udhibiti; na kudumisha udhaifu wa mfumo unaoweza kusababisha upungufu wa ufanisi na hasara za kifedha.

**Ili kushughulikia mapendekezo yaliyosalia, ninapendekeza maofisa masuuli waweke vipaumbele kwenye rasilimali, kuimarisha juhudi za utekelezaji, na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani katika sekta zote.**




# SURA YA NNE

## Usimamizi wa Fedha, Matumizi, na Bajeti

# USIMAMIZI WA FEDHA, MATUMIZI, NA BAJETI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari wa kaguzi 332 za taarifa za fedha zinazohusu ufadhili wa miradi na matokeo muhimu ya ukaguzi wa usimamizi wa fedha na bajeti. Inatoa taarifa muhimu kwa serikali ili kuboresha usimamizi wa kifedha, kukuza uwajibikaji, na kuongeza uwazi katika taarifa za kifedha.

## 4.2 Ufadhili wa Miradi

Miradi ya maendeleo inafadhiliwa ya Serikali ya Tanzania na wadau wa maendeleo, ambao ni Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mfuko wa Maendeleo ya Afrika (ADF), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Uchumi Afrika (BADEA), Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani (CDC), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uingereza (DFID), Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo la Kanada (DFATD), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Jumuia ya Ulaya (EU), Shirika la Kimataifa la Upatikanaji wa Chanjo Duniani (GAVI), Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF), Mfuko wa Afya wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI (Global Fund), na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD). Wadau wengine ni Shirika la Maendeleo la Japani (JICA), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), Shirika la Ushirikianao wa Kimataifa la Elimu ya Juu la Uholanzi (NUFFIC), Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (OPEC), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Mfuko wa Suzan Thompson Buffet, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Mfuko wa Afrika wa Ustawi wa Pamoja (AGTF), na Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP), Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Serikali ya ufalme wa Norwei, Serikali ya Marekani na Benki ya Dunia.

Uchambuzi wa taarifa 332 za fedha za Mwaka wa Fedha 2023/24 ulionesha kuwa jumla ya fedha za miradi Shilingi trilioni 8.44 zilipokelewa. Kati ya hizo, Shilingi trilioni 5.97 zilitumika na kubakiza salio la Shilingi trilioni 2.50 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024. **Jedwali Na. 8** ni muhtasari wa maelezo ya uchambuzi huu wa kina kwa kila sekta.

**Jedwali Na. 8: Uchambuzi wa utendaji wa kifedha kisekta**

| Sekta | Fedha Zilizopo (Sh./Mil.) | Fedha Zilizotumika (Sh./Mil.) | Bakaa (Sh./Mil.) |
|---|---:|---:|---:|
| Kilimo | 254,886.54 | 150,644.13 | 104,242.41 |
| Mawasiliano na Uchukuzi | 882,875.11 | 661,816.30 | 221,058.81 |
| Elimu | 1,753,803.33 | 820,339.03 | 933,464.30 |
| Nishati na Madini | 243,918.99 | 179,247.18 | 64,671.81 |

| Sekta | Fedha Zilizopo (Sh./Mil.) | Fedha Zilizotumika (Sh./Mil.) | Bakaa (Sh./Mil.) |
|---|---|---|---|
| Afya | 758,724.62 | 430,928.29 | 327,796.33 |
| Miradi Mingine | 642,609.07 | 336,733.38 | 305,875.69 |
| Jamii | 700,816.49 | 627,842.91 | 72,973.59 |
| Maji | 3,204,688.42 | 2,729,803.67 | 474,884.75 |
| **Jumla** | **8,442,322.58** | **5,937,354.88** | **2,504,967.69** |

***Chanzo***: *Taarifa za ukaguzi 2023/24*

## 4.3 Usimamizi wa Matumizi

### 4.3.1 Fedha za Mradi Zilizokopwa Kutorejeshwa Shilingi Milioni 635.44

Jedwali la kwanza la Mkataba wa Ufadhili wa Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) wa tarehe 21 Mei mwaka 2020 na Sehemu Ndogo ya 4 ya Sehemu ya 2 ya Mkataba wa Ufadhili wa Mradi wa Ujenzi wa Ujuzi na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (EASTRIP) inataka fedha za miradi zitumike kufanikisha malengo ya miradi hiyo na kwamba watekelezaji wanapaswa kuzingatia mikataba ya ufadhili ili kuhakikisha kuwa fedha zinatumiwa tu kwa shughuli zilizokusudiwa za mradi.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia ilikopa Shilingi 635,447,342 kutoka katika miradi ya EASTRIP na SEQUIP.

Hatua hii ilikiuka sheria na masharti yaliyobainishwa katika mikataba ya fedha za miradi na miongozo ya utekelezaji wa miradi inayosimamia uendeshaji wa miradi hii. Maelezo kuhusu fedha zilizokopwa na kutorejeshwa yamebainishwa katika **Jedwali Na. 9**.

**Jedwali Na. 9: Fedha za miradi zilizokopwa na kutorejeshwa**

| Na. | JIna la Mradi | Maelezo ya Kukopa edha | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | EASTRIP | Kutekeleza shughuli za Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | 135,447,580 |
| 2 | SEQUIP | Kutekeleza shughuli za Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | 499,999,762 |
| **Jumla** | | | **635,447,342** |

***Chanzo:*** *Hati za malipo na viambatisho vyake vya Mwaka wa Fedha 2023/24*

Kushindwa kurejesha fedha kwenye miradi husika kunakwamisha ufikiaji wa malengo ya miradi hiyo, jambo linaloweza kusababisha ucheleweshaji katika utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa za miradi.

**Ninapendekeza menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia irejeshe haraka kwenye miradi husika fedha zilizokopwa ili kuepuka usumbufu katika utekelezaji wa shughuli zilizopangwa za miradi.**

### 4.3.2 Malipo ya Shilingi Milioni 892.92 Kufanywa Pasipo Vipimo vya Kazi Zilizofanyika au Kuidhinishwa na Mhandisi

Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi zinazofanya ununuzi ziidhinishe malipo kwa kuzingatia vipimo vilivyoidhinishwa katika vipindi maalumu vya mkataba. Aidha, Aya ya 25.3 ya Mwongozo wa Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi kwa Utaratibu wa Nguvukazi (force account) uliotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) wa Mei 2020 unaelekeza kuwa vipimo vya pamoja vya kazi zilizokamilika vifanywe na meneja wa mradi kwa kushirikiana na taasisi inayotekeleza mradi.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa miradi minne ililipa jumla ya Shilingi 892.92 milioni kwa mafundi na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule na vyuo vya walimu, ikiwa pamoja na madarasa, matundu ya vyoo, majengo ya utawala, mabweni, na majiko bila kutumia nyaraka za vipimo vinavyothibitisha kazi zilizotekelezwa.

Kasoro hii ilikotokana na upungufu wa watumishi katika idara ya ujenzi kulikosababisha kuidhinishwa kwa malipo bila kuhakikiwa kwa kina, kutathmini, na kupima kazi zilizofanyika. Maelezo ya kazi ambazo zilifanywa bila nyaraka za vipimo vya kazi na kuidhinishwa na mhandisi yameoneshwa kwenye **Jedwali Na. 10**.

**Jedwali Na. 10: Malipo ya kazi yaliyofanywa pasipo vipimo vya kazi**

| Na. | Jina la Mradi | Mtekelezaji | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | EPforR II | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | 132,135,785 |
| 2 | WSSP II | Wizara ya Maji | 320,565,827 |
| 3 | ESPJ Program | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | 161,820,003 |
| 4 | SEQUIP | OR-TAMISEMI | 278,406,980 |
| **Jumla** | | | **892,928,595** |

***Chanzo:*** *Kumbukumbu za malipo na vithibitisho kwa Mwaka wa Fedha 2023/24*

Idara ya ujenzi kuidhinisha malipo bila kukagua na kupima kazi iliyokamilishwa kunaongeza hatari ya malipo ya ziada, malipo ya kazi isiyokamilika, na uwezekano wa matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Ninapendekeza wasimamizi wa miradi wahakikishe kuwa kazi zinakaguliwa na kupimwa kabla ya kuidhinisha malipo ili kuepuka malipo ya ziada na malipo ya kazi zisizokamilika.**

### 4.3.3 Watu Walioathiriwa na Miradi Kutolipwa Fidia ya Shilingi Bilioni 24.75

Kifungu cha 3(1) (g) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 kinaelekeza watu, ambao haki zao za umiliki wa ardhi zimesitishwa au kumilikiwa na serikali kulipwa kwa fidia kamili, ya haki, na kwa wakati. Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Utwaaji Ardhi, Sura ya 118 pia kinataka malipo ya fidia, pamoja na riba ya asilimia sita kwa mwaka kuanzia tarehe ya kumiliki ardhi hadi tarehe ya malipo, endapo ardhi itachukuliwa kabla ya malipo ya fidia kufanyika.

Mapitio ya miradi 360 ilionyesha kwamba miradi saba ilikuwa na malimbikizo ya fidia zinazodaiwa jumla ya TZS bilioni 24.75, ikihusisha waathirika wa miradi (PAPs) 1,879. Changamoto ilibaki bila kutatuliwa huku baadhi ya miradi ikiwa imetekelezwa na mingine ikiwa katika hatuka za kukamilika, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la 11.

**Jedwali Na. 11: Watu waliothiriwa na miradi kutolipwa fidia**

| Na. | Jina la Mradi | Mtekelezaji | Idadi ya Waathiriwa wa Miradi | Kiasi (Sh.) | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa Maendeleo ya Bonde la Msimbazi (MBDP) | OR-TAMISEMI | 1,034 | 10,915,731,297 | Unaendelea |
| 2 | Mradi wa Kusafirisha Umeme Mkubwa na Uwekaji Umeme Vijijini - Geita- Nyakanazi kv 220 | Shirika la Umeme Tanzania | 392 | 1,352,808,948 | 99% |
| 3 | Mradi wa Kuunganisha Umeme Kenya na Tanzania (KTPIP) | Shirika la Umeme Tanzania | 80 | 12,210,077,532 | 98% |
| 4 | Mradi wa Kufua Umeme katika Mto Malagarasi | Shirika la Umeme Tanzania | 52 | 4,880,844 | Unaendelea |
| 5 | Mradi wa Usafirishaji wa Umeme Kigoma - Nyakanazi KV 400 | Shirika la Umeme Tanzania | 274 | 176,696,538 | 94.30% |
| 6 | Mradi Endelevu wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Arusha | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha | 15 | 45,231,723 | 100% |
| 7 | Mradi Wa Umeme Wa Maji Wa Mkoa Wa Maporomoko ya Rusumo | Shirika la Umeme Tanzania | 32 | 51,632,589 | 100% |
| **Jumla** | | | **1,879** | **24,757,059,472** | |

***Chanzo:*** *Taarifa za fidia*

Ucheleweshaji wa fidia ulisababishwa na migogoro juu ya viwango vya fidia, kutokuwapo kwa baadhi ya watu walioathiriwa na miradi, nyaraka zisizokamilika, na masuala ya uhamiaji yasiyotatuliwa.

Changamoto hizi zinaathiri uhusiano na jamii. Pia, zinaweza kuhatarisha maendeleo endelevu ya miradi kwa siku zijazo, pamoja na kuongeza gharama ya fidia kutokana na mabadiliko ya kiuchumi.

**Ninapendekeza watekelezaji wa miradi (a) waweke kipaumbele na kuharakisha mchakato wa malipo kwa watu walioathiriwa na miradi (b) washirikiane na mamlaka za serikali za mitaa na ofisi za usajili wa ardhi ili kuthibitisha umiliki wa ardhi na kutatua migogoro, ili kuhakikisha kuwa malipo yanafanywa kwa wakati.**

### 4.3.4 Malipo ya ziada kwa Wakandarasi Shilingi Milioni 586.43

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa tarehe 1 Agosti 2023, Wakala wa Barabara ilimlipa Kampuni ya M/S China Civil Engineering Construction Company (CCECC) jumla ya Shilingi 3,894,793,405.21 kwa Madai ya Malipo ya Mkandarasi Namba 1 (IPC Na. 1) chini ya Mradi wa Ushirikiano wa Usafiri Tanzania (TanTIP). Katika malipo haya, nilibaini malipo ya ziada ya jumla ya Shilingi 540,792,094 yaliyotokana na matumizi yasiyo sahihi ya fomula ya marekebisho ya bei.

Vilevile, katika Mradi wa Barabara ya Mkoa wa Iringa (Ipogolo - Kilolo), nilibaini jumla malipo ya ziada ya Shilingi 45,640,034 katika Madai ya Malipo ya Wakandarasi Namba 2 na 3, ambayo yamehusisha shilingi 9,462,996 za uchimbaji wa miamba iliyokuwa imelipwa katika malipo ya ankara za nyuma; Shilingi 18,743,120 za vipimo vya maabara zilizotakiwa kulipwa na mkandarasi; na Shilingi 17,433,918 zilizothibitishwa kimakosa kama kiasi cha malipo ya mkandarasi ya ada ya Bodi ya Kuepusha/Kusimamia Migogoro (DAAB).

**Ninapendekeza menejimenti ya Wakala wa Barabara Tanzania ipitie upya mchakato wa malipo na kuhakikisha kuwa hesabu za marekebisho ya bei zinazingatia kwa makini masharti ya mkataba, hususani matumizi sahihi ya fomula kama ilivyoainishwa katika kifungu kidogo cha 3.7.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba. Aidha, Wakala wa Barabara Tanzania uwatakaje wakandarasi kurejesha fedha walizolipwa zaidi na kutekeleza mfumo wa kuthibitisha hesabu kabla ya kuidhinisha malipo katika miradi inayoendelea.**

### 4.3.5 Malipo kwa Fedha Taslimu Shilingi Bilioni 2.01 Kutofanyika kwa Usahihi

Kanuni ya 93(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 (zilizorekebishwa mwaka 2004) inaelekeza malipo yafanyike moja kwa moja kwa wapokeaji waliotajwa kupitia uhamishaji wa benki au hundi.

Hata hivyo, tathmini yangu kwenye miradi minne iligundua kuwa jumla ya Shilingi 2,014,922,360 zililipwa kwa fedha taslimu ikiwa ni malipo ya posho, malipo ya kazi kwa mafundi wa ndani, na malipo kwa wazabuni na wakandarasi. Hali hii ilitokana na kutotumia njia mbadala za malipo, hivyo kusababisha kutegemea mtu mmoja kushughulikia na kusambaza kiasi kikubwa cha fedha. **Jedwali Na. 12** linaonesha miradi iliyofanya malipo kwa fedha taslimu kinyume na taratibu.

**Jedwali Na. 12: Miradi yenye Malipo kwa fedha taslimu kinyume na taratibu**

| Na. | Jina la Mradi | Mtekelezaji | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | SRWSSP | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini | 353,735,825 |
| 2 | RISE | Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini Tanzania | 1,088,213,933 |
| 3 | HEET | Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania | 164,800,000 |
| 4 | SEQUIP | OR-TAMISEMI | 408,172,602 |
| **Jumla** | | | **2,014,922,360** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Ukaguzi ya Mwaka wa Fedha 2023/24*

Vitendo hivi huongeza hatari ya usimamizi mbaya wa fedha, udanganyifu, na uwepo wa miamala isiyoidhinishwa. Malipo kwa fedha taslimu husababisha ugumu katika ufutiliaji na uthibitishaji wa matumizi, na hupunguza uwazi na uwajibikaji.

**Ninapendekeza menejimenti za taasisi husika zizingatie kanuni za kifedha kwa kuhakikisha malipo yote yanafanywa kupitia uhamishaji wa kibenki au hundi. Pia, ziangalie uwezekano wa kufanya malipo kwa njia mbadala kama malipo ya kielekitroni yatashindakana.**

### 4.3.6 Matumizi ya Shilingi Milioni 6.10 Yasiyo na Viambatisho vya Malipo

Kanuni ya 86 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 inasema kuwa "Utoaji wowote wa fedha za umma utafanyika vizuri kwa njia iliyoagizwa ya vocha ya malipo ambayo lazima iwe na/au imeambatishwa na maelezo kamili ya huduma ambayo malipo yanafanywa, kama vile tarehe, namba, umbali, na viwango ili kuwezesha kukaguliwa bila kumbukumbu ya hati zingine zozote. Pia, Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 inasema “Vocha

ya malipo ambayo haijakamilika kwa sababu ya kukosekana kwa nyaraka muhimu, itachukuliwa kama vocha iliyokosekana".

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa watekelezaji watatu wa miradi walilipa jumla ya Shilingi 6,102,348,668 kwa ajili ya kununua vitu mbalimbali bila kuwa na viambatisho muhimu kama risiti za kielekitroni na hati za madai kutokana na kutokuwa na udhibiti wa ndani wa ushahidi wa maandishi unaothibitisha malipo yaliyofanyika kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 13**.

**Jedwali Na. 13: Miradi yenye Matumizi yasiyo na viambatisho**

| Na. | Jina la Mradi | Mtekelezaji | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | SRWSSP | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini | 327,901,927 |
| 2 | TASAF III PSSN II | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii | 390,684,853 |
| 3 | SRWSSP | OR-TAMISEMI | 220,727,951 |
| 4 | TACTIC | OR-TAMISEMI | 137,500,000 |
| 5 | SEQUIP | OR-TAMISEMI | 5,025,533,938 |
| **Jumla** | | | **6,102,348,668** |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi zilizowasilishwa kwa watekelezaji 2023/24*

Hali hii inaleta shaka juu ya uhalali wa matumizi yaliyokosa viambatisho muhimu na uhalali wa shughuli inayodaiwa kuwa imefanyika. Pia, sikuweza kuthibitisha kwamba mlipaji alilipa kiasi kilichotajwa.

**Ninapendekeza taasisi husika iimarishe udhibiti wa ndani kwa kuhakikisha malipo yote yanaambatishwa na nyaraka muhimu kama vile risiti za kielekitroni, ankara, au mikataba.**

### 4.3.7 Fedha Zilizotumika Kinyume na Maelekezo ya Miradi Shilingi Milioni 545.57

Aya ya 8.1 ya Mwongozo wa Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi kwa Utaratibu wa Nguvukazi (force account) inasema kwamba mtekelezaji wa mradi anatakiwa kuimarisha utekelezaji wa mradi kwa wakati katika suala la ununuzi wa zana na vifaa vinavyotumika katika miradi.

Nilibaini halmashauri 14 zilitumia fedha kiasi cha Shilingi 545,576,889 za Mfuko wa EPforR II kwa shughuli ambazo hazikuhusiana na mradi kutokana na mipango isiyo sahihi na ukosefu wa uzingatiaji wa miongozo. Hatua hii ilisababisha matumizi mabaya ya rasilimali kwa shughuli zisizohusiana moja kwa moja na miradi iliyoidhinishwa. Orodha ya halmashauri husika inaoneshwa katika **Kiambatisho Na. II.**

Ugawaji mbaya wa fedha za mradi huathiri utekelezaji na ukamilishaji kwa wakati wa shughuli zilizopangwa, hivyo kuchelewesha ufikiaji wa malengo ya mradi. Pia, husababisha ufanisi mbovu katika matumizi ya rasilimali, hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi na usimamizi mbaya wa kifedha.

**Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia izingatie kikamilifu miongozo ya mradi na kanuni za kifedha. Pia, iimarishe upangaji na usimamizi wa mtiririko wa fedha ili kusaidia kupunguza upungufu wa bajeti na kupunguza hatari ya upotevu wa fedha.**

### 4.3.8 Kuchelewa Kuwasilishwa Kodi ya Zuio Shilingi Bilioni 46.66 na Kutokatwa Kodi ya Zuio Shilingi Bilioni 6.76

Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 322, 2019 (iliyorekebishwa) inataka mawakala wa kuzuia kodi kutuma kodi iliyozuiliwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ndani ya siku saba baada ya kila mwisho wa mwezi wa kalenda. Zaidi ya hayo, mashirika ya wakazi wanaofanya malipo kwa bidhaa zinazotolewa na biashara za wakazi lazima yawasilishe kodi ya zuio kama ilivyoelezwa katika sheria.

Hata hivyo, katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa kodi ya zuio ya kiasi cha Shilingi bilioni 46.66 iliyokatwa kutoka kwa wakandarasi na washauri wa Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) ilichelewa kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa siku 57 hadi 241 kutokana na udhaifu wa ufuatiliaji. **Jedwali Na. 14** linaonesha idadi ya siku ambazo kodi ya zuio ilichelewa kuwasilishwa.

**Jedwali Na. 14: Kuchelewa kuwasilisha kodi ya zuio**

| Mwezi | Tarehe ya kutolewa | Tarehe iliyowasilishwa | Idadi ya siku zilizocheleweshwa | Jumla ya kiasi cha kodi ya zuio (Sh.) | Kiasi cha kodi ya zuio kisichowasilishwa kwa wakati (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 23/7 | 7/8/2023 | 4/4/2024 | 241 | 1,863,748,690 | 1,747,067,989 |
| 23/10 | 7/8/2023 | 4/4/2024 | 149 | 15,454,262,315 | 15,451,700,092 |
| 23/11 | 7/8/2023 | 4/4/2024 | 119 | 18,211,983,476 | 18,185,647,832 |
| 23/12 | 7/8/2024 | 4/4/2024 | 88 | 6,762,829,515 | 6,732,087,679 |
| 24/1 | 7/8/2024 | 4/4/2024 | 57 | 4,586,441,894 | 4,546,272,908 |
| Jumla | | | | | **46,662,776,500** |

***Chanzo:*** *Marejesho ya kodi ya zuio*

Aidha, nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania ilishindwa kukata kiasi cha Shilingi 6,756,805,077 na kupeleka Mamlaka ya Mapato Tanzania kutokana na kufanya malipo moja kwa moja, hivyo kushindwa kukata kodi ya zuio kutoka kwenye chanzo. Hali hii iliwaruhusu wakandarasi kupokea kiasi kamili cha ankara moja kwa moja kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Pia, Wakala

wa Barabara Tanzania iliwaachia wakandarasi jukumu la kupeleka kodi ya zuio kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania, kinyume na utaratibu. Pia, Wakala wa Barabara Tanzania haikukata kodi ya zuio kutoka kwenye malipo ya awali (advance payment) kiasi cha Shilingi 1,295,668,611. Kushindwa kuwasilisha kodi ya zuio kunaweza kusababisha shirika kupewa adhabu kwa kutozingatia sheria za kodi.

**Ninapendekeza wasimamizi wa Mradi wa Reli ya Kisasa na Wakala wa Barabara Tanzania wahakikishe wanapeleka kwa wakati kodi ya zuio na kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa malipo ya kodi kwa ufanisi. Aidha, kuhakikisha kuwa Mkandarasi anawasilisha makato ya kodi ya zuio kutoka Hati za Madai (IPC) zilizopita kabla ya kuendelea na hati za madai zinazofuata.**

## 4.4 Usimamizi wa Bajeti

### 4.4.1 Kutofanyika kwa Shughuli Zenye Thamani ya Shilingi Bilioni 428.46 Zilizowekwa kwenye Bajeti

Kanuni ya 40(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 inaelekeza kuwa makadirio ya matumizi yatakayoandaliwa chini ya Kifungu cha 18 cha Sheria yanaonesha kiwango kinachotarajiwa kutumika na Serikali katika mwaka husika, na hakitajumuisha matumizi yasiyohesabika kama vile matumizi yasiyotabiriwa.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kutotekelezwa ipasavyo kwa shughuli zilizokuwa kwenye bajeti zenye thamani ya jumla ya shilingi 428,468,122,533 kwa watekelezaji wa miradi 23. Hali hii ilitokana na kuchelewa kwa taratibu za ununuzi, utiaji saini wa mikataba, na utoaji wa fedha kutoka mamlaka husika na wafadhili. Ucheleweshaji huo ulizuia utekelezaji wa miradi, na uliathiri utoaji wa huduma na ufanisi wa miradi kwa ujumla. Orodha ya miradi ambayo shughuli zake hazikufanyika inaoneshwa katika **Kiambatisho Na. III**.

**Ninapendekeza watekelezaji wa miradi husika waboreshe mipango ya ununuzi na idhini za mkataba, na waongeze ufanisi katika utoaji wa fedha ili kuzuia kuchelewa kutekeleza miradi.**

### 4.4.2 Kutopata kwa Uhakika Fedha Shilingi Bilioni 141.75 za Bajeti Kutokana na Kutofaulu Ulipaji Unaohusisha Matokeo (DLRs)

Ufadhili wa programu za maendeleo unategemea utendaji kazi, na malipo yanayotolewa baada ya kufaulu wa matokeo yaliyoainishwa katika mikataba ya ufadhili wa fedha na miongozo ya uendeshaji. Kuzingatia viashiria vya utendaji vilivyokubaliwa kunahitajika, na malipo yote yanategemea uthibitisho wa

kujitegemea ili kuhakikisha uwajibikaji na uwazi. Mbinu hii inahakikisha kwamba msaada wa kifedha unawiana na malengo ya programu na hutolewa tu wakati matokeo yanayoweza kupimika yanapofikiwa. Ingawa mahitaji mahususi yanaweza kutofautiana katika mipango tofauti, ni lazima sekta zote zifikie malengo ya utendaji wao ili zistahili kupokea fedha.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa jumla ya Shilingi 141,757,169,215 hazikulipwa kwa watekelezaji wa miradi sita kutokana na kutofikiwa ipasavyo kwa ulipaji unaohusisha matokeo (DLRs). Hali hii ilisababishwa na kuchelewa kutekelezwa kwa miradi na kutokuwapo kwa nyongeza ya muda wa kutekeleza miradi kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 15**.

**Jedwali Na. 15: Miradi iliyokosa fedha kwa kutofaulu ulipaji unaohusisha matokeo**

| Na. | Jina la Mradi | Mtekelezaji | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | TSMP Awamu ya Pili | Shirika la Viwango Tanzania | 17,508,561,416 |
| 2 | EASTRIP | DIT - Kampasi ya Mwanza | 233,321,345 |
| 3 | SEQUIP | OR-TAMISEMI | 73,958,386,376 |
| 4 | EPforR awamu ya pili | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | 3,812,810,478 |
| 5 | SWASH | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | 39,021,721,600 |
| 6 | SWASH | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | 7,222,368,000 |
| | | **Jumla** | **141,757,169,215** |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi za Mwaka wa Fedha 2023/24*

Kushindwa kufaulu ulipaji unaohusisha matokeo na kupata malipo pungufu kunaweza kuharibu uaminifu miongoni mwa wadau wakuu, kama vile wafadhili, mashirika ya serikali, na umma. Zaidi ya hayo, kutopata na kutoa fedha kama ilivyopangwa kunaweza kuzuia kufikiwa kwa malengo mapana ya programu na kuhatarisha malengo ya kimkakati ya muda mrefu.

**Ninapendekeza watekelezaji wa miradi wahakikishe wanazingatia kufikia na kufaulu ulipaji unaohusisha matokeo ulioainishwa ili kuhakikisha kuwa fedha zinatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu.**

### 4.4.3 Kuchelewa kwa Utoaji wa Bajeti ya Shilingi Bilioni 427.36

Utoaji wa fedha za miradi unatarajiwa kuendana na mzunguko wa bajeti na ratiba ya utekelezaji wa shughuli za miradi kama inavyoidhinishwa katika mpangokazi wa mwaka kwa kila mradi.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa watekelezaji 17 wa miradi walichelewa kupata fedha za kutekeleza miradi kiasi cha Shilingi 427,368,144,904. Ucheleweshaji huo ulitokana na michakato ya ndani ya muda mrefu na masuala ya mfumo wa malipo wa "D-Fund". Miradi 16 ilichelewa kupata fedha kwa kipindi cha hadi

mwaka mmoja na Mradi wa SEQUIP ulichelewa kwa muda wa miaka hadi minne. **Kiambatisho Na. IV** kinaonesha mchanganuo wa miradi iliyochelewa kupata fedha za bajeti.

Kuchelewa kutolewa kwa fedha kunaathiri utekelezaji kwa wakati wa shughuli za miradi.

**Ninapendekeza watekelezaji wa miradi wapunguze visababishi vya kuchelewa kupata fedha za miradi. Hatua hii itasaidia fedha za bajeti kupokelewa ndani ya muda uliokusudiwa ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa miradi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.**



# SURA YA TANO

## Usimamizi wa Ununuzi

## USIMAMIZI WA UNUNUZI

### 5.1 Utangulizi

Usimamizi wa ununuzi katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini unazingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, Kanuni zake za Mwaka 2013 (zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2016), na miongozo ya ziada ya ununuzi, ambayo huandaliwa kwa pamoja na Serikali ikishirikiana na washirika wa maendeleo. Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa ununuzi katika miradi ya maendeleo.

### 5.2 Kutotekelezwa kwa Ununuzi Uliyopangwa Wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 133.24

Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kukadiria kwa usahihi mahitaji yao ya bidhaa, huduma, na kazi kadiri inavyowezekana, hususani kwa huduma na shughuli zilizopangwa katika mpangokazi wa mwaka na kujumuishwa kwenye makadirio ya mwaka.

Nilipitia shughuli za ununuzi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2024 na kubaini kutotekelezwa kwa mipango ya ununuzi ya mwaka iliyoidhinishwa yenye thamani ya Shilingi 133,245,739,645 kwa miradi sita kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 16**.

Kutotekelezwa kwa shughuli hizi za ununuzi kulisababishwa na ukadiriaji usio sahihi na kutokutekelezwa kwa ufanisi mipango ya ununuzi. Kushindwa kuteleleza ununuzi uliopangwa kunadhihirisha upungufu wa ufanisi katika kuzingatia mipango ya ununuzi na kucheleweshwa kwa miradi muhimu ya miundombinu inayolenga kuboresha huduma za maji, uhakika wa chakula, na usafi wa mazingira vijijini.

**Jedwali Na. 16:Miradi yenye ununuzi uliopangwa ambao haujatekelezwa**

| Na. | Mradi | Jina la Mtekelezaji | Kiasi (Dola za Marekani) | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | EHPMP | NEMC | 1,888,953 | 4,962,148,171 |
| 2 | SRWSSP | RUWASA | | 55,445,157,516 |
| 3 | TFSRP | NIRC | | 29,600,900,000 |
| 4 | TFSRP | Wizara ya Kilimo | | 41,406,397,858 |
| 5 | CRTAES-FNS | Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela<br>Kituo cha Utafiti katika Maendeleo ya Kilimo | 330,000 | 866,886,900 |
| 6 | TSSP | TANROADS | | 964,249,200 |
| **Jumla** | | | | **133,245,739,645** |

***Chanzo:*** *Majalada ya Mikataba*

**Ninapendekeza menejimenti za Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ziboreshe usahihi wa upangaji, kuharakisha michakato ya ununuzi, na kuimarisha ufuatiliaji ili kuhakikisha kukamilika kwa wakati kwa miradi na utekelezaji wa mipango ya ununuzi iliyoidhinishwa ili kuwezesha umma kunufaika ndani ya muda uliopangwa.**

## 5.3 Kufanya Majadiliano bila Kibali cha Bodi za Zabuni kwa Mikataba ya Shilingi Billion 1.97

Kanuni ya 227 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaelekeza kuwa bodi ya zabuni ziidhinishe mipango ya majadiliano kabla ya kuanza kwa mazungumzo yoyote. Hata hivyo, mapitio ya majalada ya zabuni za Mpango Endelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini unaotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini yalibaini kuwa Ofisi za Mikoa ya Lindi na Morogoro zilifanya majadiliano na wakandarasi kwa mikataba yenye thamani ya Shilingi 1,977,775,551 bila kupata kibali cha mipango ya majadiliano kutoka bodi zake za zabuni.

Hali hii ilitokana na upungufu katika mifumo ya uthibiti wa ndani katika usimamizi wa michakato ya ununuzi. Ukosefu wa usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa menejimenti ulisababisha ofisi hizi kutofuata taratibu za lazima za kupata idhini kutoka kwa bodi za zabuni.

Bila mifumo ya kufuatilia na kutatua changamoto, mikataba iliyoidhinishwa yenye jumla ya Shilingi 1,977,775,551 inaweza kuwa katika hatari ya kuwa na matumizi mabaya ya fedha. Ukosefu wa taratibu madhubuti za idhini unaongeza uwezekano wa hasara za kifedha au kutokuwapo kwa ufanisi katika utekelezaji wa mikataba hiyo.

**Ninapendekeza menejimenti ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini iboreshe mifumo ya udhibiti wa ndani katika michakato ya ununuzi ili kuhakikisha kuwa shughuli zote za ununuzi zinafuata kikamilifu sheria za ununuzi.**

## 5.4 Upungufu katika Usanifu wa Miradi Uliosababisha Gharama ya Ziada za Shilingi Bilioni 1.94

Aya ya 4.1 ya Mwongozo wa Usanifu, Usimamizi wa Ujenzi, Uendeshaji na Matengenezo (DCOM), Toleo la Nne, Juzuu ya Kwanza, wa Mwaka 2020 wa Wizara ya Maji inasisitiza umuhimu wa kufanya tathmini sahihi ya mahitaji ya maji kwa wakati uliopo na kwa baadaye katika kupanga na kusanifu miradi ya usambazaji wa maji.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa miradi mitatu ya maji yenye thamani ya Shilingi 6,739,625,559.39 iliyotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini chini ya Mpango Endelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (SRWSSP) katika mikoa ya Rukwa na Kagera ilitumia Shilingi 1,057,354,508, ambazo ni zaidi ya fedha zilizokubaliwa katika mikataba. Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Kagera ilitumia gharama za ziada za Shilingi 884,920,550 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 17.**

**Jedwali Na. 17: Gharama za ziada kwa miradi**

| Mradi | Mtekelezaji | Region | Jumla ya Mkataba (Sh.) | Gharama ya Ziada (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| SRWSSP | RUWASA Rukwa | Rukwa | 6,739,625,559.39 | 1,057,354,508 |
| | RUWASA Kagera | Kagera | 4,225,721,712.10 | 884,920,550 |
| **Jumla** | | | **6,739,625,559.39** | **1,942,275,058** |

***Chanzo:*** *Majalada ya mikataba*

Gharama hizi za ziada zilitokana na usanifu duni wa mradi, ambao ulisababisha kutokuwapo kwa vipengele muhimu katika makisio ya gharama za ujenzi (BOQ), kama vile matanki ya kuhifadhi maji na miundombinu ya vyanzo vya maji, pamoja na kiasi kidogo cha uchimbaji. Hali hii inakiuka Aya ya 4.1 ya Mwongozo wa Usanifu, Usimamizi wa Ujenzi, Uendeshaji na Matengenezo (DCOM), Toleo la Nne, Juzuu ya 1 wa Mwaka 2020 wa Wizara ya Maji.

**Ninapendekeza menejimenti ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ihakikishe utekelezaji wa tathmini ya kina wa maeneo na usanifu sahihi wa miradi kwa mujibu wa Kifungu cha 2.3.1 cha Mwongozo wa Usanifu, Ujenzi, na Uendeshaji wa Miundombinu ya Maji wa Wizara ya Maji ili kuzuia gharama za ziada na kuepuka kutoweka vipengele muhimu vya miradi.**

## 5.5 Mabadiliko ya Kiasi cha Mahitaji na Ongezeko la Gharama Shilingi Bilioni 14.97 bila Kupata Idhini ya Bodi za Zabuni

Kanuni ya 110(7) ya Kanuni za Ununuzi za Umma za Mwaka 2013 (kama zilivyofanyiwa marekebisho na Kanuni za Ununuzi za Umma za Mwaka 2016) inaelekeza kwamba mabadiliko yoyote yanayobadilisha mawanda, kiwango, au nia ya mkataba baada ya utekelezaji wake lazima yapate idhini ya maandishi kutoka kwa bodi ya zabuni kabla ya kutekelezwa.

Tarehe 13 Septemba 2021, Wakala wa Barabara Tanzania alisaini Mkataba Na. TRD/HQ/1013/2021/2022 na Kampuni ya M/S Sinohydro Corporation Ltd JV kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Awamu ya 1, Kipande cha 1, Fungu Na. 1 (Miundombinu) kwa thamani ya Shilingi 165,627,031,495.52 kwa miezi 36 unaishia tarehe 20 Aprili 2025. Baadaye,

tarehe 14 Mei 2022, Wakala wa Barabara Tanzania ilisaini Mkataba Na. TRD/HQ/1064/2021/2022 na Kampuni ya M/S Beijing Construction Group JV kwa ajili ya Fungu Na. 2 (Majengo) kwa thamani ya Shilingi 194,403,506,327.45 ambapo muda wa awali wa kukamilika ulipangwa kuwa tarehe 29 Novemba 2025, kisha kubadilika hadi tarehe 31 Machi 2025.

Hata hivyo, mapitio ya hati za madai ya wakandarasi Na. 15 kwa Fungu la 1 Na. 7 kwa Fungu la 2 yalibaini kazi za ziada kutokana na mabadiliko ya kiasi cha mahitaji ya mradi yenye jumla ya Shilingi 14,066,207,038.45 (Shilingi 12,658,079,407.86 kwa Fungu la 1 na Shilingi 1,408,127,630.59 kwa Fungu la 2) bila kupata idhini ya Bodi ya Zabuni.

Vivyo hivyo, tarehe 20 Agosti 2021, TANROADS alisaini Mkataba Na. TRD/HQ/1008/2021/2022 na Kampuni ya China Railway 15 Bureau Group kwa ajili ya kuboresha Barabara ya Mkange-Tungamaa-Pangani (km 120.8), likiwemo Daraja la Pangani (525), kwa kiwango cha lami. Mapitio ya hati ya malipo Na. 9 kwa mkandarasi kwa Kipande cha 3 yalibaini kazi ya ziada kutokana na mabadiliko ya kiasi cha mahitaji kwa shilingi 906,699,474, ambayo pia hayakupata idhini ya Bodi ya Zabuni, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 18.**

**Jedwali Na. 18: Kazi za ziada ambazo hazikuidhinishwa na bodi za zabuni**

| Jina la mtekelezaji | Maelezo ya Mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| TANROADS | TRD/HQ/1013/2021/2022 | 14,066,207,038 |
| TANROADS | TRD/HQ/1008/2021/2022 | 906,699,474 |
| **Jumla** | | **14,972,906,512** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi uliofanywa na mkaguzi kwenye hati ya madai Na. 15 Fungu la 1 na Na. 7 Fungu la 2 na Na. 9 Fungu la 3*

Mabadiliko haya ya kiasi cha mahitaji, ambayo yalisababisha ongezeko la gharama yalitekelezwa bila idhini ya awali kutoka bodi za zabuni kama inavyotakiwa na Kanuni ya 110(7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013.

**Ninapendekeza menejimenti ya Wakala wa Barabara Tanzania iimarishe udhibiti wa usimamizi wa mikataba ili kuhakikisha kuwa mabadiliko ya kiasi cha mahitaji yanapata idhini kutoka Bodi ya Zabuni kabla ya utekelezaji.**

## 5.6 Mkataba wa Thamani ya Dola za Marekani Milioni 30.75 (Shilingi Bilioni 80.78) Kutolewa kwa Mkandarasi kabla ya Kufanya Uchunguzi wa Kina

Kwa mujibu wa Kanuni ya 373(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013, taasisi nunuzi zinapaswa kufanya uchunguzi wa kina kwa mtoahuduma aliyependekezwa kabla ya kumpa mkataba. Uchunguzi huu unahusisha kuthibitisha uzoefu wa mtoahuduma, sifa, historia ya mashauri ya kisheria, uwezo wa kifedha, na utendaji wake wa miradi ya awali.

Mapitio yangu ya Mkataba Na. TZ-DAWASA-6497-CW-RFB kati ya Wizara ya Maji – Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) chini ya Mradi wa Kusaidia Sekta ya Maji Awamu ya II (WSSP II) na Kampuni ya M/S METITO kwa ajili ya usanifu, ujenzi, na uendeshaji wa Mtambo wa Kusafisha Majitaka kilichopo Mbezi Beach wenye thamani ya dola za Marekani 30,752,186.91 (bila kujumuisha kodi ya ongezeko la thamani na gharama za umeme), yalibaini kuwa licha ya mkataba huo kufanyiwa tathmini ya kiufundi na kifedha, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam haikufanya uchunguzi wa kina na wa kutosha hasa ikizingatiwa thamani kubwa ya mkataba huo. Matokeo yake, utekelezaji wa mradi uko mbioni kusitishwa bila maelezo, huku mkandarasi akishindwa kuwasilisha dhamana ya malipo ya awali inayohitajika na kutofanya maendeleo yoyote muhimu katika kazi husika.

Hali hii ilitokana na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam kutofanya uchunguzi wa kina kabla ya kumpa mkandarasi mkataba.

**Ninapendekeza menejimenti ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam ihakikishe inafanya kwa makini uchunguzi wa kina kwa mikataba yote yenye thamani kubwa, ikiwa pamoja na kuthibitisha uwezo wa mkandarasi na historia ya utendaji, ili kupunguza athari na kuhakikisha utekelezaji unaoridhisha wa miradi.**

## 5.7 Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi Vyenye Thamani ya Shilingi Bilioni 3.1 kutoka kwa Wazabuni Wasioidhinishwa

Ukaguzi wa taratibu za ununuzi wa vifaa vya ujenzi vilivyotumiwa katika Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa chini ya Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kwa ajili ya ujenzi wa shule mbalimbali katika mkoa wa Mara, ulibaini kuwa ununuzi wa vifaa vyenye thamani ya shilingi 3,100,824,370 ulifanyika kinyume na masharti ya ununuzi ya Vifungu vya 31.4, 31.5 32(2) na 32.3 vya Mwongozo wa Mamlaka ya Uthibiti wa Ununuzi wa Umma wa Utekelezaji wa Kazi za Ujenzi kwa Kutumia Nguvukazi ya Taasisi Nunuzi wa Mei 2020.

Vifaa hivyo vilinunuliwa kutoka kwa wazabuni ambao hawakuwa wameidhinishwa, au katika maduka yasiyokuwa na idhini ndani ya jamii husika, au bila kuwa na makubaliano yoyote ya kimkataba kutoka kwa Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA).

Udhaifu huu ulitokana na kushindwa kuhusisha wazabuni waliothibitishwa na kufuata taratibu sahihi za ununuzi kwa kuwashindanisha wazabuni. Matokeo yake, ununuzi ulifanyika kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa, jambo linalodhoofisha kanuni za uwazi, uwajibikaji, na matumizi sahihi ya fedha za umma. Kuvunjwa kwa taratibu za ununuzi kunaonesha wasiwasi kuhusu uadilifu wa mchakato wa ununuzi. **Jedwali Na. 19** linaonesha halmashauri zilizofanya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa.

**Jedwali Na. 19: Halmashauri Zilizofanya Ununuzi wa Bidhaa za Ujenzi kutoka kwa Wazabuni Wasioidhinishwa**

| Mtekelezaji (Halmashauri) | Kiasi (Sh.) |
|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti | 274,306,074 |
| Halmashauri ya Mji Mdogo wa Tarime | 883,591,555 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Rorya | 430,993,665 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Butiama | 464,917,208 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Musoma | 438,024,996 |
| Halmashauri ya Mji wa Musoma | 608,990,881 |
| **Jumla** | **3,100,824,379** |

***Chanzo:*** *Majalada ya mikataba*

**Ninapendekeza mamlaka husika za serikali za mitaa zihakikishe ununuzi wote unafanywa kutoka kwa wazabuni walioidhinishwa kama inavyotakiwa na kanuni zilizotajwa hapo juu.**

## 5.8 Ununuzi Uliofanywa Nje ya Mfumo wa Kielekitroni wa Ununuzi wa Umma (NeST) Wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 4.49

Kanuni ya 342(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi zote zinazohusika na ununuzi kutumia kikamilifu au kwa sehemu Mfumo wa Kielekitroni wa Ununuzi wa Umma, sambamba na kutumia taratibu zilizopo zisizo za kimfumo. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa Waraka Na. 2 tarehe 23 Julai 2023 unaozitaka taasisi nunuzi kuanza kutumia Mfumo wa Kielekitroni wa Ununuzi wa Umma kuanzia tarehe 1 Oktoba 2023, kuchukua nafasi ya matumizi ya Mfumo wa Kielekitroni wa Ununuzi wa Umma (TANePS).

Ukaguzi wangu wa taarifa za ununuzi na majalada ya zabuni kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ulibaini kuwa watekelezaji sita wa miradi walifanya ununuzi mbalimbali wa jumla ya shilingi 4,497,053,164 nje ya Mfumo wa Kielekitroni wa

Ununuzi wa Umma, kinyume na Kanuni ya 342(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013. **Jedwali Na. 20** linaonesha ununuzi uliofanywa nje ya Mfumo wa Kielekitroni wa Ununuzi wa Umma.

**Jedwali Na. 20: Miradi yenye Ununuzi nje ya Mfumo wa Kielekitroni wa Ununuzi wa Umma**

| Mradi | Mtekelezaji | Kiasi (Dola za Kimaremaki) | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| SEQUIP | OR-TAMISEMI | | 2,620,711,633 |
| ESPJ | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | | 1,311,013,027 |
| TSMP II | Ofisi ya Taifa ya Takwimu | | 190,600,000 |
| Ruzuku ya Mfuko wa Kimataifa wa VVU (TZA-H-MOFP) | Wizara ya Afya | 86,903.89 | 213,062,150 |
| Mfuko wa Afya wa Pamoja | Halmashauri ya Jiji la Mwanza | | 137,512,785 |
| Mfuko wa Afya wa Pamoja | Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa | | 24,153,569 |
| **Jumla** | | | **4,497,053,164** |

***Chanzo:*** *Taarifa za ununuzi na majalada ya zabuni kwa Mwaka wa Fedha 2023/24*

**Ninapendekeza watekelezaji wa miradi wahakikishe wanazingatia kikamilifu Kanuni ya 342(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kwa kufanya shughuli zote za ununuzi kupitia Mfumo wa Kielekitroni wa Ununuzi wa Umma (NeST). Ununuzi wowote utakaofanyika nje ya mfumo huu lazima uwe na sababu za msingi za kimaandishi na uidhinishwe.**




# SURA YA SITA

## Usimamizi wa Mikataba na Hali Halisi ya Utekelezaji wa Miradi

# USIMAMIZI WA MIKATABA NA HALI HALISI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua mambo muhimu kuhusu matokeo ya ukaguzi wa usimamizi wa mikataba na utendaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2024. Hususani, sura inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa utekelezaji wa mikataba na hali halisi ya mikataba katika taasisi za umma.

## 6.2 Usimamizi wa Mikataba

### 6.2.1 Mikataba Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 13.45 Kusainiwa Bila Kuhakikiwa

Kanuni za 59(1)(2) na 60(1)(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013, kama zilivyorekebishwa na Kanuni ya 2 na ya 3 za Kanuni za Marekebisho ya Ununuzi wa Umma za Mwaka 2016 (Tangazo la Serikali Na.121 la Mwaka 2016) zinataka mikataba yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni moja ihakikiwe na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ile yenye thamani ya chini ya shilingi bilioni moja ihakikiwe na maafisa wa sheria kabla ya kusainiwa kwake.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mikataba yenye thamani ya Shilingi 13,452,879,289.88 ilisainiwa bila kufanyiwa uhakiki na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au maafisa sheria. Mikataba 251 yenye thamani ya Shilingi 3,550,230,773.44 ilihusiana na miradi sita, wakati Mkataba Na. 88Z5/2023/2024/W/0 wenye thamani ya Shilingi 9,902,648,516.44 (ikiwa pamoja na kodi ya ongezeko la thamani) ulikuwa wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa SEQUIP. **Jedwali Na. 21** linaonesha mikataba ambayo haikuhakikiwa.

**Jedwali Na. 21: Mikataba Iliyosainiwa bila Kuhakikiwa**

| Na. | Jina la Mradi | Mtekelezaji | Idadi ya Mikataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ESPJ | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | 44 | 1,872,560,257 |
| 2 | SEQUIP | OR - TAMISEMI | 77 | 674,792,920 |
| 3 | EPforR Awamu ya pili | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | 79 | 494,622,845 |
| 4 | BOOST | OR - TAMISEMI | 39 | 297,060,000 |
| 5 | SRWSSP | OR - TAMISEMI | 11 | 159,133,751 |
| 6 | BOOST | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | 1 | 52,061,000 |
| | | **Jumla** | **251** | **3,550,230,773** |

***Chanzo***: *Taarifa za Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/24*

Kasoro hii ilisababishwa na uhitaji wa kutekeleza mradi ndani ya muda mfupi, hali iliyolazimisha kukiuka hatua ya kupeleka mikataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na maafisa sheria kwa ajili ya uhakiki. Sababu nyingine ni ukosefu wa maafisa sheria katika ngazi za vyuo vya maendeleo ya wananchi, kwa mikataba inayohusiana na Mradi wa Uwezeshaji Kupitia Ujuzi. Kasoro hii inaongeza hatari ya kutokea migogoro ya kisheria inayoweza kusababisha hasara za kifedha na kuathiri sifa ya taasisi husika.

**Ninapendekeza menejimenti za OR-TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia zihakikishe kuwa watekelezaji wa miradi kama vile halmshauri za wilaya na vyuo vya maendeleo ya wananchi wanahakikisha kuwa mikataba yao inahakikiwa na maafisa wa sheria kabla ya kusainiwa. Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ihakikishe mikataba yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni moja inapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki kabla ya kusainiwa.**

### 6.2.2 Malipo ya Riba ya Shilingi Bilioni 1.29 Kutokana na Kuchelewesha Malipo ya Wakandarasi

Vifungu vidogo vya 14.7(c) na 14.8 vya Masharti ya Jumla ya Mkataba vinataka, endapo mkandarasi hatolipwa ndani ya siku 56 kuanzia tarehe ambayo mhandisi (meneja wa mradi) atapokea taarifa na nyaraka za uthibitisho wa malipo, mkandarasi ana haki ya kulipwa riba kwa kiasi ambacho hakijalipwa. Riba hii itaongezeka kila mwezi katika kipindi chote cha ucheleweshaji. Aidha, Kifungu cha 50 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba wa SRWSSP kinamtaka mkandarasi kuwasilisha taarifa za kila mwezi za maendeleo ya kazi kwa meneja wa mradi, ambaye atahakiki na kuthibitisha malipo ndani ya siku 28. Mwajiri anapaswa kulipa kiasi kilichohakikiwa ndani ya siku 28. Ucheleweshaji wa malipo husababisha riba inayohesabiwa kuanzia tarehe ya malipo yalipopaswa kufanyika hadi tarehe ya malipo halisi.

Uhakiki wangu ulibaini kuwa miradi mitano katika sekta za uchukuzi na maji ililipa riba ya kiasi cha Shilingi 1,294,779,077.60 kutokana na kuchelewa kulipa madai ya wakandarasi, kinyume na masharti ya mkataba. Ucheleweshaji huu ungeweza kuepukwa kama malipo yangefanyika kwa wakati. **Jedwali Na. 22** linaonesha miradi na riba iliyolipwa kutokana na kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi.

**Jedwali Na. 22: Miradi na riba iliyolipwa kutokana na kuchelewesha malipo ya wakandarasi**

| Na. | Jina la Mradi | Mtekelezaji | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa Kuboresha Barabara ya Kimataifa: Rumonge - Gitaza (km 45) na Kabingo - Kasulu - Manyovu (km 260) | TANROADS | 510,782,987 |
| 2 | Mradi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Pili | TANROADS | 360,780,035 |
| 3 | Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira - Ziwa Viktoria (LV WATSAN) | MWAUWASA | 207,198,193 |
| 4 | Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato - Awamu ya Kwanza | TANROADS | 110,662,937.60 |
| 5 | Mradi wa Kuboresha Barabara ya Kimataifa: Bagamoyo - Horohoro/Lungalunga - Malindi - Awamu ya kwanza | TANROADS | 105,354,925 |
| | **Jumla** | | **1,294,779,077.60** |

***Chanzo:*** *Taarifa za kifedha za miradi na hati za malipo ya wakandarasi*

Hali hii ilisababishwa na kukosekana kwa uratibu miongoni mwa wadau wa maendeleo; kutokuwapo kwa ufanisi katika mifumo ya malipo ya ndani na ya nje kama vile mfumo wa "D-Fund"; uhaba wa fedha kutoka Hazina; taratibu za muda mrefu za mapitio na uidhinishaji; kuchelewa kutolewa kwa fedha kwa pande zote mbili; na changamoto za mifumo zinazohusiana na taratibu za mwongozo za msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Dosari hizi zinazuia utekelezaji wa mikataba kwa kiwango kinachostahili, hivyo kusababisha ucheleweshaji mkubwa wa utekelezaji wa miradi; ongezeko la gharama za miradi; na kuhitaji nyongeza ya fedha, ambazo zingeweza kuelekezwa kwenye shughuli zingine za kipaumbele.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia watekelezaji wa miradi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi, irahisishe na kupitia michakato ya malipo, kuhakikisha mtiririko wa fedha unatosheleza, na uidhinishaji wa hati za malipo za wakandarasi na hati za madai (ankara) ufanyike kwa wakati ili kuepuka adhabu na riba. Aidha, ipitishe mifumo bora kwa kuhakikisha uidhinishaji kupitia mfumo wa "D-Fund" inakamilika haraka, na malipo kwa wakandarasi na washauri elekezi yafanyike kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya mkataba ili kuepuka ucheleweshaji usio wa lazima katika kufikia malengo ya mradi na kupunguza gharama za riba zinazotokana na kucheleweshwa kwa malipo.**

### 6.2.3 Malipo ya Awali Shilingi Bilioni 13.79 Yasiyokuwa na Dhamana

Kifungu cha 14.2.4 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinataka mwajiri kufanya malipo ya awali kwa mkandarasi endapo mkandarasi atawasilisha dhamana ya benki isiyo na masharti kutoka benki inayokubalika na mwajiri. Malipo ya awali yanapaswa kutolewa na taasisi nunuzi tu baada ya kupokea dhamana ya malipo ya awali kutoka benki yenye sifa zinazokidhi vigezo vilivyowekwa.

Wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini malipo ya awali yenye jumla ya Shilingi 13,792,176,593.92 yalifanyika bila kupata Dhamana za Malipo ya Awali zinazohitajika, hali inayosababisha hatari kubwa ya kifedha. Hususan, malipo ya awali ya Shilingi 4,028,532,995.75 yalitolewa kwa mikataba 15 yenye thamani ya Shilingi 32,422,363,559.26, iliyotekelezwa na ofisi tano za kanda za Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RUWASA) chini ya Mpango Endelevu wa Usambazaji wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (SRWSSP), bila kupata dhamana zinazohitajika. Vilevile, chini ya Awamu ya tatu ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP III), malipo ya awali ya Shilingi 9,612,834,696 yalifanywa kwa mradi wenye thamani ya mkataba wenye thamani ya Shilingi 48,064,173,480.50, bila kupata dhamana inayohitajika.

Zaidi ya hayo, baada ya kukagua Mkataba Na. ME-011/2021-2022/W/Contract/02 kwa ajili ya Mradi wa Pili wa Msaada kwa Sekta ya Maji (WSSP II) kwa ujenzi wa Jengo la Kituo cha Ubora wa Rasilimali za Maji (WRCOE) katika Manispaa ya Dodoma, lenye thamani ya Shilingi 1,885,111,277.12 (bila VAT), nilibaini kuwa kufikia tarehe 17 Oktoba 2023, mkandarasi alikuwa tayari ametoza 88% ya thamani ya mkataba, ilhali malipo ya awali ya Shilingi 150,808,902 yalikuwa bado hayajapata dhamana. Aidha, muda wa kurejesha malipo haya ulikuwa umepita, kwani mkataba ulikoma tarehe 30 Oktoba 2023, hivyo kuongeza hatari ya kutorejeshwa kwa fedha hizo. Ninahusisha dosari hizi na usimamizi dhaifu wa mikataba na uangalizi hafifu. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye **Jedwali Na. 23**.

**Jedwali Na. 23: Malipo ya awali yasiyokuwa na dhamana**

| Jina la mradi | Mtekelezaji | Idadi ya Mikataba | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Kiasi cha Dhamana (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| SRWSSP | RUWASA | 15 | 32,422,363,559.26 | 4,028,532,995.75 |
| WSSP Awamu ya Pili | Wizara ya Maji | 1 | 1,885,111,277.12 | 150,808,902.17 |
| WSDP Awamu ya Tatu | Wizara ya Maji | 1 | 48,064,173,480.50 | 9,612,834,696 |
| **Jumla** | | **17** | **82,371,648,316.88** | **13,792,176,593.92** |

***Chanzo:*** *Majalada ya miradi*

**Ninapendekeza kwamba Serikali iimarishe udhibiti wa usimamizi wa mikataba na ihakikishe malipo ya awali kwa wakandarasi hayafanyiki bila kuwepo dhamana ya malipo hayo.**

### 6.2.4 Madai ya Muda Mrefu ya Wakandarasi Shilingi Bilioni 13.70

Kifungu cha 14.7.1 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba ya Kawaida kati ya Wakala wa Barabara Tanzania na wakandarasi kinawataka Wakala wa Barabara Tanzania kuwalipa wakandarasi ndani ya siku 56 tangu wahandisi wakazi wanapopokea maombi ya malipo kutoka kwa wakandarasi.

Ukaguzi wangu ulibaini madai ya muda mrefu ya wakandarasi yenye thamani ya Shilingi 13,701,000,959.19 kwenye miradi mitatu ya kuboresha barabara chini ya Miradi ya Kuboresha Barabara ya Kimataifa ya Rumonge - Gitaza (km 45) na Kabingo – Kasulu - Manyovu (km 260) unaosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania. Kati ya kiasi hiki, Shilingi 7,133,386,508.51 zilikuwa mchango wa Serikali ya Tanzania, huku Shilingi 6,567,614,450.68 zilikuwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Ucheleweshaji wa malipo ulianzia siku 57 hadi 781, zaidi ya muda wa siku 56 unaohitajika kwa mujibu wa masharti ya mkataba. **Jedwali Na. 24** linaonesha wakandarasi na kiasi cha fedha za madai ya muda mrefu.

**Jedwali Na. 24: Madai ya muda mrefu ya wakandarasi**

| Kipande Na. | Nambari ya Hati ya Malipo | Mkandarasi | Chanzo cha Fedha | Kiasi (Sh.) | Idadi ya siku ya kuchelewa mwezi Oktoba 2024 (Wigo) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 6 | Zhejiang | Serikali ya Tanzania | 1,139,708,834.44 | 130-341 |
| 2 | 17 | Sino Hydro | Serikali ya Tanzania | 2,680,548,305.63 | 98-617 |
| 3 | 28 | Stecol | Serikali ya Tanzania | 3,313,129,368.44 | 57-781 |
| | | | Benki ya Maendeleo ya Afrika | 6,567,614,450.68 | 57-547 |
| **Jumla** | | | | **13,701,000,959.19** | |

***Chanzo:*** *Taarifa za maendeleo za kila mwezi na hati za madai ya wakandarasi kwa Vipande vya 1, 2 na 3*

Hali hii ilisababishwa na upungufu wa fedha zilizotolewa na Wizara ya Fedha ikiwa ni mchango kutoka Serikali ya Tanzania na ucheleweshaji wa kupata idhini (no objection) kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kazi za nyongeza zilizozidi kiasi cha mkataba kilichoidhinishwa. Ucheleweshaji huu wa muda mrefu una madhara kama vile malimbikizo ya riba, kuongezeka kwa gharama za miradi, na usumbufu wa mtiririko wa fedha kwa wakandarasi. Changamoto hizi

zinaathiri utekelezaji wa miradi, hivyo kusababisha ucheleweshaji zaidi wa utekelezaji na kuhatarisha kutokamilika kwa miundombinu muhimu kwa wakati.

**Ninapendekeza TANROADS ashirikiane na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha kuhakikisha madai ya wakandarasi yanalipwa kwa wakati kuepuka tozo za riba. Aidha, ihakikishe maombi ya kupata idhini (no objection) yanawasilishwa kwa wakati ili kuepuka ucheleweshaji katika utekelezaji wa miradi.**

### 6.2.5 Utekelezaji wa Kazi Bila Uwasilishaji wa Dhamana za Utendaji Shilingi Bilioni 47.90

Kanuni ya 29(5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inatamka kwamba iwapo mkataba utafanyiwa marekebisho baada ya kusainiwa hivyo kusababisha ongezeko la gharama zaidi ya asilimia 10, taasisi inayohusika itawataka wakandarasi kuwasilisha dhamana ya ziada ya utendaji ya asilimia 10 ili kufidia ongezeko hilo. Aidha, Sehemu ya 11.2 ya Mwongozo wa Dhamana katika Ununuzi wa Umma wa Mwezi Februari Mwaka 2022 unataka mzabuni awasilishe dhamana ya utendaji kabla ya kusaini mkataba.

Mapitio yangu ya nyaraka za mikataba kwa miradi iliyotekelezwa yalibaini dosari zinazohusiana na uwasilishaji wa dhamana za utendaji wa wakandarasi na wasambazaji wa huduma na bidhaa kama inavyofafanuliwa hapa chini.

**(a) Kutowasilishwa dhamana ya utendaji Shilingi bilioni 9.90**

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilisaini mkataba Na. 88Z5/2023/2024/W/07 na Kampuni ya Ramada Construction Engineers kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya mkoa (Shule ya Sekondari Kidete) kwa bei ya mkataba ya shilingi 9,902,648,516.44. Hata hivyo, mapitio yangu yalionesha kuwa dhamana ya utendaji kwa kazi hiyo haikuwasilishwa na mkandarasi, kinyume na Kanuni 29(5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 na Kifungu cha 62.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba.

**(b) Kuongeza muda wa mikataba bila kuongeza dhamana za utendaji Shilingi bilioni 5.70**

Wizara ya Afya ilisaini mkataba na Kampuni ya T-MARC Tanzania tarehe 25 Novemba 2022 kwa ajili ya kununua, kuhifadhi, kuweka chapa, kutangaza, na kusambaza kondomu za kiume kwa thamani ya shilingi 5,707,492,397.34 kwa mwaka mmoja chini ya Mfuko wa Kimataifa wa Kudhibiti UKIMWI (TZA-H-MOFP), unaotekelezwa na Wizara ya Fedha. Dhamana ya utendaji ya benki iliyowasilishwa tarehe 2 Novemba 2022 ilikuwa halali hadi 31 Disemba 2023.

Hata hivyo, Wizara iliongeza mkataba kutoka tarehe 23 Januari 2024 hadi 22 Julai 2024 bila kuongeza dhamana ya utendaji ili kufidia muda wa mkataba ulioongezwa.

**(c) Kutohuishwa kwa dhamana za utendaji kazi Shilingi bilioni 4.21 ili kuendana na bei ya marekebisho ya mkataba**

Wasambazaji wa bidhaa kwa kipande cha I hadi cha IV chini ya Mradi wa Tanzania wa Kidijiti (DTP) unaotekelezwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano, na Teknolojia za Habari, waliwasilisha dhamana za awali za utendaji kazi za asilimia 10 ya thamani ya mkataba ya Shilingi 35,757,491,467 isiyojumuisha kodi ya ongezeko la thamani. Mnamo mwezi Julai 2024, thamani ya mkataba ilirekebishwa kuwa Shilingi 42,193,839,931.14 ikiwa na kodi ya ongezeko la thamani 18%. Marekebisho hayo ya mkataba yanahitaji kuhuishwa dhamana ya utendaji kwa Shilingi 4,219,383,993.12 sawa na 10% ya thamani ya mkataba.

Dosari hizi zilitokana na ufuatiliaji hafifu wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kuhakikisha dhamana za utendaji zinawasilishwa. Aidha, kushindwa kuwasilisha dhamana za utendaji kunaiweka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwenye hatari ya kupata hasara za kifedha, kudhoofisha uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi, na kuhatarisha ukamilishaji wa miradi kwa wakati.

**Ninapendekeza menejimenti za watekelezaji wa miradi ziimarishe udhibiti ili kuzuia dosari kama hizi siku zijazo; na zihakikishe wakandarasi na wasambazaji wa huduma na bidhaa wanawasilisha na kuhuisha dhamana za utendaji kulingana na masharti ya mkataba ili kukidhi kikamilifu muda wa mkataba, hivyo kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa miradi na kutoa fidia endapo kutakuwa na utendaji duni au usiokidhi viwango vilivyowekwa.**

## 6.3 Hali Halisi ya Utekelezaji wa Miradi

### 6.3.1 Ujenzi wa Shule Mpya 35 za Msingi na 148 za Sekondari Katika Maeneo Yasiyopimwa Shilingi Bilioni 125.14

OR-TAMISEMI imekuwa ikitekeleza mradi wa BOOST ili kuimarisha upatikanaji sawa wa elimu bora katika shule za awali na msingi kote Tanzania Bara. OR-TAMISEMI inatekeleza pia Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) wenye lengo la kuongeza upatikanaji wa elimu ya sekondari, kuweka mazingira wezeshi ya kujifunzia kwa wasichana, na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya sekondari kwa wasichana na wavulana. Miradi hii imekuwa ikifadhili ujenzi wa shule mpya za sekondari na msingi sehemu mbalimbali nchini.

Ili kuhakikisha uendelevu wa miradi hii, Katibu Mkuu wa OR-TAMISEMI kupitia barua yenye Kumb. Na. DB.291/297/04/51 ya tarehe 22 Machi 2023, aliagiza mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha shule hizo zinajengwa katika maeneo yaliyopimwa na hati miliki za viwanja husika zinapatikana ndani ya miezi mitatu tangu tarehe ya agizo.

Mapitio ya nyaraka na ziara za ukaguzi wa miradi zilibaini kuwa shule mpya 35 za msingi zenye thamani ya Shilingi 15,819,500,000 na shule mpya 148 za sekondari zenye thamani ya Shilingi 109,327,133,843 zilijengwa katika maeneo ambayo hayakupimwa, kinyume na maelekezo.

Ufuatiliaji hafifu wa maafisa masuuli katika kupata maeneo kwa ajili ya ujenzi wa shule ulisababisha hali hii, hivyo kuziweka shule hizo katika hatari ya migogoro ya ardhi kama vile migogoro ya umiliki na mipaka.

**Ninapendekeza menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa ziharakishe ufuatiliaji ili maeneo yaliyojengwa shule hizo yapimwe na hati miliki zipatikane bila kuchelewa zaidi.**

### 6.3.2 Kutotumika kwa Miundombinu ya Miradi Iliyokamilika Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 10.15

OR - TAMISEMI ilitoa agizo lenye Kumb. Na. DA.291/297/06 la tarehe 9 Agosti 2023 linalowataka watekelezaji wa miradi kuhakikisha kuwa ujenzi na ukarabati wa miundombinu unakamilika ndani ya miezi mitatu baada ya kupokea fedha.

Aidha, Kifungu cha 3.3.8 cha Kitabu cha Miundombinu Iliyolengwa Kutelekezwa cha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF III-PSSN II) kinataka miradi iliyokamilika kukaguliwa, kuthibitishwa kwa kuzingatia ubora na vigezo vingine vilivyoainishwa awali, na kuzinduliwa rasmi kupitia sherehe ya ufunguzi, kisha kutolewa hati ya kumaliza kazi za utekelezaji wa miradi kwa jamii.

Mapitio yangu ya nyaraka za miradi na ziara za ukaguzi zilizofanyika mwezi Agosti 2024 kwa lengo la kutathmini hali ya utekelezaji wa miradi yalibaini kuwa miundombinu ya shule yenye thamani ya Shilingi 10,159,860,156, ikijumuisha ujenzi wa vyoo, madarasa, maabara, maktaba, na vyumba vya TEHAMA katika miradi mitatu ya sekta za elimu na maji, ilikamilika lakini haikuwa kitumika. Vilevile, miradi midogo ya Miundombinu Iliyolengwa Kutelekezwa (Targeted Infrastructure) katika maeneo 15 ya utekelezaji wa miradi chini ya TASAF III-PSSN II yenye thamani ya Shilingi 2,853,955,649.90, ilikamilika lakini haikuwa imeanza kutumika. Aidha, katika sekta ya kilimo, Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu (TANIPAC) uliohusisha ujenzi wa kituo cha karantini, maabara ya uthibiti wa ubora, na maghala yenye thamani ya Shilingi 5,742,587,254 ulikuwa

umekamilika lakini haukuanza kutumika. **Jedwali Na. 25** linaonesha miundombinu ya miradi iliyokamilika lakini haikuwa inatumika.

**Jedwali Na. 25: Miundombinu ya miradi iliyokamilika lakini haikuwa inatumika**

| Jina la Mradi | Mtekelezaji | Aina ya Miundombinu Iliyokamilika | Muda Ujenzi Ulipokamilika | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| EPforR Awamu ya Pili | Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia | Madarasa na vyoo vilivyokamilika kujengwa | Ndani ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 | 500,000,000 |
| TASAF III-PSSN II | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii | Miradi Midogo ya Miundombinu Iliyolengwa Kujengwa ambayo imekamilika | Ndani ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 | 2,853,955,649 |
| SEQUIP | OR-TAMISEMI | Vyumba vya madarasa, maabara, maktaba, vyumba vya TEHAMA na vyoo vilivyokamilika | Miradi miwili tarehe 15/08/2023 na miradi saba tarehe 30/06/2024 | 1,063,317,252 |
| TANIPAC | Wizara ya Kilimo | Kituo cha karantini, maabara ya uthibiti ubora, na maghala | Mradi mmoja tarehe 31/07/2023 na miradi miwili tarehe 22/08/2022 | 5,742,587,254 |
| **Jumla** | | | | **10,159,860,156** |

***Chanzo***: *Ziara za ukaguzi wa miradi mwezi Agosti 2024*

Tatizo hili lilitokana na kutokuwapo kwa samani, vifaa vya maabara, vifaa vya TEHAMA, ukosefu wa huduma ya maji kwa matumizi ya vyoo vya shimo, na kuchelewa kutoa vyeti vya kumaliza kazi kwa shule husika. Katika miradi ya TASAF III-PSSN II, watekelezaji wa miradi katika maeneo husika hawakuwa na maandalizi ya kutosha ya kuandaa sherehe za uzinduzi na ukamilishaji wa vyeti vya kumaliza kazi ili kuruhusu utumiaji wa miundombinu iliyokamilika. Aidha, kulikuwa na usimamizi duni wa mkataba katika Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu.

**Ninapendekeza menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia ishirikiane na OR-TAMISEMI ili kuharakisha ununuzi wa samani, vifaa, na upatikanaji wa huduma ya maji ili miundombinu ya shule iliyokamilika ianze kutumika bila kuchelewa zaidi; Menejimenti za usimamizi katika maeneo ya watekelezaji wa miradi husika ziharakishe maandalizi ya sherehe za ufunguzi na kukabidhi vyeti vya kumaliza kazi ili miradi itumike bila kuchelewa zaidi; Menejimenti ya Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu (TANIPAC)**

**uimarishe usimamizi wa mikataba ili kutatua changamoto zilizobaki na kuruhusu mradi kuanza kutumika bila kuchelewa zaidi.**

### 6.3.3 Michoro ya majengo ya shule za sekondari 83 kutoidhinishwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Kanuni ya 248 ya Kanuni za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (Tahadhari za Moto katika Majengo) za Mwaka 2015 inasisitiza kuwa, wakati wa kuandaa pendekezo la ujenzi wa jengo jipya, kufanya upanuzi, au kubadilisha muundo wa jengo lililokusudiwa kujengwa, ni muhimu kuhakikisha mipango hiyo inakidhi kanuni za ujenzi zilizowekwa na mamlaka za serikali za mitaa. Aidha, mamlaka ya serikali za mitaa zinapaswa kushauriana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kabla ya kuidhinisha mipango husika.

Hata hivyo, nilibaini kuwa michoro ya usanifu wa muundo wa majengo ya shule 83 za sekondari katika halmashauri 78 zilizokuwa chini ya Mradi wa EPforR Awamu ya Pili, haikuidhinishwa wala kupitiwa upya na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Halmashauri hizo zilipokea jumla ya Shilingi 9,773,868,500 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na madarasa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024.

Kasoro hii ilitokana na usimamizi duni ambapo michoro ya miundo ya majengo haikuthibitishwa kwa umakini wa kutosha. Kutozingatia kanuni za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuna hatari kubwa kwamba miundombinu ya majengo ya shule za sekondari 83 isiwe na kiwango sahihi kwa ajili ya matumizi yenye kujitosheleza kwa wanafunzi.

**Ninapendekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa zishirikiane na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili kuhakikisha michoro ya majengo ya shule 83 za sekondari inakaguliwa kwa kuzingatia taratibu, na kama kutakuwa na marekebisho yoyote yahayohitajika yashughulikiwe ipasavyo; na (b) mamlaka za serikali za mitaa zihakikishe kuwa michoro ya majengo yote inawasilishwa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa ukaguzi na uidhinishaji kabla ya kuanza kwa ujenzi.**

### 6.3.4 Ujenzi wa Miradi 13 Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 47.42 Kufanyika Bila Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii

Kifungu cha 81 (3) (4) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kinaelekeza kazi ya ujenzi isifanyike bila kupata cheti cha tathmini ya athari za mazingira kinachotolewa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, na kwamba mtu yeyote atakayekiuka kifungu kidogo cha (3) anahesabiwa kuwa ametenda kosa.

Mapitio yangu yalibaini kuwa ujenzi wa miradi 13 yenye thamani ya Shilingi 47,427,056,110 ulitekelezwa bila kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamii. Mradi mmoja wenye thamani ya Shilingi 24,921,111,947 unahusiana na RWSSP iliyotekelezwa na RUWASA, wakati miradi mingine 12 yenye jumla ya Shilingi 22,505,944,163 inahusiana na mradi wa SEQUIP uliotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. V**.

Fedha zilizotolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari zimetengwa kwa ajili ya ujenzi bila kipengele cha tathmini ya athari za mazingira na jamii. Aidha, fedha hizi zilitolewa kwa maagizo ya utekelezaji wa muda mfupi, kwa kawaida miezi mitatu baada ya kupokea fedha. Hivyo, kulikuwa na usimamizi duni katika utekelezaji wa tathmini ya athari za mazingira na jamii katika Programu Endelevu ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Kushindwa kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamii kabla ya kuanza kwa mradi kunaweza kuuweka mradi huo kwenye hatari ya uharibifu wa mazingira, kutozingatia sheria, na hatari za kiafya na usalama, si tu kwa mradi bali pia kwa jamii. Bila kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamii, athari mbaya kama vile mmomonyoko wa ardhi, uchafuzi wa maji, au uharibifu wa viumbe hai (bioanuwai), haziwezi kutambuliwa au kushughulikiwa ipasavyo.

**Ninapendekeza menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ihakikishe kuwa fedha zinazotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi zinajumuisha kipengele cha kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamii. Watekelezaji wa miradi wanapaswa kuhakikisha kuwa tathmini ya athari za mazingira na jamii inafanywa kabla ya kuanza ujenzi.**



# SURA YA SABA

## Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Mradi wa Bwawa la Umeme wa Maji la Julius Nyerere

# UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA MRADI WA BWAWA LA UMEME WA MAJI LA JULIUS NYERERE

## 7.1 Utangulizi

Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP) unalenga kuzalisha umeme kwa gharama nafuu, kudhibiti mafuriko, na kusaidia umwagiliaji, usambazaji wa maji, utunzaji wa mazingira, na uhifadhi wa wanyamapori. Mradi una uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 na gigawati 6,307 kwa mwaka. Mradi unatekelezwa na Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO) na kusimamiwa na mshauri elekezi chini ya Wakala wa Barabara Tanzania. Mradi huu unajengwa na ubia wa wakandarasi (Kampuni ya Arab Contractors kwa ushirikiana na Kampuni ya Elsewedy Electric JV). Gharama ya mradi ni shilingi trilioni 6.56 na unafadhiliwa kikamilifu na Serikali ya Tanzania.

Mradi ulipangwa kukamilika tarehe 14 Juni 2022, lakini baada ya kuchelewa, sasa umekadiriwa kukamilika kufikia tarehe 31 Mei 2025. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi huu mwezi Disemba 2024, maendeleo ya jumla ya utekelezaji wa mradi yalikuwa 99.35%, aidha, imekubaliwa kuwa tarehe ya kukamilisha mradi itategemea mazingira ya mwenendo wa kazi zinazoendelea.

Ukaguzi ulitathmini iwapo TANESCO inasimamia mradi huu kwa kuzingatia muda, gharama, na ubora ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya mradi. Ukaguzi wangu wa mradi huu ulihusu utekelezaji wa mradi kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwezi Disemba 2022 hadi Disemba 2024.

## 7.2 Upangaji, Usanifu na Ununuzi kwenye Mradi

### 7.2.1 Mpango Hafifu wa Utayari na Dharura Katika Kukabiliana na Mafuriko

Kanuni ya 6(1) (j) ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Tathmini na Ukaguzi wa Athari kwa Mazingira) za Mwaka 2018 inataka kufanyika maandalizi ya mpango wa utayari, dharura, na kukabiliana na mafuriko ili kuhakikisha afya na usalama wa wafanyakazi na jamii inayouzunguka mradi katika muda wote wa maisha ya mradi.

Nilibaini kuwa mpango wa utayari, dharura na kukabiliana na maafa ulioandaliwa na TANESCO ulikuwa hauijitoshelezi ili kukabiliana na athari za mafuriko kwa ujumla wake wakati wa uzalishaji wa umeme katika Mradi wa Bwawa la Umeme wa Maji la Julius Nyerere. Mpango huo haukujumuisha mpango-mkakati wa mawasiliano ya dharura na wadau muhimu kama vile Ofisi ya Waziri Mkuu - Idara ya Usimamizi wa Maafa, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Bodi ya Bonde la Mto Rufiji, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, na Mamlaka ya

Hifadhi za Taifa Tanzania. Pia, mpango huo haukujitosheleza kwenye kuchukua hatua za kuongeza elimu na uelewa kwa jamii zinazoishi ukanda wa chini ya bwawa katika maeneo hatarishi na yanayokumbwa na mafuriko kila mwaka.

Kasoro hizi zilitokana na TANESCO kutokuwa na maandalizi ya kutosha wakati wa makabidhiano ya shughuli za ujenzi wa bwawa, na kutozingatia, kwa kiasi kikubwa, athari zinazoweza kutokea kutokana na kushindwa kuhimili kwa bwawa na kufurika kwa maji wakati malango ya kuzuia na punguza maji yanapofunguliwa kutokana na kuongezeka kwa kasi kwa maji yanayoingia katika bwawa.

Upungufu huo unaweza kuongeza athari iwapo bwawa litashindwa kuhimili uzito wa ujazo wa maji, hivyo kusababisha upotevu wa maisha, uharibifu mkubwa wa maliasili na miundombinu, uharibifu wa mazingira, na hasara kubwa za kiuchumi.

**Ninapendekeza TANESCO iandae Mpango Mkamili wa Kujiandaa na Kukabiliana na Dharura wenye mkakati wa kimawasiliano kwa wadau muhimu na program za kuchochea ufahamu na kuzuia athari za mafuriko kwa jamii zilizohatarini kukumbwa na mafuriko.**

## 7.3 Usimamizi wa Mikataba

### 7.3.1 Kuajiri Kampuni ya Kigeni ya Sheria Bila Kupata Idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kifungu cha 20(1) cha Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu), Sura ya 268, marekebisho toleo la mwaka 2019, kinataka ushiriki wa washauri na wizara, serikali au wakala wowote kwa ajili ya kutoa huduma za kisheria ufanywe baada ya kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusiana na masuala yanayohitaji ushauri.

Nilibaini kuwa TANESCO iliajiri kampuni ya kigeni ya sheria inayowakilisha serikali katika Bodi ya Usuluhishi wa Migogoro ya kimkataba (DAB) bila kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliidhinisha kupitia majibu ya barua yenye Kumb. Na. CBC.69/381/04/2023 ya tarehe 18 Aprili 2023.

Aidha, mapitio yangu ya nyaraka yamebaini kampuni hiyo ya kisheria ilishaanza kazi kabla ya kupata kibali cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo kampuni hiyo ilipewa kazi tangu 15 Machi 2023.

Kuajiri kampuni ya kigeni kabla ya idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, TANESCO inavunja matakwa ya kisheria hali inayoweza kupelekea kuteua kampuni ya kisheria isiyo na ufanisi. Kampuni hiyo inakosa uzoefu wa kutatua migogoro katika ujenzi wa miradi mikubwa kama vile miradi ya mabwawa ya umeme wa maji ambayo inatumia viwango vya kimataifa vya mikataba vya FIDIC, inayojumuisha matakwa ya jumla ya kimkataba (Mkataba wa Ujenzi na Usanifu toleo la kwanza la mwaka 1999 - kitabu cha njano, Mkataba wa kukabidhi funguo/EPC toleo la kwanza la 1999 – kitabu cha fedha, na Mkataba wa ujenzi, toleo la kwanza la 1999 – Kitabu chekundu)

Kutokana na dosari hizi, uwakilishi wa kisheria kwa TANESCO haukuwa wa ufanisi wa kulinda maslahi ya TANESCO. Hii imethibitishwa na uamuzi wa rufaa ambao Bodi ya Usuluhishi wa Migogoro ya Kimkataba (DAB) uliotolewa Oktoba 2024, ulimpa mkandarasi ushindi katika madai mawili na baadaye kufidiwa. Katika madai mengine mawili, mkandarasi alishinda, lakini makadirio yaliachwa mikononi mwa mwakilishi wa mwajiri (mshauri elekezi) kwa uamuzi. Dai moja, mkandarasi alipewa ushindi lakini makadirio yalifutwa na dai lingine lilifutwa lakini madai ya fidia yalikataliwa.

**Ninapendekeza TANESCO iombe mwongozo na kibali kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale inaposhirikiana na vyombo vya sheria vya nje wakati wa utekelezaji wa shughuli zake.**

### 7.3.2 Mshauri wa Huduma za Kisheria Kulipwa Shilingi Milioni 752.87 Bila Kuwa na Mkataba

Kanuni ya 317(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaitaka taasisi ya ununuzi na kampuni kukubaliana kuhusu viwango vya malipo anavyolipwa mtaalamu, na malipo kufanywa kulingana na muda uliotumika.

Mapitio yangu yalibaini kuwa TANESCO ililipa jumla ya Shilingi 752,873,457.90 kwa ajili ya huduma za kisheria zilizofanywa kati ya tarehe 30 Juni 2023 na 31 Mei 2024 bila mkataba na Kampuni ya Huduma za Kisheria (M/S Fasken). Kati ya kipindi hicho TANESCO ilikuwa tayari limemlipa mshauri kwa kutumia barua kama kiambatisho yenye (Kumb. Na. DMDPRI/PC/JNHPP/06/20223 ya tarehe 12 Juni 2023). Baadaye TANESCO na mshauri walisaini mkataba ambao haukuwa na namba ya kumbukumbu ya utoaji wa huduma.

**Ninapendekeza TANESCO ihakikishe kuwa makubaliano yote kwa siku zijazo yanaidhinishwa rasmi kwa kuwa na mikataba sahihi, ikiwa pamoja na namba za kumbukumbu na masharti yaliyo wazi, kabla ya kufanya malipo. Pia, TANESCO iimarishe udhibiti wa ndani ili kuhakikisha uzingatiaji wa kanuni za ununuzi na za kifedha ili kuepuka matatizo kama hayo siku zijazo.**

### 7.3.3 Kutokata Kodi ya Zuio Shilingi Milioni 130.91 Kutoka Kwa Malipo Ya Mwanasheria

Kifungu cha 83(A) na aya ya 4(c) ya Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, Sura ya 332 na Marakebisho yake Toleo la Mwaka 2019 linataka kukatwa kwa kodi ya zuio kwa malipo yanayofanywa kuhusiana na utoaji wa huduma kwa kiwango cha asilimia 15 kwa wasio wakazi na asilimia 5 kwa wakazi, na asilimia 2 kwa wasambazaji wa bidhaa kwa kampuni za ndani ya nchi.

Nilibaini kuwa, TANESCO haikuzuia na kupeleka kodi ya zuio la 15% ya Shilingi 130,915,556 kwenye malipo aliyolipwa Kampuni ya Sheria na Mtaalamu wa Umeme wa Maji.

Udhaifu huu ulisababishwa na udhibiti duni wa mchakato wa malipo ya ndani na usimamizi wa kodi wa TANESCO hali inayosababisha upotevu wa mapato ya serikali.

**Ninapendekeza TANESCO lihakikishe kodi ya zuio ya kiasi cha Shilingi 130,915,556 inakatwa kutoka kwa mshauri wa sheria na mtaalamu wa umeme wa maji na kuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania bila kuchelewa zaidi.**

### 7.3.4 Kutolipa Fidia kwa Kuchelewa Kukamilisha Mradi Shilingi Milioni 327.93

Kifungu cha 8.7 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba ya Miradi ya Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi kinaelekeza kwamba kama mkandarasi atashindwa kukamilisha kazi ndani ya muda uliotakiwa, mkandarasi atalipa fidia ya ucheleweshaji wa kazi kwa mwajiri kwa kosa hilo. Pia, kifungu cha 8.7 cha masharti mahususi ya mkataba kinaainisha kiasi cha fidia ya ucheleweshaji kuwa asilimia 0.1 ya bei ya mkataba kwa kila siku iliyochelewa, na kiwango cha juu cha ucheleweshaji kuwa asilimia 5 ya bei ya mkataba.

Mapitio yangu ya mkataba wa uhandisi, ununuzi, na ujenzi yalionesha kuwa mkataba ulisainiwa tarehe 12 Disemba 2018 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 14 Juni 2022. Hata hivyo, nilibaini kwamba TANESCO kupitia Mshauri Elekezi (TECU) haikukata fedha ya ucheleweshaji wa kukamilika kwa mradi kiasi cha Shilingi 327,931,025,254 kama fidia kutoka kwenye malipo ya mkandarasi, ilhali mpaka wakati wa ukaguzi wangu tarehe 31 December 2024 mradi ulikuwa umechelewa kukamilika kwa siku 352 kulingana na tarehe iliyobadilishwa ya kukamilisha mradi 14 Januari 2024.

TANESCO na TECU walionesha kuwa fidia ya ucheleweshaji ilitakiwa kuwa Shilingi 273,788,089,010 kwa kuzingatia mikataba ya makabidiano na utwaaji wa kazi kwa sehemu zinazokamilika. Hata hivyo, hakuna ushahidi uliotolewa kwa wakaguzi wa ukamilishaji wa kazi ambazo hazijakamilika. Hivyo, madai ya kiasi cha Shilingi 327,931,025,254 bado ni halali chini ya kifungu cha 8.7 cha mkataba. Kushindwa kukata fedha ya fidia kwa ajili ya ucheleweshaji wa ukamilishaji wa mradi kulitokana na ufuatiliaji duni wa mkataba kutoka kwa mshauri elekezi wa mradi. Bila ufuatiliaji, wakandarasi wanaweza kupunguza kasi ya ukamilishaji wa kazi kwa wakati, na kusababisha ucheleweshaji wa mradi na kuongezeka kwa gharama za mradi.

**Ninapendekeza TANESCO ihakikishe fidia ya ucheleweshaji wa mradi Shilingi 327,931,025,255 inakatwa kwenye malipo ya mkandarasi ya kazi zinazoendelea.**

## 7.4 Utekelezaji wa Wajibu wa Ushiriki kwa Jamii (CSR)

### 7.4.1 Ucheleweshaji wa Utekelezaji wa Miradi ya Uwajibikaji na Ushirikishaji wa Jamii Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 262.34

Kifungu cha 2.1.6 cha Mkataba wa Uwajibikaji na Ushirikishaji wa Jamii kinataka Shirika la Umeme Tanzania na mkandarasi kufanya na kusaini makubaliano ya kina ya utekelezaji wa miradi ya uwajibikaji kwa kijamii ndani ya mwezi mmoja (1) baada ya kusaini mkataba wa ujenzi wa Mradi wa Ujenzi wa Bawa la Umeme wa Maji la Julius Neyerere. Mkataba huo ulisainiwa tarehe 12 Disemba 2018. Hivyo, makubaliano ya kina yalipaswa kuhitimishwa na kusainiwa tarehe 13 Januari 2019.

Mapitio yangu ya Taarifa ya Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMP) ya mwezi Agosti 2024 na taarifa Na. 66 ya maendeleo ya mradi ya kila mwezi ya mwezi Oktoba 2024 ilibaini ucheleweshaji wa takribani miaka mitano na miezi tisa ya utekelezaji wa miradi ya kijamii yenye thamani ya Shilingi 262,343,199,340. Miradi hiyo ni ya uendelezaji na ujenzi wa vyuo vya ufundi wa umeme, mawasiliano na teknolojia, na afya katika Mkoa wa Kigoma, Chuo cha Umeme Lindi, Chuo cha Afya Tanga; na Chuo cha Afya Dodoma.

Mapitio yangu zaidi yalibaini kuwa miradi ya kijamii awali ilipangwa ikamilike mwezi Juni 2023. Aidha, wakati wa ukaguzi wangu (31 Disemba 2024) miradi hii ya kijamii ilikua haikukamilika ingawa Mradi wa Ujenzi wa Bawa la Umeme wa Maji la Julius Neyerere ulikua unakaribia kukamilika kwa 99.35%.

Hadi wakati wa ukaguzi huu, suala hili lilikuwa linachunguzwa na Timu ya Majadiliano ya Serikali (GNT) ingawa lilikuwa bado halijatatuliwa. Wakati

huohuo, tarehe 11 Oktoba 2024, Shirika la Umeme Tanzania lilituma barua yenye Kumb. Na. DMDPRI/PC/JNHPP/06/528 kwenda Ofisi ya Mwansheria Mkuu wa Serikali ili kupata mwongozo kuhusu suala hilo.

**Ninapendekeza TANESCO ishirikiane na Timu ya Majadiliano ya Serikali (GNT) ili mkandarasi alipe asilimia moja ya bei ya mkataba iliyocheleweshwa kama sehemu ya asilimia nne ya bei ya mkataba kwa ajili ya miradi ya kijamii kwa kutoa barua za madai ili kuharakisha mazungumzo na kutekeleza malipo kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kijamii ili kufikia malengo ya kijamii kwenye mradi huo.**



# SURA YA NANE

## Ukaguzi wa Kiufundi wa Usambazaji Umeme Vijijini

# UKAGUZI WA KIUFUNDI WA USAMBAZAJI UMEME VIJIJINI

## 8.1 Utangulizi

Serikali ya Tanzania inatambua mchango wa sekta ya nishati katika kuchochea ukuaji na kufikia malengo ya kitaifa ikiwemo umeme vijijini ifikapo mwaka 2033. Serikali ilianzisha Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Mfuko wa Nishati Vijijini (REF). Maagizo kupitia rejea Na. CAB/72/416/02) kutoka Wizara ya Nishati ya mwezi Januari 2020 yalizipatia kazi REA na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuunganisha umeme maeneo ya migodi ya madini.

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa kipindi cha kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2023/2024, kwa sababu REA alitekeleza miradi ya umeme katika maeneo ya uchimbaji wa madini, viwanda, na kilimo ili kuongeza upatikanaji wa nishati na kusaidia maendeleo. Ukaguzi pia ulilenga kutathmini ufasaha na ufanisi wa usimamizi wa REA kwa miradi ya umeme vijijini ili kuhakikisha upatikanaji wa nishati endelevu na kuboresha maisha. Tathmini ilifanyika kwa Vipande (Lots) 1, 3, 4, na 5, ikijumuisha maeneo manne muhimu ikiwa pamoja na upangaji wa mradi na usanifu; tathmini ya mahitaji, utoaji, na matumizi ya fedha za mradi; ununuzi wa mkandarasi na vifaa vya umeme; na usimamizi wa mkataba unaojumuisha gharama za mradi, wakati, na vipengele vya ubora, mazingira, kijamii, usalama, usimamizi wa afya, na rasilimaliwatu kwenye miradi ya umeme vijijini.

## 8.2 Mipango na Usanifu wa Mradi

### 8.2.1 Kutokuwapo kwa Utafiti wa Mahitaji ya Nishati ya Umeme

Sehemu ya 3.1 kwenye ukurasa wa 16 wa Upembuzi Yakinifu wa Usambazaji Umeme kwenye Maeneo ya Wachimbaji Wadogo wa Madini, Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji, na Viwanda wa Mwaka 2022 ilisisitiza haja ya kufanya utafiti wa soko la umeme ili kubaini maeneo ambayo hayana umeme, na wateja watarajiwa na kukadiria mahitaji ya umeme. Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa REA hakufanya utafiti huo kama ilivyosisitizwa. Badala yake, alitegemea data kutoka tafiti za awali na dhana zisizo na mahitaji halisi ya nishati ya umeme katika maeneo ya usambazaji umeme. Zoezi hili liliathiri usahihi wa makadirio ya mahitaji ya umeme na utambuzi wa maeneo yasiyo na umeme.

Kutofanyika kwa utafiti kunaweza kuathiri usahihi wa mahitaji ya nishati ya umeme, makadirio ya mahitaji ya nishati ya umeme, na utambuzi wa maeneo yasiyo na nishati ya umeme. Hali hii huongeza hatari ya uzembe katika upangaji kabla ya ujenzi, kama vile makadirio ya chini au kupita kiasi kwa mahitaji ya

umeme, hivyo kusababisha ucheleweshaji wa mradi, kuongezeka kwa gharama, au upotezaji wa rasilimali.

**Ninapendekeza REA afanye utafiti wa kina wa mahitaji ya nishati ya umeme kwa miradi ya siku zijazo ili kuhakikisha utambuzi sahihi wa maeneo yasiyo na nishati ya umeme, wateja watarajiwa, na makadirio sahihi ya mahitaji ya nishati ya umeme. Hali hii itaboresha upangaji na usanifu wa miradi na kuhakikisha kuwa rasilimali zinazotolewa zinaleta tija na ufanisi kulingana na takwimu za kuaminika.**

### 8.2.2 Ongezeko la Gharama ya Shilingi Bilioni 15.34 Kutokana na Maandalizi Hafifu ya Mchanganuo wa Bei za Vipande Vya 1 Hadi 6

Kanuni ya 69(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaitaka taasisi ya ununuzi kutathmini na kukisia mahitaji yake ya bidhaa na huduma na kufanya kazi kwa usahihi kadiri inavyowezekana kuhusu huduma au shughuli, ambazo tayari zimeratibiwa katika mpangokazi wa mwaka na kujumuishwa katika makadirio ya mwaka.

Ukaguzi wangu ulibaini kutofautiana kwa majedwali ya bei ya REA kwenye Vipande 6 kutokana na utofauti wa makadirio ya gharama, mkataba na bei ya mabadiliko ya mkataba. Wigo wa utofauti huo ni kati ya asilimia 3.14 na 32.63 kuzidi makadirio ya mhandisi mshauri, ambapo gharama za makadirio ya Kipande cha 1 na 4 yanazidi makadirio halisi ya bajeti kwa 20% hali inayoleta shaka ya kupatikana kwa thamani ya fedha kwenye mradi, kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 26.**

**Jedwali Na. 26: Ongezeko la gharama za kazi katika Vipande vya 1 hadi 6**

| Kipande | Makadirio (Sh. Bilioni) | Mkataba Uliosainiwa (Sh. Bilioni) | Tofauti[3] (Sh. Bilioni) | Upishano kwa % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 9.04 | 11.99 | 2.95 | 32.63 |
| 2 | 14.31 | 14.99 | 0.68 | 4.75 |
| 3 | 14.36 | 18.05 | 3.69 | 25.70 |
| 4 | 8.15 | 10.46 | 2.31 | 28.34 |
| 5 | 38.27 | 39.47 | 1.20 | 3.14 |
| 6 | 15.81 | 20.33 | 4.52 | 28.59 |
| **Jumla** | **99.94** | **115.28** | **15.34** | **15.37** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi wa mwaka 2024*

[3] Kati ya mkataba uliosainiwa na makadirio

Udhaifu huu ulisababishwa na kutofanyika kwa usahihi wa makadirio ya gharama hali iliyoathiri uwezo wa REA kukataa zabuni hiyo iliyokuwa na gharama za juu kama inavyooneshwa na kifungu cha 59 (2) (d) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011. Hali hii inaongeza hatari ya majadiliano yasiyo na ufanisi na thamani ya mradi yenye shaka.

**Ninapendekeza REA aboreshe usahihi wa makadirio ya gharama kwa kuandaa majedwali ya bei elekezi, kuimarisha mawasiliano kati ya idara za ununuzi na mtumiaji. Pia, REA aimarishe njia bora za kuchambua mapungufu na kuboresha ufanisi wa majadiliano.**

### 8.2.3 REA Kutumia Transifoma Zilizokuwa na Uwezo wa Chini Kuliko Uliopendekezwa Katika Upembuzi Yakinifu

Kifungu cha 39 (1)(b) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 kinaitaka idara tumizi kuandaa michanganuo ya kiufundi kama vile taarifa za mahitaji na/au hadidu za rejea za ununuzi na kuziwasilisha kwenye Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi.

Nilibaini kuwa, upembuzi yakinifu haukujumuisha transifoma za kVA 50 na kupendekeza transifoma zenye uwezo wa kVA 100 na kVA 200 kutumika kwa mikoa yote, na kVA 315 kwa mikoa yote isipokuwa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Simiyu, na Tanga. Hata hivyo, REA aliondoa transifoma za kVA 315 na kuzibadilisha na kVA 50 bila uchunguzi wa mahitaji ya nishati ya umeme. Kuondoa kabisa transifoma zenye uwezo wa kVA 315 na kubadilisha na transfroma zenye uwezo wa kVA 50, kVA 100, na kVA 200 kunaashiria kupuuzwa kwa mahitaji yaliyowekwa awali, hivyo kuhatarisha upungufu wa miundombinu, kukatika kwa umeme, na kushuka kwa uchumi.

REA alifafanua kuwa njia za msongo mdogo wa umeme na wa kati zimejengwa kwa ajili ya upanuzi wa mahitaji ya sasa na ya baadaye, kwa kutumia nyaya za milimita za mraba 100 na 95 za aina ya ABC zinazoingiza na kutoa umeme kwenye gridi. Wakala ulisema kuwa TANESCO inasimamia uwezekano wa upatikanaji wa mahitaji na nguvu za usambazaji umeme baada ya makabidhiano ya miundo kwa nguzo za aina ya H zinazobeba transifoma kubwa zaidi.

Hata hivyo, nilibaini kwamba, hakukuwa na uhalali wa dhamira ya TANESCO ya utoshelevu wa utaratibu huu au ufafanuzi wa kushughulikia upungufu wa uwezo wa transifoma. Hali hii inadhoofisha uwezo wa miundombinu ya umeme kukidhi mahitaji yaliyotabiriwa katika maeneo ya miradi.

**Ninapendekeza REA aweke kipaumbele katika kufanya uchunguzi wa mahitaji ya nishati ya umeme kwa miradi ya siku zijazo ili kuhakikisha utambuzi sahihi wa maeneo ambayo hayajafikishiwa umeme na wateja watarajiwa na makadirio sahihi ya mahitaji ya umeme. Hali hii itaboresha upangaji na usanifu wa miradi na kuhakikisha kuwa rasilimali zinatolewa kwa ufanisi kulingana na data za kuaminika.**

### 8.2.4 Ufungaji wa Vifaa Bila Kufanya Majaribio ya Vipimo Vinavyokubalika Kiwandani

Kifungu cha 7.2 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba na Fomu ya Utaratibu wa Ununuzi Na.14A, inasisitiza kuwa vifaa lazima vipimwe kimajaribio ili kutambua iwapo vinafaa kwa utekelezaji wa miradi. Zaidi ya hayo, wafanyakazi wenye sifa na maabara zinatakiwa kutumika na kushuhudia vipimo kabla ya kutumia vifaa hivyo.

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini kuwa, licha ya kuwapo kwa vifaa ambavyo vilipitia kwenye vipimo vya majaribio na kukubalika, REA aliruhusu matumizi ya vifaa mbadala katika Kipande cha 3 na cha 4, ambavyo havikufanyiwa vipimo vya kukubali katika Mikoa ya Geita, Iringa, Kagera, Mara, Mbeya, Mwanza, Njombe, Rukwa, Simiyu, na Songwe. Vifaa ambavyo havikufanyiwa vipimo ni pamoja na vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya msongo wa umeme, nyaya za msongo wa njia za umeme, na vifaa vya kutuliza athari na mita za umeme.

REA alifafanua kuwa, vifaa ambavyo vilipitia vipimo vya kukubalika havikuingizwa nchini kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO -19. Vifaa hivyo ni pamoja na insuleta, nyaya, nyaya za njia za msongo wa umeme, vifaa vya usaidizi, nyaya za aina ya ACSR, na vifaa vya kutuliza radi ambavyo tayari vilijaribiwa katika Kampuni ya M/S Yueqing Laurence IMP. & EXP. Co. Ltd nchini China, na mita zilizojaribiwa katika Kampuni ya M/S Tanzania Clou Electronics Co. Ltd. Changamoto za mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 zilimfanya mkandarasi Kampuni ya M/S Ok Electrical and Electronics Service Ltd. kuomba kibali kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa REA ili kutumia wasambazaji mbadala wa ndani. Wasambazaji waliopendekezwa ni Kamapuni ya M/S Volex kwa vifaa vya njia za umeme, nyaya, nyaya za njia za umeme, na vifaa vya kutuliza radi; Kampuni ya M/S Everwell kwa nyaya za ACSR; na Kampuni ya M/S Bahdela kwa mita za umeme.

Barua ya tarehe 27 Septemba 2023 yenye Kumb. Na. AG 143/355/04/6 kutoka REA kwenda kwa Kampuni ya M/S Ok Electrical and Electronics Services Limited ilitoa kibali kwa wasambazaji hawa, kwa masharti kwamba mkandarasi awasilishe hati za dhamana na taarifa za ukaguzi. REA alitegemea uthibitisho

wa nyaraka za uingizaji na ukaguzi wa utoaji vifaa kutoka nje bandarini yaani ( PVoC) kabla ya usafirishaji wa nyenzo na vifaa vya njia za usambazaji umeme zilizoagizwa, kama vile insuleta, nyaya, nyaya za njia za umeme, vifaa vya kusaidia kushikilia nguzo, nyaya aina ya ACSR, na vifaa vya kutuliza radi kutoka kwa Kampuni ya Volex Electronics & Decorators Ltd, kinyume na mahitaji ya kupata matokeo ya vipimo vya ubora wa vifaa au dhamana zinazohitajika na ripoti za vipimo vya ubora wa kukubali.

Aidha, ilibainika kuwa, mkandarasi aliomba kutumia mita mbadala kutoka Kampuni ya Bahadela kwa sababu mito hizo zilikuwa zinapatikana ndani ya nchi. Hata hivyo, taarifa ya vipimo vya ubora wa kukubalika ilifanywa na Kampuni ya Tanzania Clou Electronics Co. Ltd, ambayo pia ilikuwa kampuni ya ndani iliyochaguliwa kusambaza vifaa. Kwa mujibu wa ukaguzi wa taarifa za vipimo vya ubora, nilibaini kuwa REA hakuwa na ushahidi wa vipimo vya ubora wa kukubaliwa uliofanywa na Kampuni ya Bahdela.

Kutumia vifaa ambavyo havikupitia au kufaulu vipimo vya kukubalika kunaweza kuwa na athari kubwa za kiufundi kwa ubora wa vifaa na kwa uimara wa mradi au vifaa kama vile insuleta, fyuzi na vifungashio vya kisasa. Vifaa visivyofikia ubora unaotakiwa vinaweza kushindwa kufikia viwango vya utendaji vinavyohitajika, hivyo kuathiri uaminifu wa jumla na uimara wa miundombinu ya umeme.

Hali hii inaweza kusababisha ongezeko la uwezekano wa kushindwa, kama vile kuvunjika au kuharibika kwa vifaa, kushindwa kuwa na uhimilivu wa muundo wa vifaa vya kusaidia radi hivyo kuzimika kwa umeme. Zaidi ya hayo, matumizi ya vifaa visivyothibitishwa huibua wasiwasi juu ya uwezo wake wa kuhimili hali ya mazingira, mahitaji ya mzigo wa umeme, na udhaifu wa uendeshaji, uwezekano wa kusababisha matengenezo ya mara kwa mara, kupunguzwa kwa maisha ya miundombinu ya umeme, na ufanisi duni wa uendeshaji na usambazaji wa umeme.

**Ninapendekeza REA ahakikishe upimaji muhimu unafanywa na kusimamiwa kulingana na kiwango kinachohitajika na kuimarisha udhibiti wa ubora kwa kutekeleza ukaguzi wa mara kwa mara na hatua za kurekebisha ili kuhakikisha uzingatiaji wa masharti ya mkataba wa uwekaji nguzo, usafishaji na uondoaji wa uoto chini ya njia za kusambazia umeme, utunzaji wa nyenzo na hatua za usalama, na kuhakikisha kazi zinafanywa na wafanyakazi wenye sifa.**

### 8.2.5 Mabadiliko yasiyo na nyaraka ya vijiji kwa Kipande cha 3 Katika Mkoa wa Geita

Kifungu cha 13.1 cha Masharti Maalumu ya Mkataba Na. AE/008/2020-22/HQ/W/34 kinataka mabadiliko yoyote yaanzishwe na meneja wa mradi wakati wowote kabla ya kuukabidhi mradi.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa REA alifanya mabadiliko yasiyo na nyaraka katika mawanda ya mradi wa umeme, ikiwa pamoja na kubadilisha vijiji ili vipatiwe nishati ya umeme. Awali upembuzi yakinifu ulitenga Kijiji cha Magema Mkoani Geita kwa ajili ya kuwekewa umeme, lakini wakati wa utekelezaji, REA aliamua kuelekeza mradi katika Kijiji cha Ikumbayaga bila kuweka kumbukumbu za mabadiliko haya kupitia maelekezo ya meneja wa mradi au kibali cha mwajiri, kama inavyotakiwa na Kifungu cha 13.1 cha mkataba.

Hali hii ilisababisha kutofikia lengo lililokusudiwa la kusambaza umeme katika maeneo yaliyotengwa na yaliyolengwa. Mabadiliko hayo ya mawanda yasiyo na nyaraka yalisababishwa na usimamizi usioridhisha wa REA wakati wa uchunguzi uliofanywa na mkandarasi kuhakikisha mradi unatekelezwa katika eneo lililotengwa katika mkataba.

**Ninapendekeza REA atekeleze utaratibu rasmi wa kuandika na kuhalalisha mabadiliko yoyote katika mawanda ya mradi ihakikisha kuendana upembuzi yakinifu wa awali au tafiti za uchunguzi na au kupata vibali vinavyohitajika.**



# SURA YA TISA

## Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano

# UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA MINARA YA MAWASILIANO

## 9.1 Utangulizi

Mwaka 2006, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ili kuboresha upatikanaji wa mawasiliano mijini na vijijini katika maeneo, ambayo hayajafikiwa. Kupitia mfuko huo, serikali imejenga minara ya mawasiliano 2,185 tangu mwaka 2006 ili kutoa huduma za mawasiliano katika kata 1,974 na vijiji 5,111. Chini ya Awamu ya 5, Awamu ya 5A; Ukanda wa Mipakani na Maeneo Maalumu Awamu ya 5 na Awamu ya 6; na Ukanda wa Mipakani na Maeneo Maalumu Awamu ya 6 na Awamu ya 8, UCSAF ulitoa ruzuku ya ujenzi wa minara 515 ya mawasiliano vijijini katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi uliolenga kutathmini iwapo UCSAF ulisimamia ipasavyo ujenzi wa minara ya mawasiliano ili kuhakikisha upatikanaji na uendelevu wa huduma za mawasiliano katika maeneo ya mijini na vijijini, ambayo hayakufikiwa. Ukaguzi ulihusisha miaka minne ya fedha kuanzia 2020/2021 hadi 2023/2024.

## 9.2 Kupanga na Kutambua Maeneo ya Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano katika Maeneo Yasiyofikiwa

### 9.2.1 Kutokuwa na Mipango ya Kutosha Kuhusu Utambuzi wa Maeneo Ambayo Hayajafikiwa na Huduma za Mawasiliano

Kifungu kidogo cha 6(a) cha Sheria ya Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote ya Mwaka 2006 kinautaka UCSAF kutambua maeneo yatakayopatiwa ruzuku. Mapitio yangu yalibaini kuwa mfuko wa upatikanaji wa mawasilano kwa wote haikupanga kufanya utambuzi na kuainisha maeneo mapya yasiyo na huduma za mawasilano katika kipindi cha miaka ya fedha 2021/2022 hadi 2022/2023 kwa ajili ya ujenzi wa minara. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa kanzidata kamili ya maeneo ya vijijini na mijini yasiyo na huduma za mawasilano au yenye huduma duni za mawasilano, bila utaratibu au uhuishaji wa kanzidata kwa kila robo mwaka kama inavyohitajika. Hali hii ilisababisha utambuzi duni wa maeneo yaliyo na huduma hafifu au yasiyofikiwa na huduma za mawasiliano.

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote hupokea taarifa za maeneo yasiyofikiwa kutoka kwa vyanzo kama vile Chama cha Watoahuduma za Mtandao wa Simu Tanzania (TAMNOA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, mamlaka za serikali za mitaa, wabunge, na umma. Ingawa uhakiki wa mara kwa mara wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ulitoa orodha ya maeneo yasiyofikiwa kwa ajili ya

kuzingatiwa katika miradi ya UCSAF, Mamlaka haikupanga utambuzi wa maeneo hayo wala kuchukua hatua zinazohitajika. Maofisa wa mfuko walifafanua kuwa uchaguzi wa maeneo yasiyo na huduma au yasiyofikiwa na huduma za mawasiliano kulitokana na malalamiko yaliyothibitishwa kutoka kwa wabunge na Serikali za mitaa, na kufanya mchakato huo kuwa wa kusubiria na si wa utekelezaji kwa vitendo, ambao ni kinyume na Kifungu cha 6(a) cha Sheria ya Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote ya Mwaka 2006.

Kutokuwapo kwa utambuzi wa kutosha wa maeneo yasiyofikiwa na huduma kulisababisha kupeleka ruzuku ya kiasi cha Shilingi 4,284,985,000 kwa ajili ya ujenzi wa maeneo mapya ambayo tayari yalishafikiwa na huduma. Pia, jumla ya Shilingi 5,763,835,000 zilitolewa kwa maeneo ambayo hayakutambuliwa kama maeneo yasiyofikiwa na huduma kwa Awamu ya 6 na Awamu ya 5 kama inavyoelezwa katika (a) na (b) hapa chini.

**(a) Shilingi bilioni 4.28 zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa minara katika maeneo ambayo tayari yalikuwa yameshafikiwa na huduma**

Mapitio ya miradi ya awamu ya sita ya UCSAF yalibaini kuwa kata 24 zilipewa watoahuduma kwa ajili ya ujenzi wa minara ya mawasiliano kwa gharama ya Shilingi 4,284,985,000. Hata hivyo, kata hizo zilikuwa tayari zina huduma za mawasiliano ambazo zilikuwa zimefanyika kwenye miradi mingine au ileile. Uchambuzi zaidi kwenye **Jedwali Na. 27**.

Mahojiano yangu yalifichua kuwa hali ya ardhi na ukuaji wa idadi ya watu ilikuwa sababu za kurudia kata zilezile kwa watoahuduma tofauti. Aidha, sikupewa ushahidi wowote wa kuhalalisha urudiaji wa kata ambazo tayari zilikuwa zimefikiwa na huduma.

### Jedwali Na. 27: Ruzuku zilizotolewa kwa kata ambazo tayari zilishafikiwa na huduma

| Mkoa | Wilaya | Kata | Awamu ya awali | Awamu Iliyohudiwa | Kiasi Kilichotolewa katika Awamu ya Kwanza (Sh.) | Ruzuku Iliyotolewa katika Awamu Iliyofuata (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | Dodoma | Chihanga | 4 | 8 | 170,000,000 | 320,000,000 |
| | Dodoma | Hombolo Makulu | BSZ PH6 | 8 | 50,000,000 | 170,000,000 |
| | Kondoa | Kalamba | 8 | 8 | 125,000,000 | 145,000,000 |
| Pwani | Rufiji | Chumbi | BSZ PH6 | 8 | 165,000,000 | 174,400,000 |
| | Rufiji | Ngorongo | 1A | BSZ PH 6, 8 | 187,008 | 525,000,000 |
| Tabora | Uyui | Ibiri | 5 | 8 | 114,000,000 | 145,000,000 |
| | Urambo | Itundu | 5 | 8 | 123,500,000 | 145,000,000 |
| Singida | Ikungi | Ighombwe | 5 | 8 | 114,000,000 | 180,000,000 |
| | Manyoni | Mwamagembe | BSZ | 8 | 170,974 | 180,000,000 |

| Mkoa | Wilaya | Kata | Awamu ya awali | Awamu Iliyohudi wa | Kiasi Kilichotolewa katika Awamu ya Kwanza (Sh.) | Ruzuku Iliyotolewa katika Awamu Iliyofuata (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lindi | Mtama | Mandwanga | 4 | BSZ PH6, 8 | 145,000,000 | 360,000,000 |
| | Mtama | Namupa | BSZ PH6 | 8 | 145,000,000 | 360,000,000 |
| | Mtama | Navanga | BSZ PH6 | 8 | 145,000,000 | 360,000,000 |
| | Ruangwa | Matambarale | BSZ PH6 | 8 | 145,000,000 | 320,000,000 |
| Kagera | Biharamulo | Kaniha | 2B | 8 | 30,000 | 145,000,000 |
| Simiyu | Meatu | Kisesa | 5 | 5A | 117,000,000 | 145,000,000 |
| | Masasi | Namwanga | 4 | BSZ PH6, 8 | 123,000,000 | 491,835,000 |
| K'manjaro | Rombo | Tarakea Motamburu | 5 | BSZ PH 6, 8 | 165,000,000 | 118,750,000 |
| **Jumla** | | | | | **1,846,887,982** | **4,284,985,000** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa wakaguzi kwa miradi inayotekelezwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote mwaka 2024*

(b) **Shilingi bilioni 5.76 kutolewa kwa kata ambazo awali hazikutambuliwa kama maeneo yasiyofikiwa na huduma katika Awamu ya 6 na ya 5 za Maeneo ya Mipakani na Ukanda Maalumu**

Mapitio yangu ya miradi ya Awamu ya 5 na 6 yalibaini kuwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote uliwapa ruzuku watoahuduma za mawasiliano kujenga minara ya simu katika kata 39 ambazo awali hazikutambuliwa kama zisizofikiwa na huduma. Kata 24 kati ya 39 alipewa Airtel katika miradi ya Awamu ya 5 na 6 ili ijenge minara ya simu. Kata hizi hazikutambuliwa kama zisizofikiwa na huduma za mawasiliano wala hazikujumuishwa katika mipango ya kila mwaka ya UCSAF. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha kuwa maeneo hayo yalihitaji huduma hizo za kujengewa minara ya mawasiliano. **Jedwali Na. 28** linaonesha maeneo yaliyopewa ruzuku, ambayo awali hayakuwa na huduma za mawasiliano.

### Jedwali Na. 28: Ruzuku kwa maeneo ambayo awali hayakuwa na huduma za mawasiliano

| Awamu | Mtoahuduma | Idadi ya kata | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Awamu 5 | Airtel | 3 | 294,000,000 |
| | MIC (Honora/Tigo) | 1 | 125,000,000 |
| Awamu 6 BSZ | Airtel | 21 | 3,125,000,000 |
| | Vodacom | 3 | 408,000,000 |
| | MIC (Honora/Tigo) | 3 | 491,835,000 |
| | Viettel | 8 | 1,320,000,000 |
| **Jumla** | | **39** | **5,763,835,000** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa wakaguzi kwa orodha ya miradi iliyotekelezwa na mikataba iliyosainiwa kwa mwaka 2024*

**Ninapendekeza menejimenti ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ipitie upya maeneo waliyogawa na yaliyofanyika katika maeneo yaliyotengwa ili kuepuka kutoa ruzuku kwa maeneo, ambayo tayari yalishafikiwa na huduma za mtandao wa simu.**

## 9.3 Usimamizi wa Ununuzi

### 9.3.1 Fedha za Ruzuku Shilingi Bilioni 7.17 Zilizogawiwa Kuzidi Kiwango cha Juu Kinachoruhusiwa kwa Miradi ya Awamu ya Nane

Jedwali Na. 1 Sehemu ya Kwanza (iv) ya hati ya zabuni iliyotolewa na UCSAF kwa ajili ya utoaji wa huduma za mawasiliano inaainisha kiasi cha ruzuku kilichotengwa na Mfuko kwa kila eneo au kata iliyoteuliwa.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa Kampuni za Airtel na MIC Tanzania Limited (Yas) zilipewa zaidi ya kiwango cha juu cha ruzuku kinachoruhusiwa, jumla ya Shilingi 7,171,000,000 (yaani Kampuni ya MIC Shilingi 6,995,000,000 na Kampuni ya Airtel Shilingi 176,000,000). **Jedwali Na. 29** linaonesha tofauti kati ya ruzuku zilizotengwa na zilizotolewa .

**Jedwali Na. 29: Tofauti kati ya ruzuku zilizotengwa na zilizotolewa**

| Mtoahuduma | Idadi ya kata/ maeneo yaliyogawiwa | Ruzuku iliyotengwa (Sh.) | Ruzuku iliyotolewa (Sh.) | Tofauti (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| Airtel | 50 | 10,020,700,000 | 10,196,700,000 | 176,000,000 |
| TTCL | 100 | 32,000,000,000 | 32,000,000,000 | - |
| Vodacom | 53 | 9,490,000,000 | 9,490,000,000 | - |
| MIC | 38 | 6,685,000,000 | 13,680,000,000 | 6,995,000,000 |
| **Jumla Ndogo (Kuongezeka kwa Ruzuku)** | | **58,195,700,000** | **65,366,700,000** | **7,171,000,000** |
| Viettel | 34 | 4,986,800,000 | 4,980,000,000 | (680,000,000) |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa wakaguzi kwa hati ya zabuni na mikataba ya Awamu ya 8, mwaka 2024.*

Jedwali linaonesha kuwa gharama za ruzuku kwa ajili huduma za mawasiliano Awamu ya 8 zilizidi kiasi kilichotengwa kwa Shilingi 6,995,000,000 kwa Kampuni ya MIC na Shilingi 176,000,000 kwa kampuni ya Airtel sawa na jumla ya Shilingi 7,171,000,000. Jedwali linaonesha pia kwamba, Shirika la Simu Tanzania (TTCL) na Kampuni ya Vodacom hazikuwa na ongezeko, wakati Kampuni ya Viettel ilipokea ruzuku chini ya kiwango kilichotengwa cha Shilingi 680,000,000.

Gharama za ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa minara ya mawasiliano ya simu kwa maeneo ya kata/maeneo yaliyotengwa ziliongezeka kwa Shilingi 7,171,000 hivyo kuathiri mtiririko wa fedha wa UCSAF. Hali hii ilithibitishwa na Mfuko kushindwa kulipa malipo kamili ya awali ya Shilingi 22,400,000,000 kwa watoahuduma. Badala yake, Mfuko uliweza kulipa malipo ya awali Shilingi 15,600,000,000 na kushindwa kulipa Shilingi 6,800,000,000.

Mahojiano yaliyofanyika kati ya timu ya ukaguzi na menejimenti ya UCSAF yalionesha kuwa mgao wa ruzuku kwa Kampuni ya MIC Tanzania Limited ulitokana na mapendekezo ya minara mingi kwa kila kata ili kuimarisha mawasiliano ya simu. Wakati kamati ya tathmini ilihalalisha hili, ukaguzi uligundua kwamba ni upendeleo tu uliotumika kwa Kampuni ya MIC, na gharama zake zilizidi kiwango cha ruzuku kilichowekwa kwa Shilingi 155,000,000 kwa kila eneo la ujenzi. Utoaji wa ruzuku kwa kila eneo la ujenzi badala ya eneo lililotengwa ulikinzana na ukomo na mahitaji ya zabuni za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, na unathibitisha kuwa ni mara ya kwanza kwa njia hii ilitumika ikiinufaisha Kampuni ya MIC Tanzania Limited pekee.

**Ninapendekeza UCSAF uzingatie kiasi cha ruzuku kilichotengwa kwa kila eneo au kata ili kupunguza ongezeko la gharama za uendeshaji wa utoaji wa huduma za mawasiliano.**

### 9.3.2 Kutolewa Fedha Shilingi Bilioni 1.75 Kama Ruzuku kwa Ajili ya Ujenzi wa Minara Katika Kipande cha 14 Ambacho Tayari Kilipatiwa Ruzuku na Kilishafikiwa na Huduma za Mtandao

Kifungu kidogo 6(a) cha Sheria ya Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote ya Mwaka 2006 kinautaka UCSAF kutambua maeneo yatakayopatiwa ruzuku.

Nilibaini kuwa kata 14 kati ya 66 zilizoruhusiwa kupewa ruzuku zilitolewa kwa wazabuni waliofanikiwa kupata zabuni za ujenzi wa minara katika maeneo ambayo tayari yalishafikiwa na huduma za mtandao. Kata hizo 14, ambazo tayari zilikuwa na mtandao wa mawasiliano, ziligawiwa na kustahiki ruzuku ya Shilingi 1,756,290,000 bila uthibitisho. Kasoro hii ingeweza kuepukwa kwa uthibitisho sahihi. **Jedwali Na. 30** linaonesha kata, ambazo zilishafikiwa na huduma za mtandao lakini zilipewa ruzuku.

**Jedwali Na. 30: Kata ambazo zilishafikiwa na huduma za mtandao lakini zilipewa ruzuku**

| Halmashauri | Kata | Kijiji | Bei Nukuu (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Mbogwe | Iponya | Iponya | 125,000,000 |
| Karagwe | Bweranyange | Chamchuzi | 125,000,000 |

| Halmashauri | Kata | Kijiji | Bei Nukuu (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Karagwe | Nyakakika | Kaiho | 125,000,000 |
| Karagwe | Rugu | Ruhita | 125,000,000 |
| Kakonko | Gwarama | Gwarama, Kabare, Nyakiyobe | 160,050,000 |
| Gairo | Nongwe | Tarafa Nongwe HQ | 99,875,000 |
| Masasi | Mchauru | Maparawe, Mtuma, Mwitika | 131,835,000 |
| Masasi | Mkululu | Songambele | 99,875,000 |
| Masasi | Namwanga [Mkundi] | Chipango, Mkolopola, Nakalola, Nangwale | 131,835,000 |
| Ludewa | Lupingu | Lupingu | 104,750,000 |
| Nyasa | Chiwanda | Mtupale, Ng'ombo | 121,510,000 |
| Songea | Ndongosi | Nambendu | 125,000,000 |
| Bariadi | Nkololo | Mwamoto, Nkololo, Bubale, Mwabadimu | 160,050,000 |
| Ileje | Chitete | Chitete, Ikumbilo | 121,510,000 |
| **Jumla** | | | **1,756,290,000** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Taarifa ya Tathmini ya Mkaguzi ya Mwaka 2024*

Ugawaji wa maeneo kwa wazabuni, ambayo tayari yalishafikiwa na huduma za mtandao kulisababibishwa na udhaifu katika utambuzi wa maeneo yasiyo na mtandao wa mawasiliano. Kasoro hii ilisababisha ongezeko la gharama kwa mradi huo kiasi cha Shilingi 1,756,290,000.

**Ninapendekeza UCSAF uthibitishe mitandao ambayo haipo katika maeneo/kata zilizoteuliwa ambazo tayari zimepewa ruzuku ili kupunguza hatari ya kugawa ruzuku maradufu kwenye eneo moja la ujenzi wa mtandao.**

## 9.4 Usimamizi wa Mkataba

### 9.4.1 Fedha Shilingi Bilioni 3.80 Kutotolewa Kama Fidia ya Ucheleweshaji wa Ukamilishaji wa Miradi ya Minara Awamu za 5, 5a, 6, na Maeneo ya Mipakani na Ukanda Maalumu, Awamu ya 6

Kifungu cha 26.1 cha Masharti Maalumu ya Mikataba kinataka kukata kiwango cha fidia ya ucheleweshaji wa kumaliza kazi kwa moja ya kumi ya asilimia moja (yaani 0.1%) ya ruzuku ya mkataba wa mwisho kutokana na kuchelewa kutekeleza mkataba.

Mapitio yangu yalibaini kuwa jumla ya Shilingi 3,803,279,079 kama fedha ya fidia ya miradi ya Awamu ya 5, 5A, 6, na Maeneo ya Mipakani na Ukanda Maalumu Awamu ya 6 kutokana na kuchelewa kwa utekelezaji wa mkataba. Kiasi hiki ni pamoja na Shilingi 729,110,225 kwa Awamu ya 5; shilingi 32,480,000 kwa Awamu ya 5A; na Shilingi 1,088,000,000 kwa Maeneo ya Mipakani na Ukanda Maalumu Awamu ya 6. **Jedwali Na. 31** linaonesha kiasi cha fidia ambacho hakikudaiwa.

**Jedwali Na. 31: Madai ya fidia yasiyodaiwa**

| Awamu | Mtoahuduma | Idadi ya Siku Zilizochelewa | Kiasi Kisichodaiwa (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 5 | Vodacom, Honor (Tigo) & Airtel | 2 -443 | 729,100,225 |
| 5A | Airtel for Mtwara (Lukuledi) | 224 | 32,480,000 |
| 6 | TTCL | 529 - 865 | 1,088,000,000 |
| BSZPH6 | Vodacom, Honora (Tigo), Airtel, TTCL & Halotel | 14 - 767 | 1,953,688,854 |
| **Jumla** | | | **3,803,279,081** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa wakaguzi kwa hali ya malipo na kazi zilizotekelezwa hadi mwezi Septemba 2024*

Mapitio na mahojiano kati yangu na menejimenti ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote yalibaini kuwa fidia ya ucheleweshaji wa mradi kwa siku mbili hadi 767 haikudaiwa kwa sababu Mfuko ulikusudia kuimarisha uhusiano mzuri kati yake na watoahuduma. Kutokana na hali hiyo, watoahuduma hao walisita kutoa huduma za mawasiliano katika maeneo ya vijijini, na Mfuko ulishawishika tena kutoa zabuni kwa watoahuduma haohao kwa miradi mingine waliyoalikwa kuomba zabuni.

Kushindwa kudai fidia ya kuchelewa kukamilisha miradi kunapunguza fursa ya Mfuko kupata fidia kwa miradi iliyocheleweshwa. Watoahuduma walisita kutumikia maeneo ya vijijini kutokana na umbali na faida ndogo, wakihitaji Mfuko kuwashawishi kuomba zabuni. Hata hivyo, niligundua kuwa Mfuko ulishindwa kutathmini faida ya maeneo ya ruzuku na idadi ya watumiaji. Kutozingatia masharti ya mkataba kulisababisha upotevu na hasara kwa serikali.

**Ninapendekeza UCSAF itekeleze kipengele cha mkataba na kukata fidia ya ucheleweshaji wa miradi "*liquidated damages*" kwa watoahuduma na kuhakikisha mikataba inakamilika kwa wakati.**

### 9.4.2 Malipo ya Awali ya Shilingi Bilioni 12.80 Kulipwa Bila Dhamana ya Benki

Kifungu cha 36.1 cha Masharti Maalumu ya Mikataba kinataka kwamba 70% ya ruzuku ya mkataba kama malipo ya awali yalipwe dhidi ya uwasilishaji wa dhamana ya benki au dhamana ya bima ya thamani sawa na asilimia hiyo.

Mapitio yangu yalibaini kuwa kiasi cha Shilingi 12,803,295,000 kililipwa kwa watoahuduma bila dhamana ya benki inayotakiwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 32.**

**Jedwali Na. 32: Malipo ya awali yaliyofanywa bila dhamana ya benki**

| Awamu ya mradi | Mtoahuduma | Namba ya hati ya malipo | Malipo ya awali (sh.) |
|---|---|---|---|
| 5 | Tigo | T2290000V2300269 | 695,385,000 |
| 5A | Airtel | T2290000V2301867 | 464,000,000 |
| 6 | TTCL | T2290000V2301327 | 224,000,000 |
| BSZPH6 | Halotel | T2290000V2401143 | 792,000,000 |
| | Vodacom | T2290000V2500423 | 957,310,000 |
| | TTCL | T2290000V2200056 | 94,600,000 |
| 8 | Tigo | T2290000V2400893 | 9,576,000,000 |
| **Jumla ya malipo ya awali kulipwa bila dhamana ya benki** | | | **12,803,295,000** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Wakaguzi wa malipo ya awali kwa watoahuduma za mawasiliano bila dhamana ya benki, 2024*

Mahojiano yangu yalibaini kuwa watoahuduma waliepuka kushikilia fedha za ziada katika benki ili kuwapo na wepesi wa mabadiliko ya uendeshaji huduma. Hata hivyo, malipo yaliyofanywa bila kuwasilisha dhamana ya benki au dhamana ya bima yana hatari kubwa katika urejeshaji fedha walizokopeshwa au fidia ikiwa kuna migogoro, utendaji duni au uvunjivu wa mkataba.

**Ninapendekeza UCSAF uwaelekeze watoahuduma kuwasilisha dhamana za benki kwa malipo ya awali yaliyofanywa kwa watoahuduma.**

### 9.4.3 Miradi Iliyotekelezwa Bila Mikataba ya Shilingi Bilioni 1.04

Kifungu kidogo cha 69(7 na 8) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2023 kinataka kwamba, zabuni, ofa au pendekezo linapokubaliwa na Afisa Masuuli, taasisi nunuzi na mzabuni aliyefaulu lazima waingie makubaliano ya mkataba rasmi. Muundo wa mkataba utajumuisha masharti ya jumla na masharti yaliyoainishwa katika hati za zabuni.

Mapitio yangu yalibaini kuwa maeneo nane ya mradi kwa Awamu ya 5, 5A, 6, na awamu ya 6 ya mipakani na kanda maalumu yenye thamani ya Shilingi 1,041,172,000 yalitekelezwa bila mikataba kama ilivyooneshwa **Jedwali Na. 33.**

**Jedwali Na. 33: Miradi ya minara ya mawasiliano iliyotekelezwa bila ya mikataba**

| Awamu ya mradi | Mtoahuduma | Idadi ya maeneo | Kiasi cha mkataba (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 5 | Tigo | 1 | 125,000,000 |
| 5A | Airtel | 1 | 145,000,000 |
| 6 | TTCL | 1 | 320,000,000 |
| BSZPH6 | Halotel, Vodacom, and TTCL | 5 | 451,172,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jumla** | | **8** | **1,041,172,000** |

***Chanzo:*** *Mikataba iliyosainiwa kati ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na watoahuduma na kanzidata ya miradi kuanzia mwezi Septemba 2024*

Upungufu huu uliotokana na kutotambuliwa kwa maeneo ambayo hayakupata huduma za mawasiliano ulichangia kujitokeza kwa maeneo muhimu ya kupewa ruzuku katikati ya utekelezaji wa mradi. Kuchelewa kwa kukamilika kwa nyongeza ya mikataba na UCSAF kunachangiwa na upungufu katika ushiriki wa watoahuduma na usimamizi wa mikataba.

**Ninapendekeza UCSAF uhakikishe kuwa maombi ya zabuni ya awali ya watoahuduma wanaohusika yanazingatiwa kikamilifu ili kuwa na mikataba na majukumu fungamanishi ya kimkataba.**

## 9.5 Ubora wa Huduma za Mawasiliano kwa Minara Iliyojengwa

### 9.5.1 Miradi Iliyothibitishwa Kuwa Hewani Kutofikia Viwango vya Upatikanaji Wa Mtandao na Kutofikia Viwango vya Ubora

Kanuni ya 9 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma) ya Mwaka 2018 inahitaji kwamba Majaribio ya Kibali cha Muda (PAT) yafanywe ili kuthibitisha viwango vya ubora wa upatikanaji wa simu kuwa zaidi ya 99% na kiwango cha mafanikio ya simu kuwa zaidi ya 95%.

Kinyume na hitaji hilo, wakati wa uhakiki wangu wa tovuti na utekelezaji wa PAT, nilibaini kuwa maeneo sita kati ya 13 yaliyojengwa na kuwekwa hewani yalikuwa na upatikanaji wa simu wa chini ya 99%. Upatikanaji wa mtandao katika maeneo hayo sita ulikuwa kati ya 55.32% na 96.3%, kinyume na mahitaji. Matokeo ya PAT pia yalionesha kuwa maeneo matatu kati ya 13 yaliyo hewani hayakufikia kiwango cha mafanikio ya simu cha 95%. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye **Jedwali Na. 34**.

**Jedwali Na. 34: Miradi iliyothibitika kuwa hewani lakini haikufikia viwango**

| Halmashuri | Jina la eneo lililojengwa/kata | Upatikanaji wa mtandao (%) | Hali ya matokeo ya vipimo (>99=faulu; and <99=feli) | Hali ya matokeo ya mtihani juu ya kiwango cha mafanikio ya simu (>95=faulu; na <95=feli) |
|---|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Rombo | Tarakea, Motamburu | 86.11 | Haukufikia viwango | Haukufikia viwango |

| Halmashuri | Jina la eneo lililojengwa/kata | Upatikanaji wa mtandao (%) | Hali ya matokeo ya vipimo (>99=faulu; and <99=feli) | Hali ya matokeo ya mtihani juu ya kiwango cha mafanikio ya simu (>95=faulu; na <95=feli) |
|---|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe | Kurui | 55.32 | Haukufikia viwango | Haukufikia viwango |
| Halmashauri ya Wilaya ya Msalala | Jana | 69.23 | Haukufikia viwango | Haukufikia viwango |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mlele | Kamalampaka, Inyonga | 96.3 | Haukufikia viwango | Haukufikia viwango |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mlele | Songambele, Kamsisi | 61.54 | Haukufikia viwango | Haukufikia viwango |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa | Mpwapwa mjini | 90.18 | Haukufikia viwango | Haukufikia viwango |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa wakaguzi wa upimaji uliofanywa wakati wa ziara za maeneo yalijengwa minara mwaka 2024*

Ninahusisha hitilafu hii na upungufu katika upangaji na udhibiti wa ubora wakati wa ujenzi wa minara ya mawasiliano. Matokeo yake, maeneo yaliyokusudiwa kupata mtandao yanakumbwa na hitilafu za huduma, jambo linalosababisha kutoridhika kwa walengwa.

**Ninapendekeza UCSAF ufuatilie uendelevu wa minara ya mawasiliano ili kuhakikisha mwendelezo wa utoaji wa huduma bora za mawasiliano.**

### 9.5.2 Asilimia 42 ya Maeneo ya Kazi Yaliyokamilika Hayakufanyiwa Vipimo vya Kuthibitisha Ubora wa Kazi

Kwa mujibu wa mikataba kati ya UCSAF na watoa huduma kwa kipindi cha 2020/21-2023/24, UCSAF inapaswa kukagua maeneo yaliyokamilika kupitia Majaribio ya Kibali cha Muda (PAT) ili kuhakikisha yanakidhi viwango vinavyohitajika na ubora wa huduma.

Hadi Septemba 2024, UCSAF ilikuwa haijafanyia majaribio maeneo 119 kati ya 281 (sawa na 42%). Aidha, ni 12% tu ya maeneo yaliyopimwa ndiyo yalifanyiwa ukaguzi ndani ya miezi mitatu baada ya kukamilika, huku 88% yakichukua muda mrefu zaidi.

Zaidi ya hayo, baada ya kipindi cha miezi tisa cha huduma ya muda, UCSAF haikuzindua rasmi miradi 93 kati ya 141 iliyokuwa imefaulu PAT. Kwa ujumla,

PAT zilifanyika katika chini ya nusu ya maeneo yaliyokamilika kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 35**.

**Jedwali Na. 35: Maeneo ya kazi yaliyokamilika bila kufanyiwa vipimo vya kuthibitisha ubora**

| Awamu ya Mradi | Jumla ya Idadi ya Maeneo Yaliyokamilishwa | Hali Halisi ya Vipimo vya Viwango Vinavyokubalika | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Zilizofanywa | Hazikufanywa | Asilimia ya Vipimo vya Kiwango cha Kukubalika Haijafanywa |
| BSZPH5 | 32 | 19 | 13 | 41 |
| BSZPH6 | 94 | 76 | 18 | 19 |
| 5 | 62 | 62 | 0 | 0 |
| 5A | 7 | 5 | 2 | 29 |
| 6 | 26 | 0 | 26 | 100 |
| 8 | 60 | 0 | 60 | 100 |
| **Jumla** | **281** | **162** | **119** | **42** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi wa maeneo ya ujenzi wa minara ya UCSAF wa mwezi Septemba 2024*

Uchunguzi wa ziada na mahojiano yaliyofanywa mnamo Agosti 2024 yalibaini kuwa sababu za ucheleweshaji wa PAT zilikuwa ratiba ya ukaguzi wa kila robo mwaka, ugumu wa kufikia maeneo ya mbali, na ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi. Kwa mfano, PAT kwa Kisiwa cha Rubondo 2 na Maisome jijini Mwanza, zilizojengwa na TTCL, hazikufanyika kutokana na ugumu wa kufikika kwa maeneo hayo.

Ukosefu wa PAT ya kutosha unaweza kusababisha hitilafu za mfumo zisizogundulika, kutokuwa na ufanisi, na kutokidhi vigezo vya utendaji. Hali hii inaweza kupelekea gharama kubwa za marekebisho, usumbufu wa uendeshaji, hatari za kiusalama, na matatizo ya kisheria.

**Ninapendekeza UCSAF ufuate mbinu na njia za ufanyaji wa vipimo vya muda wa kukubalika kwa wakati unaofaa ili kuhakikisha ugunduzi wa mapema wa hitilafu katika utoaji huduma za mawasiliano na kupendekeza marekebisho yafanyike mapema.**



# SURA YA KUMI

## Ukaguzi wa Kiufundi wa Udhibiti na Ufuatiliaji wa Tathmini ya Athari za Mazingira Katika Sekta za Ujenzi na Madini

# UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UDHIBITI NA UFUATILIAJI WA TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA KATIKA SEKTA ZA UJENZI NA MADINI

## 10.1 Utangulizi

Sekta za ujenzi na uchimbaji madini ni muhimu kwa uchumi wa nchi. Sekta ya madini pekee ilichangia asilimia 7.2, asilimia 7.25, asilimia 8.9, na asilimia 9 katika pato la taifa kwa mwaka 2020, 2021, 2023, na 2024 mtawalia. Hata hivyo, sekta zote mbili zimechangia kwenye uharibifu wa mazingira kutokana na utekelezaji duni wa tathmini ya athari za mazingira (EIAs) na mipango ya usimamizi wa mazingira (EMPs).

Nilifanya ukaguzi huu ili kutathmini kanuni na ufuatiliaji unaofanywa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na ufuatiliaji wa tathmini ya athari za mazingira na mipango ya usimamizi wa mazingira katika sekta hizi. Ukaguzi huu ulihusisha miaka mitano ya fedha kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2023/2024.

## 10.2 Mchakato wa Usajili na Uchunguzi

### 10.2.1 NEMC Haikufuatilia kwa Ufanisi Michakato ya Usajili na Uchunguzi

Sehemu ya Nne ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Tathmini na Ukaguzi wa Athari kwa Mazingira) pamoja na (Marekebisho ya Mwaka 2018) inataka miradi yote ifanyiwe mchakato wa usajili na uchunguzi kwa kutathmini masuala ya asili, ukubwa, eneo, na unyeti wa mazingira.

Nilibaini kuwa NEMC halikufuatilia ipasavyo usajili na uhakiki wa miradi ya ujenzi na uchimbaji madini, hususani miradi ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Daraja la John Pombe Magufuli, Mgodi wa Chokaa wa Dangote, na Mfumo Mpya wa Maji Jijini Arusha. Upungufu huu ulidhihirishwa na ukweli kwamba hadidu za rejea na ripoti za mawanda na wigo hazikuandaliwa vyema, hasa katika kutambua wadau, hivyo kusababisha ushirikishaji duni na kukosa taarifa kama vile data za msingi.

Aidha, nilibaini kuwa miradi ya Mgodi wa Makaa ya Mawe ya Ngaka na Daraja la John Pombe Magufuli ilianza shughuli za ujenzi bila cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira. Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka ulianza tarehe 18 Machi 2021 hadi tarehe 3 Mei 2023, wakati ujenzi wa Daraja la John Pombe Magufuli ulianza tarehe 20 Februari 2020 hadi tarehe 11 Machi 2021 bila kusajiliwa na Baraza la Usimamizi wa Mazingira na kupitisha tathmini ya athari za mazingira. Hali hii inamaanisha kuwa masuala muhimu ya kimazingira, kama vile data za

msingi kuhusu ubora wa maji, hewa, mimea, wanyama, viumbe, na ubora wa udongo hayakuzingatiwa vya kutosha.

Tathmini ya athari za kimazingira isiyokamilika husababisha kutotambua athari za kimazingira zinazosababishwa na utekelezaji wa miradi na hatua zinazofaa za kupunguza athari hizo. Kasoro hii ilitokana na tathmini ya athari za mazingira kutokuwa kamilifu, iliyokosa vipengele muhimu vya udhibiti, na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira kutopitia vya kutosha utayarishaji wa data za msingi. Zaidi ya hayo, kusajili wa Awamu ya 2 na ya 3 kama mradi mmoja hakukuzingatia matakwa mahususi ya kimazingira. Taarifa ya mawanda na hadidu za rejea ilikosa ushirikishaji wa kutosha wa wadau, hivyo kuacha wahusika muhimu ambao walipaswa kuhusishwa. Matokeo yake, tathmini ya athari za kimazingira haikufanywa kabla ya kuanza kwa mradi.

**Ninapendekeza NEMC iandae hatua za utayarishaji wa hadidu za rejea na ihakikishe kwamba zinafuatwa ipasavyo katika mchakato wote wa tathmini ya athari za mazingira.**

### 10.2.2 Utayarishaji Hafifu wa Taarifa za Msingi

Kifungu cha 18(1)(c) cha Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Tathmini na Ukaguzi wa Athari kwa Mazingira) (marekebisho ya mwaka 2018) kinamtaka mwendelezaji au mtetezi kuwasilisha taarifa ya athari za mazingira kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira.

Hata hivyo, mapitio yangu ya taarifa za athari za mazingira yalibaini kuwa miradi mitano kati ya minane ilikosa taarifa za msingi za kutosha. Taarifa zilizokosekana pia zilijumuisha muhtasari wa taarifa za msingi na maelezo mengine yoyote muhimu kuhusiana na mradi huo. Miradi hii mitano ambayo ni Mgodi wa Almasi wa Williamson, Mgodi wa Makaa ya Mawe Ngaka, Mgodi wa Dhahabu Buzwagi, Daraja la John Pombe Magufuli, na Mtandao Mpya wa Maji Jijini Arusha haikuwa na taarifa za msingi za kutosha. Hususani, nilibaini kuwa masuala yafuatayo hayakuwamo katika maelezo ya msingi:

(a) **Miradi mitano kati ya nane iliyotembelewa ilikuwa imewasilisha taarifa za msingi bila vyanzo vya kuaminika**

Nilikagua taarifa za tathmini ya athari za kimazingira na kijamii zilizohusisha data za msingi kama vile ubora wa maji, udongo, hali ya hewa, uoto ardhi na mimea, mionzi, tetemeko la ardhi, viumbe, uchumi wa jamii, na miundombinu. Hata hivyo, data za msingi hazikunukuliwa vya kutosha na kutokuwa na vyanzo vya kuaminika vya uthibitishaji wa data hizo. Hali hii ilitokana na mchakato

dhaifu wa mapitio ya taarifa za tathmini ya athari za kimazingira na kijamii uliofanywa na Baraza la Taifa la Usiamizi wa Mazingira, hivyo kusababisha kupitishwa kwa taarifa zisizo na viwango. Hivyo, taarifa za msingi zisizotegemewa zinahatarisha ufuatiliaji na kupungua kwa tathmini ya mazingira katika kipindi chote cha maisha ya mradi.

(b) **Takwimu za msingi za chuma kizito katika sampuli za maji hazikuchambuliwa kwa Mradi wa Mgodi wa Almasi wa Williamson na Mradi Mpya wa Mtandao wa Maji Jijini Arusha**

Waendelezaji wa Mgodi wa Almasi wa Williamson na Mradi wa Mtandao Mpya wa Maji hawakuchambua au kuanzisha vigezo vya msingi vya chuma kizito katika sampuli za maji zilizokusanywa, badala yake walizingatia vipengele kama vile upitishaji wa umeme (electric conductivity), jumla ya vitu vigumu vilivyoyeyushwa (total disolved solids), oksijeni iliyoyeyushwa (dissolved oxygen), uwezekano wa kupunguza oksidesheni (oxygen reduction potential), chumvichumvi, na asidi pamoja na vimelea mbalimbali. Licha ya sampuli kuchukuliwa kutoka maeneo muhimu, yakiwemo maeneo ya uchimbaji madini, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lilishindwa kuhakikisha ufuatiliaji madhubuti wakati wa utafiti wa kihaidrolojia ili kuthibitisha kuwa kanzidata za msingi kama vile kadmimu, kloromimu, risasi, urani, zinki, na chuma kizito zilijaribiwa na kuripotiwa. Hali hii ni kinyume na aya ya 3.12 ya Mwongozo wa Udhibiti wa Ubora wa Maji na Usafi wa Maji wa Mwaka 2020, ambao unaamuru vigezo vya upimaji kulingana na shughuli za binadamu.

Upungufu huu ulitokana na mapitio duni ya tathmini ya athari za mazingira, kama hadidu za rejea ilivyopuuza uchambuzi wa chuma kizito, ikionesha kushindwa kufanya kwa ukamilifu tathmini ya athari za mazingira na jamii. Kukosekana kwa data za msingi za chuma nzito katika sampuli za maji ya chini ya ardhi na maji yaliyo juu ya aridhi kunaweza kuathiri ukaguzi wa mazingira kwa miaka ijayo, bila kuacha alama ya kuamua iwapo vifaa vilivyojengwa vinachangia kuzamisha chuma kizito katika vyanzo vya maji vya ardhini au karibu na vyanzo vya maji.

**Ninapendekeza NEMC iimarishe njia za uthibitishaji na uhakikishaji wa taarifa zilizowasilishwa katika taarifa za athari kwa mazingira.**

## 10.3 Mapitio ya Taarifa ya Athari kwa Mazingira

### 10.3.1 NEMC Kutopitia kwa Kina Taarifa ya Athari za Mazingira

Sehemu ya VI ya Tathmini ya Athari za Mazingira na Kanuni za Ukaguzi za Mwaka 2005 (iliyorekebishwa mwaka 2018), inataka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira kupitia kwa kina taarifa ya athari za mazingira.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini upungufu katika ukaguzi wa mchakato wa tathmini ya athari za mazingira uliofanywa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira kama vile utambuzi wa athari, utabiri, na hatua za kupunguza athari, ambazo hazikufikia hatua zote za utekelezaji wa mradi, uthibitishaji hafifu wa maeneo ya ujenzi, na ushirikishaji mdogo wa wadau katika ukaguzi na mapitio ya taarifa za tathmini ya mazingira.

Ilibainika kuwa mradi wa Mgodi wa Almasi wa Williamson ulitambua athari za mazingira, ulitabiri, na kupendekeza hatua za kina za kupunguza athari. Hatua za kupunguza athari za kimazingira kwa miradi mingine saba hazikujulikana na zilikosa mipango ya utekelezaji, ambayo ingeweza kupunguza ufanisi wao katika kushughulikia masuala ya kimazingira. Hali hii inaongeza hatari ya madhara ya mazingira, kama vile uchafuzi wa mazingira na usumbufu kwa wakazi.

Aidha, nilibaini kuwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira halikuhusisha wadau vya kutosha wakati wa ukaguzi wa taarifa za athari za Mazingira kwa miradi iliyotembelewa, ambayo ni Mgodi wa Makaa ya Mawe Ngaka, Mtandao Mpya wa Maji Jijini Arusha, Mgodi wa Chokaa wa Dangote, Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya 3, Mgodi wa Dhahabu Buzwagi, na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato, isipokuwa Mgodi wa Almasi wa Williamson. Wakati wadau kama mamlaka za serikali za mitaa na wawakilishi wa jamii walitambuliwa katika hadidu za rejea, hakukuwa na ushahidi wa mashirikiano yaliyohusisha vikundi hivi katika mchakato wa tathmini ya athari za kimazingira. Kwa kuongezea, hakukuwa na matangazo kwa umma yaliyotolewa kualika umma kutoa maoni yao kwenye ripoti za tathmini ya athari za mazingira.

Aidha, nilibaini kuwa NEMC haikufanya uhakiki wa maeneo yanayotakiwa ili kutathmini maeneo ya miradi kwa ajili ya miradi ya sampuli ikiwemo Mtandao Mpya wa Maji Jijini Arusha, Mgodi wa Chokaa wa Dangote, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, na Mgodi wa Almasi wa Williamson isipokuwa miradi ya Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya 3, Mgodi wa Makaa ya Mawe Ngaka, na Daraja la John Pombe Magufuli. Hali hii inaibua wasiwasi kuhusu umakini na usahihi wa ukaguzi wa athari za mazingira iwapo uthibitishaji wa maeneo ya ujenzi wa miradi ungeruhusu NEMC iruhusiwe moja kwa moja kuthibitisha taarifa za mwendelezaji au mmiliki wa mradi katika taarifa za

athari za mazingira. Bila ziara hizi, athari za mazingira na kijamii hazikutambuliwa na kupunguzwa, hivyo kuathiri uendelevu wa mazingira kwenye miradi husika.

**Ninapendekeza NEMC iboreshe mchakato wa tathmini ya mazingira kwa kuhakikisha utambuzi wa kina wa athari, utabiri, na hatua za kupunguza madhara katika hatua zote za utekelezaji wa miradi. Hii inapaswa kujumuisha ukaguzi wa kutosha wa maeneo kwa miradi yote iliyochaguliwa ili kutathmini moja kwa moja athari za kimazingira na kuthibitisha taarifa za waendelezaji katika Taarifa za Athari za Mazingira.**

**NEMC inapaswa pia kuimarisha ushirikishwaji wa wadau kwa kuhakikisha yanafanyika mashauriano yenye tija na Mamlaka za Serikali za Mitaa, wawakilishi wa jamii, na umma, hasa wakati wa mchakato wa tathmini za mazingira. Matangazo ya umma yanayowaalika kutoa maoni yanapaswa kutolewa mara kwa mara ili kuhakikisha uwazi na ushirikishwaji.**

**Vilevile, NEMC inapaswa kuandaa mipango madhubuti na inayotekelezeka ya kupunguza athari za miradi yote, kwa mikakati sahihi ya utekelezaji ili kupunguza athari za kimazingira na kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu.**

## 10.4 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira Unaofanywa na NEMC

### 10.4.1 Ufuatiliaji Usioridhisha wa Utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira Uliofanywa na NEMC

Utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira uliofanywa na NEMC unakinzana na Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Tathmini ya Athari za Mazingira na Ukaguzi) (Marekebisho ya mwaka 2018), inayowataka, kila mwaka, wafadhili au waendelezaji wa miradi kufuatia kupitishwa kwa taarifa ya athari za mazingira au ukaguzi wa awali, kuandaa mpango huo, kufanya ukaguzi wa mazingira, na kupeleka NEMC.

Ukaguzi wangu ulibaini NEMC haikufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakiki utekelezaji wa hatua za kupunguza madhara katika miradi minane iliyotembelewa wakati wa ukaguzi, hususani katika kudhibiti taka ngumu na hatarishi. Utunzaji mbaya wa taka ngumu ulionekana kwenye Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Mradi wa Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka – Awamu ya 3, Daraja la John Pombe Magufuli, na Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka, ambapo taka hazikuchambuliwa, kutenganishwa, na kupangwa vizuri kulingana na aina. Aidha, ukaguzi ulibaini umwagikaji wa mafuta katika maeneo manne yaliyotembelewa, ambayo ni Mgodi wa Makaa ya

Mawe Ngaka, Mgodi wa Chokaa wa Dangote, Daraja la John Pombe Magufuli, na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato. Udhaifu huu unaleta hatari za kimazingira na kiafya, ikiwa pamoja na uchafuzi wa udongo, maji, na hewa, na madhara ya muda mrefu kwa mifumo ya ikolojia na jamii zinazoishi karibu na miradi.

Aidha, nilibaini kuwa NEMC haikuthibitisha vipimo vya uchafuzi wa mazingira vinavyofanywa na watekelezaji wa miradi kulingana na mipango ya usimamizi wa mazingira. Mipango hiyo inataka ufuatiliaji wa mara kwa mara wa uzalishaji, ubora wa maji, na uchafuzi wa udongo. Kutothibitisha viwango vya uchafuzi wa mazingira kulizuia kupunguza hatari za mazingira, kama vile uchafuzi wa hewa na maji, unaoweza kuathiri vibaya mazingira na jamii.

Mbali na hilo, nilibaini kuwa NEMC haikufuatilia utekelezaji wa ukaguzi wa mazingira unaohitajika kila mwaka kwa miradi iliyotembelewa wakati wa ukaguzi, hivyo kusababisha kutofuata hatua za mazingira zilizoainishwa katika Taarifa ya athari za mazingira na cheti cha tathmini ya athari za mazingira.

Ushughulikiaji na uhifadhi wa taka hatari usiofaa unaweza kusababisha uharibifu wa mazingira wa muda mrefu, ikiwa pamoja na uchafuzi wa udongo na maji, kuhatarisha mazingira, wanyamapori, na afya ya binadamu, hususani kwa wafanyakazi na jamii za karibu na miradi. Aidha, wakati wa ziara za wakaguzi kutembelea maeneo ya miradi, walibaini ukosefu wa hatua za kudhibiti mmomonyoko wa udongo katika machimbo na mashimo ya udongo katika Mgodi wa Chokaa wa Dangote, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Mgodi wa Makaa ya Mawe Ngaka, Daraja la John Pombe Magufuli, na Mgodi wa Almasi wa Williamson. Udhaifu huu ilisababisha uharibifu wa miamba na mkusanyiko wa juu wa udongo, hivyo kusababisha hatari za mazingira. Maghala ya kuhifadhia vifaa kama taka na mafuta yalikosa mifumo sahihi ya mifereji ili kudhibiti uchafuzi kama vile umwagikaji wa mafuta, hivyo kuongeza hatari za uchafuzi.

**Ninapendekeza NEMC ipange na kutekeleza ukaguzi wa mara kwa mara wa maeneo ili kuhakikisha kuwa mipango ya usimamizi wa mazingira inazingatiwa wakati wa kutekeleza miradi (ufuatiliaji baada ya tathmini ya athari za mazingira).**

## 10.5 Udhibiti na Ufuatiliaji wa Maandalizi, Utekelezaji, na Mipango ya Urudishiaji Maeneo Yaliyoharibiwa

Kifungu cha 102(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kinamtaka mtekelezaji, mwendeshaji, au mmiliki, baada ya kumalizika kwa mradi, kufanya kwa gharama zake mwenyewe, uondoaji salama, ukarabati wa

eneo, na urejeshaji wa mfumo wa ikolojia kabla ya kufungwa kwa mradi au shughuli.

Ukaguzi wangu uligundua kuwa NEMC haikusimamia na kufuatilia ipasavyo uondoaji wa mipango kama inavyothibitishwa na kutokuwapo kwa mipango madhubuti katika miradi ya ujenzi na uchimbaji wa madini iliyotembelewa. Mpango wa kufunga Mgodi wa Almasi wa Williamson ulisalia kuwa wa kizamani, na hakukuwa na miradi ya ujenzi iliyoandaa mipango ya kurudishia maeneo kabla ya kufunga miradi hiyo. Zaidi ya hayo, waendelezaji na wamiliki wa miradi minane iliyotembelewa walishindwa kuwasilisha hati fungani za utekelezaji wa mazingira zinazohitajika. Matokeo yake, kulikuwa na ongezeko la hatari na athari za kutozingatia mienendo bora ya mazingira na kupunguza hatua za athari za mazingira, hasa baada ya kukamilika kwa miradi.

NEMC haikusimamia au kufuatilia uboreshaji na urudishiaji wa maeneo ya ukarabati wa mazingira katika miradi ya madini iliyotembelewa. Katika Mgodi wa Chokaa wa Dangote, upandaji miti uliopangwa haukuwa wa kutosha. Katika Mgodi wa Makaa ya Mawe Ngaka, marundo ya mawe yaliwekwa karibu na mkondo wa maji, hivyo kuongeza hatari ya uchafuzi wa maji katika maeneo asili ya mifereji ya maji. Katika Mgodi wa Dhahabu Buzwagi, uoteshaji wa mimea ulicheleweshwa hadi kufungwa kwa mgodi badala ya kufanywa hatua kwa hatua wakati wa shughuli, kama ilivyopendekezwa katika ripoti ya tathmini ya athari za mazingira. Udhaifu huu huongeza hatari ya uharibifu wa mazingira kwa muda mrefu na unaweza kuacha athari zisizoweza kutatuliwa za mazingira baada ya uchimbaji kukoma.

Hali hii ilitokana na kanuni au usimamizi usiofaa wa ufuatiliaji wa maandalizi na utekelezaji wa tathmini ya athari za mazingira na mipango ya usimamizi wa mazingira, ili kupunguza athari za mazingira zitokanazo na shughuli za ujenzi na uchimbaji wa madini. Hali hii pia ilitokana na usajili duni wa miradi, mapitio yasiyo na tija ya taarifa za athari za mazingira, na ufuatiliaji duni wa mipango ya usimamizi wa mazingira.

**Ninapendekeza NEMC ianzishe na itekeleze utaratibu wa kufuatilia utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya uondoaji na ukarabati au urudishiaji na uendelevu wa mazingira yaliyoharibiwa katika miradi ya sekta ya madini.**




# SURA YA KUMI NA MOJA

## Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Utekelezaji wa Miradi ya Usambazaji Maji Vijijini Chini ya Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini

# UKAGUZI WA KIUFUNDI KWENYE UTEKELEZAJI WA MIRADI YA USAMBAZAJI MAJI VIJIJINI CHINI YA WAKALA WA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

## 11.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi uliolenga kuangalia iwapo Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) inaandaa mipango ya ujenzi, kusanifu miradi, na kutekeleza ujenzi wa miradi ya usambazaji maji vijijini kwa kuzingatia miongozo iliyopo ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa huduma ya maji vijijini.

RUWASA ina jukumu la kupanga, kubuni, kujenga na kusimamia miradi ya usambazaji wa maji vijijini. Ukaguzi wa kiufundi ulilenga kutathmini upangaji wa miradi, ubunifu, ununuzi, usimamizi wa mikataba, pamoja na masuala ya mazingira, usalama, na athari za kijamii wakati wa utekelezaji wa miradi.

Nilichagua sampuli ya miradi mitano ya maji iliyotekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2023/24. Miradi hii ni Mradi wa Usambazaji wa Maji wa Morong'anya uliopo Morogoro, Mradi wa Kemondo – Maruku mkoani Kagera, Mradi wa Igando-Kijombe uliopo Wanging'ombe, Mradi wa Kigwa-Uyui uliopo Tabora, na Mradi wa Igogo-Igurubi uliopo Igunga, Tabora. Gharama za miradi hii zilikuwa Shilingi bilioni 8.08 kwa Miradi wa Kemondo-Maruku, Shilingi bilioni 23.18 kwa Morong'anya, Shilingi bilioni 12.4 kwa Igando-Kijombe, Shilingi bilioni 20.43 kwa Igogo – Igurubi, na Shilingi bilioni 11.93 kwa Mradi wa Kigwa – Uyui.

## 11.2 Mipango na Usanifu wa Miradi

### 11.2.1 Utafiti usiojitosheleza katika kubainisha vyanzo vya maji

Nilibaini kuwa uwezo wa kuzalisha maji katika vyanzo vilivyopendekezwa katika miradi niliyokagua ulipimwa mara moja tu, hivyo kusababisha timu ya usanifu kutokuwa na uwezo wa kubaini mabadiliko wa kiwango cha maji na ubora wa maji kwenye vyanzo hivyo kwa misimu tofauti, kama inavyoelekezwa katika kifungu 1.1.4.1 cha Mwongozo wa Usanifu wa Miradi ya Maji wa Wizara ya Maji wa Mwaka 2009. Upungufu huu ulitokana na kutofanyika kwa upembuzi yakinifu ambao ungewezesha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kuchambua vipengele vyote vya mradi ili kujiridhisha utoshelevu wake.

Pia, nilibaini kuwa kutokana na kushindwa kufanyika kwa uchunguzi unaojitosheleza wa ubora wa maji kutoka katika vyanzo vilivyochaguliwa, mifumo ya kutibu maji isiyojitosheleza iliwekwa katika miradi miwili kati ya mitano niliyokagua. Miradi hiyo ni Morong'anya na Kemondo-Maruku, ambapo

iliwekwa mifumo ya klorini (mfumo wa kuua wadudu). Mifumo hiyo haikuwa na uwezo wa kuondoa kemikali na kuchuja uchafu kutoka katika maji, hivyo kuhatarisha afya ya watumiaji ikizingatiwa kuwa vyanzo hivyo ni mito na maziwa, ambapo maji yanaweza kuchafuka kutokana na kutiririshwa kwenye vyanzo wakati wa mvua na shughuli za binadamu.

Aidha, nilibaini kuwa miradi miwili ya Kigwa-Uyui na Igogo-Igurubi ilichukua maji kutoka bomba la Mamlka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga (KASHWASA) (kama chanzo) licha ya kuwa usanifu wa bomba la mamlaka hii haukujumuisha mahitaji ya maji ya miradi hii miwili. Hatua hii ilihatarisha uwezo wa chanzo hicho kuzalisha maji yanayohitajika kwa kipindi cha miaka 20 iliyokusudiwa. Pia, mradi mmoja wa Igando-Kijombe ulichukuwa maji kutoka mto ambao hukumbwa na upungufu wa maji wakati wa kiangazi kutokana na shughuli za kilimo zinazofanywa na wananchi juu ya chanzo, jambo ambalo lilihatarisha pia uwezo wa chanzo hicho.

**Ninapendekeza RUWASA afanye upembuzi yakinifu kabla ya kuanza ujenzi wa miradi ili kuhakikisha kuwa uwezo wa vyanzo na ubora wa maji kutoka katika vyanzo vitakavyotumika unabainishwa kikamilifu; Pia ahakikishe kuwa mifumo stahiki ya kutibu maji inawekwa kwenye miradi iliyojengwa bila ya mifumo hiyo.**

### 11.2.2 Uchaguzi wa Mipango Hafifu ya Msingi na Usanifu kwa Ajili ya Makadirio ya Mahitaji ya Maji

Kifungu cha 1.14.3 cha Mwongozo wa Usanifu wa Miradi ya Maji wa Wizara ya Maji wa Mwaka 2009 kinataka mradi ufanyiwe usanifu wa kutoa huduma kwa muda mfupi wa miaka mitano, muda wa kati wa miaka kumi, na muda mrefu wa miaka 20.

Nilibaini kuwa miradi yote mitano niliyoikagua ilifanyiwa usanifu wa kuweza kuzalisha maji yatakayokidhi mahitaji ya miaka 20 ijayo. Hata hivyo, timu ya usanifu haikuhakikisha kuwa miaka 20 iliyokusudiwa inaanza kuhesabiwa mwaka ambao ujenzi wa mradi utakuwa umekamilika. Hivyo, muda wa ujenzi wa mradi ulijumuisihwa ndani ya miaka 20 ya utoaji huduma. **Jedwali Na. 36** linaonesha muda wa usanifu wa miradi na miaka ya kuanzia.

**Jedwali Na. 36: Muda wa usanifu wa miradi na miaka ya kuanzia**

| Jina la Mradi | Mwaka wa Usanifu | Mwaka wa Kuanza Huduma | Hali ya Ujenzi wa Mradi (Oktoba 2024) | Miaka Iliyopita bila Mradi Kutumika | Muda Uliobaki kati ya Miaka 20 ya Huduma |
|---|---|---|---|---|---|
| Morong'anya | 2020 | 2021 | Haujakamilika | 4 | 16 |
| Igando - Kijombe | 2017 | 2019 | Haujakamilika | 6 | 14 |
| Igogo - Igurubi | 2021 | 2022 | Haujakamilika | 3 | 17 |
| Kemondo - Maruku | 2020 | 2020 | Haujakamilika | 5 | 15 |
| Kigwa Uyui | 2021 | 2022 | Haujakamilika | 3 | 17 |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi wa taarifa za usanifu wa miradi iliyokaguliwa mwaka 2024*

Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi wangu mwezi Oktoba 2024, miradi hiyo ilikuwa haijakamilika, hivyo kusababisha miaka ya kutoa huduma kabla ya kufikia uwezo wake wa juu kupungua kutoka miaka 20 hadi 17 kwa Miradi ya Kigwa-Uyui na Igogo-Igurubi; miaka 16 kwa Mradi wa Moronganya; miaka 15 kwa Mradi wa Kemondo-Maruku; na miaka 14 kwa Mradi wa Igando-Kijombe.

Hali hii ilisababishwa na kukosekana kwa mipango toshelevu ya utekelezaji wa miradi, ambayo ingebainisha muda halisi utakaotumika kwa ajili ya ujenzi, hivyo kutojumuishwa ndani na miaka 20 ya usanifu wa mradi.

**Ninapendekeza RUWASA ahakikishe kuwa muda halisi utakaotumika katika utekelezaji wa mradi haujumuishwi ndani ya muda wa usanifu wa mradi ili kutopunguza muda wa huduma uliokusudiwa.**

## 11.3 Menejimenti ya Ununuzi

### 11.3.1 Kutofanya Uhakiki wa Uwezo wa Mkandarasi Kabla ya Kumpa Kazi

Kanuni ya 124 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi za umma kufanya uhakiki wa taarifa zilizowasilishwa na wazabuni ili kujiridhisha kuhusu uwezo wa mzabuni husika kabla ya kumpa kazi.

Hata hivyo, nilibaini kuwa katika mikataba 14 kati ya 15 iliyosainiwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitano niliyoikagua, wakandarasi husika walipewa kazi bila ya kufanya uhakiki wa taarifa walizowasilisha wakati wa mchakato wa zabuni ili kujiridhisha kuhusu uwezo wao wa kutekeleza mradi. Hali hii

ilisababisha kuwapa kazi wakandarasi wasiokuwa na uwezo wa kutekeleza kwa wakati miradi hiyo, hivyo kusababisha ucheleweshaji wa miradi kwa kati ya miezi sita hadi miaka mitano.

Pia, kutokana na kutokuwa na uwezo unaojitosheleza, wakandarasi wanne walishindwa kufanya kazi, hivyo kusitishiwa mikataba yao. Hata hivyo, baada ya kusitisha mikataba hiyo, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini uliingia gharama za ziada za kiasi cha Shilingi bilioni 1.17 kwa ajili ya kumalizia kazi zilizoachwa na wakandarasi walioshindwa kazi. Gharama hizi zingeweza kuepukwa kama uwezo wa wakandarasi ungehakikiwa kabla ili kupata wakandarasi wenye uwezo. **Jedwali Na. 37** linaonesha mchanganuo wa gharama za ziada zilizotumika.

**Jedwali Na. 37: Gharama za ziada zilizotumika kukamilisha miradi baada ya kusitisha mikataba**

| Jina la mradi | Mkataba Uliositishwa | Gharama za Ziada Zilizotumika (Sh.) |
|---|---|---|
| Kigwa-Uyui | AE-102/2020-2021/TBR/W/03 | 296,374,100 |
| | AE-102/2020-2021/TBR/W/22 | 650,467,920 |
| Kemondo-Maruku | AE-031/2020-21/W/78 | 226,561,593 |
| | AE-102/2022-2023/KGR/W/19 Lot 01 | Hakuna[4] |
| **Jumla** | | **1,173,403,613** |

***Chanzo***: *Uchambuzi wa mkaguzi wa nukuu za mahitaji ya kazi na bei kwa mikataba iliyositishwa mwaka 2024*

Gharama hizo za ziada zilitokana na utofauti kati ya gharama zilizotumika kukamilisha kazi iliyobaki na gharama ambazo kazi hiyo ingefanywa na mkandarasi aliyesitishiwa mkataba.

Kutokufanyika kwa uhakiki wa uwezo wa wakandarasi kulitokana na usimamizi hafifu ndani ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kuhusu mchakato wa ununuzi. Hapakuwa na utaratibu wa kufuatilia michakato ya ununuzi ndani ya taasisi ili kuhakikisha taratibu zote za ununuzi zinafuatwa, ikiwemo Mwongozo wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kuhusu kuingiza mikataba ya ununuzi, ambao ulibainisha kuwa kabla ya kusaini mkataba na mzabuni lazima uhakiki ufanyike.

**Ninapendekeza RUWASA aimarishe utaratibu wa ndani wa usimamizi wa shughuli za ununuzi ili kuhakikisha kuwa taratibu za ununuzi zinafuatwa ikiwemo kufanya uhakiki wa uwezo wa wazabuni.**

[4] Wakati wa ukaguzi, kazi zilizobaki baada ya kusitisha mkataba zilikuwa hazijafanyika.

### 11.3.2 Kukubali Zabuni Zisizokidhi Matakwa ya Zabuni

Kanuni za 205(b) na 206(2) za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2023 zinaeleza kwamba zabuni zote zinazowasilishwa na wazabuni lazima zihakikiwe ili kuona iwapo zimefuata matakwa ya zabuni husika na ambazo zitakuwa kinyume na matakwa za zabuni husika zikataliwe.

Mapitio niliyoyafanya kwenye zabuni iliyotunukiwa ushindi kwa Mradi wa Morong'anya yalibaini kuwa haikujumuisha gharama za ujenzi wa matanki ya maji licha ya kuwa yalikuwa moja ya hitaji la zabuni hiyo. Zabuni hiyo ilipendekezwa kupewa ushindi kwa matarajio kwamba upungufu huo ungezungumzwa wakati wa kikao cha maelewano na mzabuni. Hata hivyo, upungufu huo haukujadiliwa wakati wa kikao hicho, hivyo kusababisha mkataba kusainiwa ukiwa na upungufu. Gharama za ujenzi wa matanki hayo zilikuja kujumuishwa kwenye mkataba kama kazi za nyongeza wakati wa utekelezaji wa mradi kwa kiasi cha Shilingi bilioni 1.26, ambapo mkandarasi aliruhusiwa kuwasilisha makadirio hayo kinyume na taratibu za ununuzi. Upungufu huu uliathiri uwezekano wa kudhibiti gharama za mradi kwa sababu gharama zilizowasilishwa na mkandarasi kabla na baada ya kusaini mkataba zilikuwa tofauti. Gharama za baada ya kusaini mkataba zinaweza kuwa kubwa kwa kuwa mkandarasi anajua kuwa ameshakabidhiwa kazi na hakuna tena ushindani.

Upungufu kama huo niliubaini pia katika zabuni Na. AE/102/2022-2023/TBR/W/13 ya Mradi wa Kigwa-Uyui, ambapo zabuni haikujumuisha gharama za ununuzi ya mabomba ya kusambazia maji. Licha ya upungufu huo, mzabuni alipendekezwa kupewa kazi hiyo. Hata hivyo, mzabuni hakupewa kazi baada ya mzabuni mwingine kwenda kukata rufaa kwenye Mamlaka ya Rufaa ya Ununuzi ya Umma, ambapo kupitia rufaa Na. PPAA/APPEAL/01/12/2023-24 ilibanisha kuwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini walifanya makosa na kuamuru mzabuni mwingine apewe kazi hiyo.

Aidha, kukubaliwa kwa zabuni zenye upungufu kulitokana na kuundwa kwa timu ya tathmini ya zabuni isiyokidhi matakwa ya mwongozo wa tathmini wa zabuni wa mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma wa mwaka 2020, ambao unabainisha kuwa timu ya tathmini ya zabuni ijumuishe mtaalamu wa kiufundi (mhandisi), mchumi na mtaalamu wa fedha. Hata hivyo timu ya kufanya tathmini iliundwa na wahandisi tuu.

**Ninapendekeza RUWASA ahakikishe kuwa mchakato wa ununuzi unafanyika kikamilifu kwa kufuata taratibu ili kuhakikisha matumizi bora ya fedha za umma.**

## 11.4 Usimamizi wa Mikataba

### 11.4.1 Utaratibu Usiofaa wa Usitishaji wa Mikataba ya Wakandarasi Uliosababisha Upotevu wa shilingi Milioni 493.08

Kwa mujibu wa Kifungu cha 69 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba, mkandarsi kushindwa kutakeleza kazi ni uvunjaji wa mikataba.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mikataba minne kati ya 15 iliyosainiwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitano niliyokagua ilisitishwa kutokana na wakandarasi husika kushindwa kutekeleza miradi. Licha ya makosa hayo ya wakandarasi, RUWASA alisitisha mikataba hiyo kwa maridhiano bila ya kuchukulia kuwa wakandarasi wamekiuka vipengele vya kimkataba. Aidha, kifungu ambacho kiliutaka Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kukata kiasi cha fedha kilichobainishwa kwenye mikataba hiyo hakikutumika, hivyo kusababisha upotevu wa kiasi cha Shilingi milioni 493.08. **Jedwali Na. 38** linaonesha mikataba iliyositishwa na kiwango cha fedha kilichotakiwa kukatwa kama fidia.

**Jedwali Na. 38: Mikataba iliyositishwa na kiwango cha fedha kilichotakiwa kukatwa kama fidia**

| Jina la Mradi | Mikataba Iliyositishwa | Kiasi cha Mkataba (Sh.) | Gharama za Kazi Kilizobakia (Sh.) | Asilimia ya Iliyotakiwa Kukatwa | Kiasi Kilichotakiwa Kukatwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| Kemondo-Maruku | AE-031/2020-21/W/78 | 145,176,816 | 67,931,007 | 5 | 7,258,841 |
| | AE-102/2022-2023/KGR/W/19 Lot 1 | 1,576,261,700 | 1,535,041,527 | 20 | 307,008,305 |
| Kigwa-Uyui | AE-102/2020-2021/TBR/W/03 | 540,851,377 | 329,632,557 | 15 | 49,444,884 |
| | AE-102/2020-2021/TBR/W/22 | 1,452,520,587 | 1,293,760,083 | 10 | 129,376,008 |
| **Jumla** | | | | | **493,088,038** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi wa mikataba iliyositishwa*

**Jedwali Na. 38** linaonesha kuwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini haukutumia mamlaka ya kimkataba uliyokuwa nayo kukata kiasi cha shilingi milioni 493.08 kutoka katika mikataba iliyositishwa ili kupunguza mzigo wa kiasi cha Shilingi bilioni 1.17, ambao ni gharama za ziada, ambazo zilitumika kumalizia kazi zilizoachwa na wakandarasi waliositishiwa mikataba yao.

Kutozingatiwa kwa vifungu vya kimkataba wakati wa usitishaji wa mikataba ya wakandarasi kulitokana na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kushindwa kufanya tathmini ya sababu zilizotolewa na wakandarasi kabla ya kukubali ombi lao la kisitisha mikataba.

**Ninapendekeza RUWASA, wakati wa kusitisha mikataba ya wakandarasi kutokana na kushindwa kufanya kazi, ahakikishe anatumia vifungu vya kimkataba vinavyotaka mkandarasi kukatwa kiasi cha fedha kwa ajili ya kufidia gharama za ziada zitakazotumika kumalizia kazi zilizobaki.**

### 11.4.2 Ongezeko la Gharama za Shilingi Bilioni 4.03 Kutokana na Usanifu Hafifu

Kifungu cha 2.1 cha Mwongozo wa Usanifu Wa Miradi ya Maji wa Wizara ya Maji wa Mwaka 2020 kinaelekeza kuwa kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi wowote wa maji ni muhimu kuandaa mipango ya utekelezaji ikiwa pamoja na kufanya usanifu wa mradi.

Nilibaini kuwa miradi yote mitano niliyokagua ilikuwa na ongezeko la gharama kutokana na mabadiliko ya usanifu wakati wa ujenzi kwa kuwa usanifu haukuakisi hali halisi ya mahitaji ya mradi. Mbadiliko hayo yalisababisha ongezeko la gharama ya kiasi cha Shilingi bilioni 6.88, ambapo hadi wakati wa ukaguzi wangu, mabadiliko ya gharama za kiasi cha Shilingi bilioni 4.038 yalikuwa yameidhinishwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. **Jedwali Na. 39** linaonesha mchanganuo wa ongezeko la gharama katika miradi.

**Jedwali Na. 39: Mchanganuo wa ongezeko la gharama katika miradi**

| Jina la Mradi | Kazi Zilizoongezeka | Gharama za Mradi (Sh.) | Ongezeko la Gharama (Sh.) | Asilimia ya Ongezeko |
|---|---|---|---|---|
| Morong'anya | Ujenzi wa chanzo, mabomba ya kusambaza maji, na matanki ya maji | 23,186,021,991 | 2,540,789,104 | 10.9 |
| Igando-Kijombe | Marekebisho kwenye chanzo, na ujenzi wa uzio na ofisi ya waendeshaji wa mradi | 12,437,407,360 | 1,368,260,600 | 11 |
| Kemondo-Maruku | Kazi za nyongeza kwenye ujenzi wa tanki la ujazo wa 3000m$^3$ | 8,088,405,067 | 129,398,800 | 1.5 |
| **Jumla ya Kazi Zilizoidhinishwa** | | | **4,038,448,504** | |
| Igogo-Igurubi | Ujenzi wa pampu ya kusukuma maji | **20,438,622,361** | **2,845,865,197** | **13.9** |

| Jina la Mradi | Kazi Zilizoongezeka | Gharama za Mradi (Sh.) | Ongezeko la Gharama (Sh.) | Asilimia ya Ongezeko |
|---|---|---|---|---|
| | (gharama hazijaidhinishwa) | | | |
| **Jumla ya Mabadiliko** | | | **6,884,313,701** | |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi wa mabadiliko ya kazi za ujenzi mwaka 2024*

**Jedwali Na. 39** linaonesha kuwa jumla ya ongezeko la kazi zenye gharama ya shilingi bilioni 6.88 lilitokea, ambapo kati ya mabadiliko hayo, kazi zenye gharama ya Shilingi bilioni 4.038 zilikuwa zimeidhinishwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Mabadiliko haya yalitokana na kuongezeka kwa kazi wakati wa ujenzi kutokana na kwamba usanifu uliofanywa haukujitosheleza.

Gharama hizi zingewezwa kupunguzwa au kuepukwa iwapo usanifu wa miradi ungefanywa kikamilifu kwa kuhakikisha kuwa mahitaji yote ya miradi yanajumuishwa. Mabadiliko wakati wa utekelezaji wa miradi unatoa nafasi kwa wakandarasi kuleta gharama zisizo na uhalisia kwa sababu wanajua kuwa hakuna ushindani hivyo huweza kuathiri udhibiti wa gharama za miradi.

**Ninapendekeza RUWASA afanye usanifu wa miradi kwa kina kabla ya kuanza ujenzi ili kupunguza mabadiliko na gharama zisizotarajiwa wakati wa ujenzi.**

### 11.4.3 Madai ya Riba Shilingi Milioni 711.79 Yaliyotokana na Ucheleweshaji wa Malipo ya Wakandarasi

Kifungu 53 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba kinataka wakandarasi kulipwa ndani ya siku 28 tangu malipo yao yatakapoidhinishwa na meneja wa mradi. Pia Kifungu cha 53.1 kinaelekeza kwamba, mwajiri anapaswa kulipa fidia pindi atakapomcheleweshea mkandarasi malipo.

Nilibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi kwa muda wa kati ya siku 66 na 331. Ucheleweshaji mkubwa ulionekana kwenye Mradi wa Morong'anya, ambapo ucheleweshaji ulikuwa kwa siku 257 kwa hati ya malipo namba tatu na siku 331 kwa hati ya malipo namba nne.

Mkandarasi aliwasilisha madai ya kiasi cha shilingi milioni 711 kama fidia ya kucheleweshewa maliyo kwa Mradi wa Morong'anya. Hadi kipindi cha ukaguzi (mwezi Oktoba 2024), madai hayo yalikuwa yakifanyiwa tathmini na meneja wa mradi. Kucheleweshwa kwa malipo ya wakandarasi kulitokana na kuchelewa fedha za utekelezaji wa mradi kutoka Wizara ya Fedha.

**Ninapendekeza RUWASA ashirikiane na Wizara ya Maji na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha malipo ya wakandarasi yanafanyika kwa wakati ili kuepuka kulipa fidia.**

### 11.4.4 Usimamizi Usioridhisha wa Ubora wa Kazi za Ujenzi

Jedwali Na. 4.41 kwenye Mwongozo wa Usanifu wa Miradi ya Maji wa Wizara ya Maji wa Mwaka 2009 linabainisha kuwa mabomba ya kusambaza maji (HDPE) yanatakiwa kufukiwa na udongo usio na mawe na kwa kushindiliwa kikamilifu kwa asilimia 80 ya uwezo wa udongo kushindiliwa.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwapo kwa upungufu katika utandazaji wa mabomba ya kusambaza maji, ambapo wakandarasi walitumia udongo wenye mawe kufukia mabomba kinyume na mwongozo wa usanifu wa miradi ya maji. Pia, ufukiaji wa mabomba ulifanywa bila kushindilia udongo, hivyo kusababisha hatari ya kulegea kwa viungio na kutoboka kwa mabomba.

Utandazaji wa mabomba usiojitosheleza ulitokana na kutoandaliwa kwa viwango vya utandazaji wa mabomba na kujumuishwa kwenye mikataba ya wakandarasi ili waweze kuizingatia wakati wa ujenzi.
Athari ya mawe kwenye mabomba yaliyofukiwa chini ni kwamba wakati maji yatakapopita kwenye bomba, yatasababisha msuguano baina ya bomba na jiwe, hivyo kusababisha mabomba kuanza kutoboka na kuvuja na kuadhiri uendelevu wa mradi wa maji.

**Ninapendekeza RUWASA ahakikishe kuwa viwango vya utandazaji wa mabomba vinaandaliwa na kujumuishwa kwenye mikataba ya wakandarasi na kuhakikisha kuwa vinafuatwa kikamilifu.**



# SURA YA KUMI NA MBILI

## Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Majitaka Maeneo ya Mijini

# UKAGUZI WA KIUFUNDI KWENYE UJENZI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU YA MAJITAKA MAENEO YA MIJINI

## 12.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi huu uliolenga kuangalia iwapo Wizara ya Maji na mamlaka za usambazaji maji safi na usafi wa mazingira zinasimamia kikamilifu ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya majitaka kwa kuzingatia muda, gharama, na ubora ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Taasisi zilizokaguliwa zilikuwa Wizara ya Maji na mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira. Taasisi hizi zina wajibu wa kujenga, kukarabati, na kuendesha miundombinu ya majitaka katika maeneo ya mijini. Ukaguzi ulichagua miradi iliyokuwa inatekelezwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2010/11 hadi 2023/2024. Miradi hiyo ilikuwa Upanuzi wa Bwawa la Majitaka Ilemela uliokuwa unatekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA); ujenzi wa miundombinu ya majitaka kwa ajili ya Manispaa ya Musoma uliokuwa unatekelezwa na Wizara ya Maji; ujenzi wa miundombinu ya kuchakata majitaka Mbezi Beach uliokuwa unatekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA); ukarabati wa miundombinu ya majitaka Area C na D Dodoma uliokuwa unatekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA); na ujenzi wa miundombinu ya majitaka Babati uliokuwa unatekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati Mjini (BAWASA).

## 12.2 Mipango na Usanifu wa Miradi

### 12.2.1 Kuzidi kwa Kiwango cha Kemikali ya Oksijeni kwenye Majitaka Yatakayozalishwa kwenye Mtambo wa Kutibu Majitaka wa Mbezi Beach

Kwa mujibu wa viwango vya Shirika la Viwango Tanzania (TBS 860:2005), maji yatakayozalishwa kutokana na majitaka yanatakiwa kuwa na kiwango cha uhitaji wa hewa ya oksijeni kisichozidi miligramu 60 kwa lita. Aidha, Kanuni ya 8(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Viwango vya Ubora wa Maji) ya Mwaka 2007 inahitaji kwamba viwango vinavyoruhusiwa vya maji taka ya Manispaa na viwandani viwe 60mg/l.

Kupitia taarifa za zabuni za mradi wa majitaka Mbezi Beach, nilibaini kuwa DAWASA iliandaa mahitaji ya mradi yaliyobainisha kuwa kiwango cha uhitaji wa hewa ya oksjeni kiwe miligramu 125 kwa lita, ambacho ni zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Hali hii ilisababisha

usanifu wa mradi kufanyika kwa kutumia hitaji hilo, ambalo ni miligramu 125 kwa lita.

Kiwango cha juu cha uhitaji wa hewa ya oksijeni katika miundombinu ya matibabu ya majitaka iliyojengwa Mbezi Beach kilisababishwa na kushindwa kwa DAWASA kuzingatia viwango vya ndani vilivyobainishwa na TBS wakati wa kuandaa mahitaji ya mradi.

Matokeo ya kumwaga maji taka yenye kiwango cha uhitaji wa hewa ya oksijeni kinachozidi kiwango kinachoruhusiwa kwa 65mg/L yatasababisha uchafuzi wa maji katika vyanzo vya maji vinavyopokea majitaka hayo, ambapo viwango vya uhitaji wa hewa ya oksijeni vitazidi mipaka inayoruhusiwa kwa 108.33%.

**Ninapendekeza DAWASA ihakikishe kuwa usanifu na utekelezaji wa miradi ya majitaka unazingatia viwango vya nchi ili kuhakikisha maji yanayotokana na majitaka hayana athari kwa mazingira.**

### 12.2.2 Kuongezeka kwa Gharama ya Shilingi Bilioni 1.66 za Mradi Kutokana na Kutojumuishwa kwa Wateja Wasiounganishwa

Aya ya 2.2.2 ya Mwongozo wa Usanifu wa Miradi ya Majitaka wa Wizara ya Maji wa Mwaka 2020 unataka kufanya uchambuzi wa hali halisi kabla ya kuanzisha mradi ikiwemo kutambua uhitaji wa huduma ya miundombinu ya majitaka.

Taarifa ya usanifu wa Mradi wa Majitaka wa Area C na D Jijini Dodoma ya mwaka 2018 ilionesha kuwa si nyumba zote zilizokuwa katika eneo la mradi zilikuwa zimeunganishwa kwenye mfumo wa majitaka uliokuwa unafanyiwa ukarabati.

Nilibaini kuwa usanifu wa mradi huo haukujumuisha kuwapo kwa nyumba hizo zisizounganishwa kwenye mifumo ya majitaka. Pia, haukujumuisha ongezeko la makazi ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na matoleo kwenye mradi kwa ajili ya kuhudumia nyumba zitakazoongezeka.

Kutokana na upungufu huo, wakati wa utekelezaji wa mradi kulikuwa na ongezeko la gharama kiasi cha Shilingi bilioni 1.66 kwa ajili ya kuweka miundombinu ya kuhudumia nyumba ambazo hazikujumuishwa kwenye usanifu wa awali. Wakati wa ukaguzi gharama hizo zilikuwa zimeidhinishwa na watekelezaji wa mradi ambao ni DUWASA huku ikisubiriwa idhini ya Wizara ya Maji.

Pia, kutojumuisha ongezeko la nyumba katika usanifu wa miundombinu hiyo kunahatarisha miundombinu iliyojengwa ya majitaka kuzidiwa uwezo kutokana

na ongezeko la watumiaji, ambao hawakujumuishwa kwenye usanifu wa awali. Hali hii ilitokana na upembuzi yakinifu hafifu ambao ungeweza kubainisha mahitaji halisi ya mradi kama ungefanyika kwa usahihi.

**Ninapendekeza DUWASA ifanye upembuzi yakinifu unaojitosheleza kwenye mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka Area C na D ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya huduma ya miundombinu ya majitaka yanajumuishwa kwenye mradi.**

## 12.3 Usimamizi wa Mikataba

### 12.3.1 Malipo ya Shilingi Bilioni 1.60 Kulipwa kwa Kazi Ambazo Hazikufanyika

Kifungu cha 12.2 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2022 yanabainisha kuwa malipo yafanyike kuendana na kazi iliyofanyika.

Nilibaini upungufu katika uandaaji wa hati za malipo katika miradi miwili ambayo ni ujenzi wa miundombinu ya majitaka Babati na ujenzi wa miundombinu ya majitaka Ilemela ambayo yalisababisha kuidhinishwa kwa kazi zenye gharama ya Shilingi bilioni 1.60 zilizokuwa hazijafanyika kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 40**.

**Jedwali Na. 40: Malipo yaliyolipwa kwa kazi ambazo hazikufanywa**

| Jina la Mradi | Mchanganuo wa Kazi ambazo Hazikuwa Zimefanyika | Kiasi Kilichoidhinishwa (Sh.) |
|---|---|---|
| Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka Babati | Uwekaji wa mkeka wa milimita 1.5 wa kuzuia maji kuingia ardhini wenye ukubwa wa mita za mraba 20,369 | 365,55 |
| | Zege lenye wavuwaya $m^3$ 118 | 106.290 |
| | Ujenzi wa kutumia mawe -$m^3$ 510 | 229.500 |
| | Njia za kutembea - $m^2$ 1416 | 10.620 |
| | Zege lenye wavuwaya- $m^2$ 965 | 868.500 |
| **Jumla kwa Mradi wa Babati** | | **1,580.370** |
| Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka Ilemela | Malipo yaliyozidishwa kwa mkandarasi msaidizi | 12.906 |
| | Malipo yaliyozidishwa kwenye zege la chini | 4.789 |
| | Malipo ya nondo ambazo hazikuwa zimebainishwa kwenye mchoro | 8.042 |
| **Jumla kwa Mradi wa Mwanza** | | **3,186.567** |
| **Jumla ya Malipo Yaliyozidishwa** | | **1,606.11** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi kwa hati za malipo ya wakandarasi mwaka 2024*

**Jedwali Na. 40** linaonesha kuwa malipo ya kiasi cha shilingi bilioni 1.60 yaliidhinishwa katika miradi miwili ya Ilemela na Babati kwa kazi ambazo hazikuwa zimefanyika. Hadi kufikia mwezi Novemba 2024, malipo hayo kwa upande wa Ilemela yalikuwa yamelipwa ilhali kwa upande wa Babati yalikuwa yameidhinishwa yakisubiri kulipwa.

Malipo ya kazi ambazo hazikuwa zimefanyika yalitokana na kutokufanyika kikamilifu kwa vipimo vya kazi iliyofanywa na mkandarasi kabla ya kuidhinisha malipo ili kuhakikisha kuwa malipo yanafanyika kulingana na kazi iliyofanyika.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji, BAWASA na MWAUWASA zitekeleze mchakato wa marejeo ya upimaji kwa kina kabla ya kuthibitisha malipo ili kuhakikisha kuwa uthibitisho unategemea tu kazi halisi zilizokamilika na kukata kiasi chote kilicholipwa zaidi.**

### 12.3.2 Riba ya Shilingi Milioni 273 Iliyolipwa kwa Mkandarasi Kutokana na Kucheleweshewa Malipo ya Kazi

Kifungu cha 14.7 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba kinamtaka mwajiri kumlipa mkandarasi madai yaliyobainishwa kwenye hati ya malipo ndani ya siku 56 tangu meneja wa mradi atakapokuwa amepokea madai hayo ya malipo.

Nilibaini kuwa katika miradi yote mitano niliyoikagua kulikuwa na ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi kwa kati ya siku 21 hadi 252. Miradi miwili ambayo ni Mradi wa Majitaka Babati na Maradi wa Majitaka Area C na D Dodoma, ilikuwa na ucheleweshaji mkubwa wa malipo ya mkandarasi kwa wastani wa siku 252 na siku 161 mtawalia. Kwa kiwango kikubwa, ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi ulisababishwa na ucheleweshaji wa fedha za miradi kutoka Wizara ya Fedha.

Pia, nilibaini kuwa, kucheleweshwa kwa malipo ya wakandarasi kuliathiri uwezo wa kufikia kwa wakati malengo ya miradi, pia kulisababisha gharama za ziada kiasi cha shilingi milioni 273 zilizolipwa na Wizara kwa mkandarasi wa Mradi wa Majitaka Musoma kama fidia ya kuchelewesha malipo ya awali na malipo ya hati namba mbili kwa siku 110 na 68 mtawalia.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, ihakikishe malipo kwa wakandarasi yanafanyika kwa wakati ili kuepuka gharama za fidia.**



# SURA YA KUMI NA TATU

## Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda

# UKAGUZI WA KIUFUNDI KWENYE MRADI WA UJENZI WA BWAWA LA KIDUNDA

## 13.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi uliolenga kuangalia iwapo Mamlaka ya wa Maji Safi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) imendaa kikamilifu mipango, usanifu, na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mkaguliwa mkuu ilikuwa Mamlaka ya wa Maji Safi na Majitaka Dar es Salaam chini ya Wizara ya Maji kwa sababu ndiyo ilitekeleza mradi huu uliokuwa na thamani ya shilingi bilioni 329.466. Wakati wa ukaguzi, ujenzi wa mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 21. Ujenzi ulianza tarehe 18 Juni 2023 na untarajiwa kukamilika tarehe 17 Juni 2026.

## 13.2 Mipango na Usanifu wa Miradi

### 13.2.1 Kukosekana kwa Bwawa Dogo kwa Ajili ya Kudhibiti Uchafu Kwenye Bwawa Kuu

Aya ya 2.3 ya Mwongozo wa Wizara ya Maji wa Usalama wa Mabwawa wa Mwaka 2020 unataka usanifu wa mabwawa kujumuisha kuwapo kwa taarifa zote zitakazowezesha usanifu kamili wa miundombinu iliyokusudiwa.

Mapitio niliyofanya kwenye usanifu na michoro ya Bwawa la Kidunda yalibaini kuwa usanifu haukujumuisha mahitaji ya bwawa dogo kwa ajili ya kudhibiti uchafu unaoletwa na maji yanayoingia kwenye bwawa kuu wakati wa uendeshaji. Upungufu huu ulitokana na kutofanyika kwa uchambuzi wa kina kabla ya usanifu hivyo kutogusia umuhimu wa kuwa na bwawa dogo kwa ajili ya kudhibiti uchafu.

Kutokana na kutokuwapo kwa bwawa dogo la kudhibiti uchafu unaiongia kwenye bwawa kuu, hakukuwa na uwezekano wa kuzuia uchafu kuingia katika Bwawa la Kidunda, jambo linaloweza kupunguza uwezo wa bwawa pindi uchafu utakapokuwa mwingi.

**Ninapendekeza DAWASA itengeneze mpango-mkakati wa namna ya kudhibiti uchafu kutoingia kwenye bwawa na kutoathiri utendaji, hii itasaidia kudhibiti mkusanyiko wa matope kwenye hifadhi ya maji, kuboresha ufanisi na bwawa kudumu kwa muda mrefu.**

## 13.3 Usimamizi wa Mkataba

### 13.3.1 Uwezekano wa Kusababisha Madai ya Riba Kutokana na Kuchelewesha Malipo ya Mkandarasi

Kifungu cha 14.7(a) cha Masharti ya Jumla ya Mikataba kinamtaka mwajiri kumlipa mkandarasi ndani ya siku 56 kuanzia siku ambayo mkandarasi atawasilisha madai yake.

Nilibaini kuwapo kwa ucheleweshaji wa malipo ya mkandarasi wa kati ya siku 16 hadi 299 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 41**.

**Jedwali Na. 41: Ucheleweshaji wa malipo kwa mkandarasi na mshauri elekezi**

| Nambari ya Hati ya Malipo | Kiasi (Sh.) | Tarehe ya mwisho ya malipo | Tarehe malipo yalipofanyika | Ucheleweshaji (siku) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 8,300,000,000 | 05/01/2024 | 06/06/2024 - | 153 |
| | 1,036,032,177 | 05/01/2024 | Haijalipwa | 299 |
| 2 | 16,791,127,802 | 27/04/2024 | Haijalipwa | 186 |
| 3 | 8,452,471,729 | 26/07/2024 | Haijalipwa | 96 |
| 4 | 6,670,760,425 | 14/10/2024 | Haijalipwa | 16 |
| Jumla | **90,670,414,368** | | | |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi katika taarifa za malipo ya mkandarasi mwaka 2024*

**Jedwali Na 41** linaonesha malipo ya kuchelewa kwa wakandarasi kati ya siku 16 hadi 299. Kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi ilikuwa siku 16 kwa Hati ya Madai Na. 4 na siku 299 kwa Hati ya Madai Na. 1.

Mahojiano yangu na maafisa wa DAWASA yalionesha kuwa kuchelewa kwa malipo kuliwasababishwa na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kutoka Hazina. Licha ya mawasiliano kadhaa kati ya DAWASA na Wizara ya Maji, kuchelewa kulikendelea. Kuchelewa kulipwa kwa Hati za Madai ya Mkandarasi kutapelekea kuongezeka kwa riba, na hatimaye kusababisha gharama zaidi.

**Ninapendekeza DAWASA ishirikiane na Wizara ya Maji na Wizara ya Fedha kuhakikisha utoaji wa fedha kwa wakati. Aidha, mipango madhubuti ya ufuatiliaji wa kifedha inapaswa kutekelezwa ili kuepuka ucheleweshaji wa malipo, kupunguza kuongezeka kwa riba, na kuepuka kuongezeka kwa gharama za mradi.**

### 13.3.2 Malipo ya Shilingi Bilioni 1.57 Kulipwa Kutokana na Mabadiliko ya Kazi Yasiyoidhinishwa

Kanuni ya 110(5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013, kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016, inabainisha kuwa ongezeko la gharama za mradi wakati wa utekelezaji, ambalo linatokana na mabadiliko ya mawanda ya kazi lazima lipate idhini kutoka bodi ya zabuni.

Mapitio yangu ya hati ya malipo ya mkandarasi namba 5 yalibaini kuwapo kwa mabadiliko ya kazi yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.57, ambazo zililipwa kwa mkandarasi bila kuidhinishwa na bodi ya zabuni. Gharama hizi zilitokana usimamizi hafifu uliopelekea ongezeko la kazi kama uchimbaji, nondo, na kazi zingine, hali hii ilisababisha kuongezeka kwa gharama za mradi zaidi ya bajeti iliyopitishwa. Maelezo zaidi kwenye **Jedwali Na. 42.**

**Jedwali Na. 42: Malipo kwa mabadiliko ya kazi ambazo hazikuidhinishwa**

| Mchanganuo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|
| Gharama za magari manne aina ya pickup | 312,810,772.08 |
| Garama ya kazi za ziada | 108,548,428.80 |
| Uendeshaji wa magari ya mradi | 13,230,346.00 |
| Uchimbaji wa udongo | 1,981,915.36 |
| Kusafisha eneo la mradi | 5,746,737.00 |
| Kusafisha eneo la mradi | 1,513,820.00 |
| Kuchimba udongo mita 0 hadi 2 kwenda chini | 30,630,504.53 |
| Kazi ya nondo | 361,003,301.55 |
| Kumwaga zege la gredi 15 kwenye kalavati | 34,497,862.01 |
| Kumwaga zege la gredi 20 kwenye kalavati | 707,834,631.20 |
| Ujenzi wa matundu yenye kipenyo cha mm 50 kwa ajili ya kutolea maji | 729,960.00 |
| **Jumla ya Ongezeko la Kazi** | **1,578,528,278.53** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi katika Hati za malipo ya mkandarasi mwana 2024*

**Ninapendekeza DAWASA ianzishe mchakato imara wa kufuatilia na kuidhinisha gharama ili kuepuka mabadiliko yasiyoidhinishwa. Pia, DAWASA inapaswa kupata idhini ya mabadiliko yote katika mradi ili kuhakikisha kwamba gharama za mradi zinadhibitiwa kuepusha hatari ya kuzidi kwa gharama ya mradi.**

### 13.3.3 Ongezeko la Gharama Kiasi cha Shilingi Bilioni 5.24 Kutokana na Tathmini Hafifu na Ucheleweshaji wa Malipo ya Fidia kwa Waathirika wa Mradi

Kanuni namba 13(2) na (3) ya Kanuni za Ardhi (Tathmini ya Dhamani ya Ardhi kwa ajili ya Fidia) za Mwaka 2001 inataka fidia kulipwa ndani ya muda wa miezi sita baada ya tathmini. Pia, kanuni hizi zinabainisha kuwa kama malipo

hayatafanyika kwa wakati, fidia ya kuchelewesha malipo hayo italipwa kwa mnufaika.

Kupitia taarifa ya malipo ya fidia ya miaka 2014, 2025 na 2020 nilibaini kuwapo kwa ucheleweshaji wa malipo ya fidia ya ardhi katika Ujenzi wa Bwawa la Kidunda, ambapo fidia hiyo ilipaswa kulipwa kabla ya mwezi Novemba 2013. Ucheleweshaji huu ulisababisha malipo za ziada ya shilingi milioni 695.27 kama fidia itokanayo na kuchelewesha malipo kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 43**.

**Jedwali Na. 43: Hali ya malipo ya fidia ya ardhi kwa bwawa la kidunda**

| Awamu za Malipo | Idadi ya Wanufaika | Kiasi Kilichopaswa Kulipwa hadi Mwezi Novemba 2013 (Sh.) | Kiasi Kilicholipwa (Sh.) | Fidia ya Kuchelewesha Malipo (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| Malipo ya Awamu ya Kwanza Mwaka 2014 | 159 | 1,106,269,300 | 1,194,770,844 | 88,501,544 |
| Malipo ya Awamu ya Pili Mwaka 2017/2018 | 1239 | 3,124,895,677 | 3,644,553,349 | 519,657,672 |
| Malipo ya Awamu ya Pili Mwaka 2023/2024 | 44 | 122,043,800 | 209,161,844 | 55,421,644 |
| **Jumla** | **1442** | **4,353,208,777** | **5,048,486,037** | **695,277,261** |

***Chanzo***: *Uchambuzi wa mkaguzi wa taarifa za malipo ya fidia mwaka 2024*

**Jedwali Na. 43** linaonesha kuwa kiasi cha Shilingi milioni 695.27 kililipwa kama gharama ya kuchelewesha malipo ya fidia ya ardhi.

Kucheleweshwa kwa malipo ya fidia ya ardhi kulitokana na wamiliki wa ardhi kutokuwa na nyaraka muhimu za kuonesha umiliki halali wa eneo husika. Pia, kulitokana na wamiliki wa maeneo hayo kutoridhishwa na tathmini iliyofanyika hivyo kuyakataa malipo hayo.

Aidha, kupitia taarifa za malipo ya fidia ya mwaka 2015 kwa vijiji 10, nilibaini kuwa DAWASA ililipa nyongeza ya fidia ya ardhi kiasi cha shilingi bilioni 4.026 baada ya kurudia tathmini ya ardhi kwa waathirika wa mradi, ambao hawakuridhishwa na tathmini iliyofanyika awali. **Jedwali Na. 44** linaonesha mchanganuo wa gharama hizo.

**Jedwali Na. 44: Mchanganuo wa gharama za fidia baada ya kurudia tahthmini**

| Jina la Kijiji | Wanufaika | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| Bwila Chini | 118 | 261,416,086.53 |
| Kwa Tupa | 137 | 235,048,782.67 |
| Kwa Wagonzi | 219 | 417,049,823.87 |
| Kariakoo | 166 | 248,048,326.48 |
| Kwa Nyagongo | 253 | 372,981,218.22 |

| Jina la Kijiji | Wanufaika | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| Vikonge | 247 | 547,021,064.23 |
| Kiburumo I | 193 | 515,677,725.15 |
| Kiburumo II | 235 | 781,126,295.04 |
| Barabara | 159 | 228,062,795.44 |
| Manyunywe | 96 | 420,329,871.45 |
| **Jumla** | **1,823** | **4,026,761,989.08** |

***Chanzo***: *Uchambuzi wa mkaguzi katika taarifa za fidia mwaka 2024*

**Jedwali Na. 44** linaonesha kuwa Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Dar es Salaam ililipa kiasi cha shilingi bilioni 4.02 kama gharama za nyongeza kwenye madai ya fidia baada ya kurudia tathmini kutokana na waathirika wa mradi kutoridhika na tathmini ya awali. Hali hii ilifanya jumla ya malipo yaliyolipwa kwa ajili ya kufidia ardhi kuwa Shilingi bilioni 9.07, ingawa bajeti ilikuwa Shilingi bilioni 3.83, hivyo kufanya ongezeko la kiasi cha Shilingi bilioni 5.24.

Ongezeko hili lilitokana na tathmini ya awali kutokanyika kikamilifu hivyo kutoakisi uhalisia. Ongezeko pia lilisababishwa na wamiliki wa maeneo husika kutoridhishwa na fidia ya awali na ucheleweshaji wa malipo ya fidia ya ardhi.

**Ninapendekeza DAWASA ifanye tathmini kamili na sahihi ya mahitaji ya fidia wakati wa awamu ya mpango ili kuepuka kurudia tathmini na gharama za ziada. Bajeti za fidia zijazo zinapaswa kutiliwa maanani na kurekebishwa inapohitajika ili kuhakikisha zinarandana na mahitaji halisi, hivyo kupunguza hatari ya kuzidi kwa gharama.**




# SURA YA KUMI NA NNE

## Ukaguzi wa Kiufundi kwenye Ukarabati na Ujenzi wa Soko Jipya la Kariakoo, Soko Kuu la Mwanza, na Stendi ya Mabasi ya Nyamhongolo

# UKAGUZI WA KIUFUNDI KWENYE UKARABATI NA UJENZI WA SOKO JIPYA LA KARIAKOO, SOKO KUU LA MWANZA, NA STENDI YA MABASI YA NYAMHONGOLO

## 14.1 Utangulizi

Ukaguzi huu ulilenga kuangalia iwapo Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri za Jiji la Mwanza, na Halmashauri ya Manispaaa ya Ilemela zilisimamia kikamilifu ujenzi wa miradi ya masoko na stendi.

Ukaguzi ulilenga katika taasisi tatu; Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ambazo zinawajibika kwa ujenzi wa Soko Kuu la Mwanza, ujenzi wa Kituo cha Mabasi cha Nyamhongolo, na ukarabati wa Soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Wakati wa ukaguzi, ujenzi wa Soko la Karikoo ulioanza mwezi Januari 2022 ukiwa na thamani ya Shilingi bilioni 28 ulikuwa umefikia 95%. Ujenzi wa Soko Kuu la Mwanza ulioanza mwaka 2019 ukiwa na thamani ya Shilingi bilioni 21.8 ulikuwa umefikia 95%; na ujenzi wa Stendi ya Nyamhongolo wenye thamani ya Shilingi bilioni 26.6 ulikuwa umekamilika na inatumika.

## 14.2 Mipango na Usanifu wa Mradi

### 14.2.1 Kutofanyika kwa Uchunguzi wa Hali ya Uchakavu wa Masoko Kabla ya Kufanyika kwa Maboresho Kusababisha Ongezeko la Shilingi Milioni 757.02 za Gharama ya Kazi Kwenye Mradi

Kifungu cha 4.4.1.1 (b) (ii) cha Hadidu za Rejea za Mkataba wa Mshauri Elekezi wa Soko la Kariakoo zilimtaka mshauri elekezi kufanya uchuguzi wa hali ya uchakavu wa Soko la Kariakoo.

Nilibaini kuwa uchunguzi wa hali ya uchakavu haukufanyika kwa masoko mawili ambayo ni Soko la Kariakoo na Soko Kuu la Mwanza, hivyo kusababisha kutoandaliwa kikamilifu kwa mawanda ya kazi ya ukarabati wa Soko la Kariakoo na kusababisha ongezeko la gharama ya mradi kwa kiasi cha Shilingi milioni 577.90. Pia, michoro na makadirio ya bei kwa miundombinu iliyokuwa ikifanyiwa ukarabati haikuandaliwa kwenye ukarabati wa Soko Kuu la Mwanza kinyume na Kanuni ya 239(8) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, zinazozitaka taasisi nunuzi kutoanzisha zabuni kama makadirio ya gharama za kazi husika hayajaandaliwa.

Udhaifu huu ulisababisha kutengwa kwa kiasi cha Shilingi milioni 400 kwa ajili ya kazi ya ukarabati, ambacho hakikutosha kufanya ukarabati huo, hivyo kusababisha ongezeko la Shilingi milioni 179.12.

**Jedwali Na. 45** linaonesha ongezeko la gharama lililosababishwa na kutofanyika kwa uchunguzi wa hali ya uchakavu ili kujua mahitaji halisi kwa ajili ya matengenezo.

**Jedwali Na. 45: Ongezeko la gharama kutokana na kutofanya uchunguzi wa hali ya uchakavu**

| Jina la Mradi | Mabadiliko Yaliyotokea | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| Soko la Kariakoo | Kuongezeka kwa kazi za mabomba kwenye jengo la zamani | 288,884,097 |
| | Mabadiliko ya mfumo wa kuingiza hewa kwenye jengo la zamani | 241,718,676 |
| | Mabadiliko ya lifti kwenye jengo la zamani | 47,303,792 |
| | **Jumla ya Gharama za Mabadiliko kwa Soko la Kariakoo** | 577,906,567.17 |
| Soko Kuu Mwanza | Kazi za nyongeza kwenye jengo la zamani katika soko kuu la Mwanza | **179,121,025** |
| **Jumla ya Gharama za Mabadiliko** | | **757,027,592** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi wa mabadiliko ya gharama yaliyotokea kwenye Soko la Kariakoo na Mwanza*

Kulikuwa na ongezeko la kiasi cha Shilingi milioni 577.9 kwa matengenezo ya Soko la Kariakoo na Shilingi milioni 179.12 kwa soko la Mwanza, hivyo kufanya jumla ya ongezeko kuwa Shilingi milioni 757.02.

Kutofanyika kwa uchunguzi wa uchakavu katika majengo kulitokana na watekelezaji wa miradi kushindwa kuwasimamia washauri elekezi ili kuhakikisha wanafanya kazi kwa kuzingatia hadidu za rejea walizopewa.

**Ninapendekeza Halmashauri za Jiji la Mwanza na Jiji la Dar es Salaam zihakikishe kuwa uchunguzi wa hali ya majengo unafanyika kikamilifu kabla ya kuyafanyia matengenezo ili kuhakikisha mawanda ya kazi na gharama zake yanaandaliwa kikamilifu.**

### 14.2.2 Mabadiliko na Ongezeko la Kazi Kulikosababishwa na Usanifu Hafifu wa Soko la Mwanza Shilingi Bilioni 1.96

Kanuni ya 22(2) ya Kanuni za Ununuzi kwa Umma za Mwaka 2013, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016, inataka usanifu wa miradi ikiwemo

uandaaji wa michoro na viwango vya ubora kuandaliwa kikamilifu kwa kuzingatia lengo la mradi na mahitaji ya mradi husika.

Nilibani ongezeko la kazi za mradi wa Soko la Mwanza lililokuwa na gharama ya Shilingi bilioni 1.96. Kuongezeka kwa gharama hizo kulitokana na upungufu wa usanifu uliofanywa, ambao haukuakisi kikamilifu mahitaji yote ya mradi. **Jedwali Na. 46** linaonesha kazi ambazo hazikujumuishwa kwenye usanifu uliofanywa.

**Jedwali Na. 46: Ongezeko la gharama kutokana na usanifu hafifu kwenye ujenzi wa soko la mwanza**

| Kazi zilizoongezeka | Kiasi (Sh.) | Maelezo ya Mabadiliko |
|---|---|---|
| Ongezeko la vyoo viwili | 232,403,600 | Hitaji la Mwanza Jiji |
| Ongezeko la maduka mapya | 172,302,500 | Hitaji la Mwanza Jiji |
| Kuongeza ukubwa wa maduka ya nje na kubomoa maeneo mbalimbali | 14,720,940 | Hitaji la Mwanza Jiji |
| Kuweka miundombinu ya kuzuia maji ya mvua | 27,839,427 | Mabadiliko ya usanifu |
| Ujenzi wa zege la kuzuia maji yasiingie kwenye maungio ya sakafu | 140,616,000 | Mabadiliko ya usanifu |
| Ujenzi wa tanki la maji na ngazi | 85,424,950 | Hitaji la Mwanza Jiji |
| Ongezeko la grili za milango | 138,376,000 | Mabadiliko ya usanifu |
| Kuongeza eneo la kuchezea watoto | 33,377,550 | Hitaji la Mwanza Jiji |
| Ongezeko la miundombinu ya zimamoto | 995,700,040 | Hitaji la Mwanza Jiji |
| Ongezeko za vifaa vya jikoni | 74,108,800 | Hitaji la Mwanza Jiji |
| Ongezeko la bati za mageti | 29,600,000 | Mabadiliko ya usanifu |
| Ongezeko la vifaa ya kuvuna maji ya mvua | 18,294,000 | Mabadiliko ya usanifu |
| **Jumla** | **1,962,763,807** | |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Mkaguzi wa Hati za Malipo ya Mkandarasi kwa Soko la Mwanza*

**Jedwali Na. 46** linaonesha mabadiliko yaliyotokea kwenye Soko la Mwanza na kusababisha ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 1.96 baada ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza kutoa mapendekezo mapya, ambayo hayakubainishwa wakati wa usanifu.

Upungufu katika usanifu ulitokana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kushidwa kuhakikisha mahitaji yote ya mradi yanabainishwa kabla ya kufanya usanifu ili kuhakikisha yanajumuishwa kwenye usanifu wa mradi.

**Ninapendekeza Halmashauri ya Jiji la Mwanza iwe inafanya uchambuzi yakinifu ili kubainisha mahitaji yote ya miradi na kuhakikisha kuwa**

**yanajumuishwa kwenye usanifu ili kupunguza ongezeko la gharama wakati wa utekelezaji wa miradi.**

## 14.3 Usimamizi wa Mikataba

### 14.3.1 Malipo ya Nondo Kiasi cha Shilingi Bilioni 9.87 Bila Kubainisha Kiasi Kilichohitajika kwa Kila Aina ya Nondo Iliyotumika

Mapitio niliyofanya kwenye nukuu ya gharama za mradi na ukubwa wa kazi na malipo ya nondo kwa miradi mitatu ya Soko la Kariakoo, Soko la Mwanza, na Stendi ya Nyamhongolo nilibaini kuwa viwango vya nondo vilivyotumika havikubainishwa kwa kila aina ya nondo bali kilitolewa kiwango jumuishi kwa nondo zote. Hali hii ilikuwa kinyume na Kifungu cha F16(b) cha Mwongozo wa Upimaji wa Kazi za Ujenzi wa Afrika Mashariki, Toleo la Kwanza la Mwaka 1976. Mwongozo huo unataka vipimo vya nondo kubainishwa kwa uzito wa kila aina ya nondo iliyotumika. **Jedwali Na.** 47 linaonesha mchanganuo wa nondo zilizolipiwa bila ya kubainisha uzito kwa kila aina za nondo zilizotumika.

**Jedwali Na. 47: Nondo zilizolipwa bila ya kubainisha uzito na unene kwa kila aina ya nondo**

| Sehemu ya Jengo | Kipengele kwenye Nukuu ya Bei | Mchanganuo | Kipimo | Uzito wa Nondo | Gharama kwa Kilo (Sh.) | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Nondo za Soko la Kariakoo** | | | | | | |
| Msingi | 3/1/2/6A; | Nondo za unene wa 8mm hadi 32mm | Kg | 527,952 | 3,226 | 1,703,173,152 |
| Gorofa ya 1 hadi ya 3 | 3/1/3/1D | | Kg | 633,906 | 3,226 | 2,044,980,756 |
| Ghorofa ya 4 & 5 | 3/1/4/1D | | Kg | 325,065 | 3,226 | 1,048,659,690 |
| Ngazi | 3/1/5/1D | | Kg | 14,336 | 3,226 | 46,247,936 |
| Lifti | 3/1/6/1B | | Kg | 57,380 | 3,226 | 185,107,880 |
| **Nondo za Soko Kuu la Mwanza** | | | | | | |
| Msingi | 2/2/U | Nondo za unene wa 8-25mm | Tani | 652 | 2,900,000 | 1,890,800,000 |
| Nguzo za Jengo na Sakafu za Juu | 2/6/D | Nondo za unene wa 8-25mm | Tani | 422 | 2,900,000 | 1,223,258,000 |
| **Nondo za Stendi ya Mabasi ya Nyamhongolo** | | | | | | |
| Msingi | 2/1/4j | Ukubwa mbalimbali | Kg | 402,516 | 2,417.04 | 972,897,272 |
| Nguzo za Jengo na Sakafu za Juu | 2/2.1f | Ukubwa mbalimbali | Kg | 305,820 | 2,417.04 | 739,179,172 |

| Sehemu ya Jengo | Kipengele kwenye Nukuu ya Bei | Mchanganuo | Kipimo | Uzito wa Nondo | Gharama kwa Kilo (Sh.) | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ngazi | 2/3.1d | Ukubwa mbalimbali | Kg | 6,715 | 2,417.04 | 16,230,423 |
| **Jumla ya Kiasi kwa Mradi yote Mitatu** | | | | | | **9,870,534,283** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi wa hati za malipo ya mkandarasi kwa Soko Kariakoo, Soko la Mwanza, na Stendi ya Nyamhongolo*

**Jedwali Na. 47** linaonesha kuwa kiasi cha shilingi bilioni 9.87 kililipwa katika miradi yote mitatu kwa kubainisha uzito wa jumla wa nondo zote bila kuonesha uzito kwa kila aina ya nondo (unene wa nondo) zilizotumika. Hali hii inamaanisha kuwa hakukuwa na tathmini ya kiwango cha kila aina za nondo zilizotumika katika majengo husika, hivyo kutokuwa na uwezo wa kuhakikisha kuwa malipo yaliyofanyika yanaakisi ukubwa wa ndondo zilizotumika.

Kutobainishwa kwa kiasi cha kila ukubwa wa nondo zilizotumika kulitokana na kutoandaliwa kwa mchanganuo wa aina na kiasi cha nondo zitakazotumika kwenye miradi wakati wa usanifu. Hali hii ilisababisha kuongezeka kwa gharama za miradi.

**Ninapendekeza Halmashsuri za Jiji la Mwanza, Dar es Salaam, na Manispaa ya Ilemele zihakikishe kuwa mchanganuo wa nondo unaandaliwa kikamilifu kabla ya kuanza mradi, na kuhakiki idadi ya nondo zilizotumika kwa kila aina ya nondo kabla ya kufanya malipo ili kuepusha hatari ya kuzidisha malipo kwa wakandarasi.**

### 14.3.2 Malipo ya Shilingi Milioni 766.90 Kurejesha Gharama za Mkandarasi Bila ya Kuwa na Nyaraka za Ushahidi

Kifungu cha 54.2 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba kinataka malipo ya gharama za mshauri elekezi kufanyika ndani ya siku 60 baada ya kupokea nyaraka za ushahidi wa gharama hizo.

Mapitio yangu ya malipo yaliyofanywa kwa washauri wa mradi yalionesha kuwa Shilingi milioni 766.90 zililipwa kama gharama za fidia kwa Washauri wa Mradi bila nyaraka za kuthibitisha vya malipo hayo. Kiasi hicho kilijumuisha Shilingi milioni 181.30 zilizolipwa kwa ujenzi mpya wa Soko la Kariakoo, na Shilingi milioni 585.60 zilizolipwa kwa Soko Kuu la Mwanza, jumla ya Shilingi milioni 766.90.

Malipo ya fidia bila nyaraka za kuthibitisha yanaonyesha kuwa Halmashauri za Jiji la Mwanza na Dar es Salaam hazikudhibiti gharama za mradi ipasavyo kwa kuhakikisha kuwa gharama zote za fidia zililipwa baada ya kupokea uthibitisho wa nyaraka za malipo. Pia, inaonesha udhaifu wa udhibiti upande wa mteja ambao unaweza kusababisha hasara kwa serikali.

**Ninapendekeza Halmashauri za Jiji la Mwanza na Dar es Salaam zifanye tathmini na kurejesha malipo ya fidia yasiyo halali ya Shilingi milioni 766.90 yaliyolipwa kwa Washauri wa Mradi.**

### 14.3.3 Madai ya Fidia ya Shilingi Bilioni 1.35 kwa Mshauri Elekezi Kutokana na Kuchelewa Kukamilika kwa Miradi

Kifungu cha 1.1 cha Masharti Mahususi ya Mkataba wa mkandarasi kinabainisha kuwa muda wa kutekeleza mradi kwa Soko la Kariakoo ulikuwa miezi 21 kuanzia tarehe 7 Januari 2022 hadi tarehe 6 Oktoba 2023. Kwa Soko la Mwanza, muda wa ujenzi ulikuwa miezi 18 kuanzia tarehe 22 Agosti 2019 hadi tarehe 25 Februari 2021.

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini kuwa mwezi Oktoba 2024, miradi miwili ya Soko la Kariakoo na Mwanza haikuwa imekamilika, ikiwa imechelewa kwa siku 376 na 44 mtawalia. Kuchelewa huku kulitokana na sababu mbalimbali kama vile halmashauri husika na mshauri elekezi kushindwa kuidhinisha michoro kwa wakati, ambapo nilibaini kuwa kulikwa na ucheleweshaji wa kati ya siku 17 hadi 78 kwa soko la Kariakoo. Wakandarasi kutokulipwa kwa wakati kulisababisha kupungua kwa kasi ya ujenzi wa miradi na ongezeko la kazi wakati wa ujenzi.

Nilibaini pia kuwa, licha ya kuchelewa kwa miradi huathiri ufikiaji wa malengo ya miradi kwa wakati, pia kuliathiri gharama za miradi. Kupitia madai ya kwenye mradi nilibaini kuwa washauri elekezi waliwasilisha madai ya kiasi cha Shilingi milioni 209.98 kwa Soko la Kariakoo na Shilingi bilioni 1.14 kwa Soko la Mwanza. Madai hayo yalikuwa kwa ajili ya kusimamia miradi kwa kipindi ambacho muda wa utekelezaji uliongezwa. Hadi kipindi cha ukaguzi wangu, madai hayo yalikuwa yanasubiri kuidhinishwa na halmashauri hizo.

**Ninapendekeza Halmashauri za Jiji la Mwanza na Dar es Salaam zihakikishe zinaidhinisha kwa wakati michoro na mabadiliko ya kazi za ujenzi na zifanye malipo ya wakandarasi kwa wakati ili kuepuka ucheleweshaji wa kazi.**



# SURA YA KUMI NA TANO

## Ukaguzi wa Kiufundi wa Ufungaji na Matengenezo ya Alama za Barabara na Taa za Kuongoza Magari

# UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UFUNGAJI NA MATENGENEZO YA ALAMA ZA BARABARA NA TAA ZA KUONGOZA MAGARI

## 15.1 Utangulizi

Wakala wa Barabara Tanzania na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini zimekuwa zikitekeleza miradi mbalimbali inayohusiana na ufungaji na matengenezo ya alama za barabarani na taa za kuongozea magari nchini.

Ili kuhakikisha thamani ya pesa, nilifanya ukaguzi wa kiufundi unaohusisha miaka nane ya kifedha kuanzia 2016/17 hadi 2023/24 kuhusu miradi ya barabara katika mikoa mitano (Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Pwani na Tabora) ili kutathmini kama mipango, uwekaji, na matengenezo ya samani za barabara na alama za usalama barabarani zilifanywa kwa ufanisi kulingana na muda, gharama, wigo, na ubora ili kuboresha usalama wa barabara kwa watumiaji. Nilitathimini vipengele vyote muhimu, kuanzia awamu ya upangaji hadi kukamilika na kutoa hitimisho kuhusu maendeleo yaliyofikiwa, udhibiti wa gharama, na ubora wa mradi. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye **Kiambatisho Na. VI**.

## 15.2 Mipango na Usanifu wa Mradi

### 15.2.1 Kuelemewa kwa Taa za Kuongozea Magari Kwenye Makutano ya Barabara Kutokana na Usanifu Uliopitwa na Wakati na Kufanya Askari wa Usalama Barabarani Kuongeza Magari

Sehemu ya 6.3 ya Mwongozo wa Uwekaji Alama za Barabarani wa Mwaka 2009 inataka lengo kuu la kufunga alama katika makutano liwe kupunguza ucheleweshaji wa foleni kwa kuondoa au kupunguza misongamano katika makutano ya barabara, vivuko vya watembea kwa miguu na vivuko vya reli.

Ukaguzi wangu ulitembelea sehemu saba za makutano ya barabara jijini Dar es Salaam na kugundua kuwa mtiririko wa magari na mifumo ya taa za kuongozea magari ilikuwa ikidhibitiwa na askari wa usalama barabarani badala ya taa na alama za kuongozea magari kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 48**.

**Jedwali Na. 48: Makutano ya barabara yanayoongozwa na askari wa usalama barabarani**

| Makutano ya Barabara | Jina la Barabara |
|---|---|
| Mwenge | Barabara ya Bagamoyo |
| Moroko | |
| Afrikana - Mbezi beach | |
| Kawe - Lugalo | |

| Makutano ya Barabara | Jina la Barabara |
|---|---|
| Goba – Mbezi Shule | |
| Kimara Bucha | Barabara ya Morogoro |
| Magomeni | |

***Chanzo**: Uchambuzi wa wakaguzi katika uhakiki wa moja kwa moja kwa barabara zilizochaguliwa mwaka 2024*

Makutano hayo yalikuwa na msongamano mkubwa wa magari, ikionesha haja ya kuwa na bajeti ya kutosha ya matengenezo ya taa za kuongoza magari. Hata hivyo, vikwazo vya bajeti vimesababisha ukosefu wa matengenezo ya kutosha, na kupunguza uwezo wa kukabiliana na ongezeko la magari na mabadiliko ya muundo kwenye barabara kuu. TANROADS hupokea mgao wa kila mwaka wa Shilingi bilioni 1.8 kwa matengenezo ya samani za barabara, ambao ni kidogo kulinganisha na bajeti halisi ya kiasi cha Shilingi bilioni 200 zinazohitajika. Aidha, misafara ya mara kwa mara, hasa kwenye Barabara ya Bagamoyo, inavuruga utendaji wa taa za kuongozea magari, na kusababisha msongamano wa magari hivyo kuhitaji udhibiti wa askari wa usalama barabarani.

Ilibainika kuwa taa za kuongoza magari katika makutano ya barabara nilizotembelea hazikuwa zinafanya kazi kwa ufanisi kudhibiti msongamano wa magari kutoka mielekeo tofauti.

**Ninapendekeza TANROADS kwa kushirikiana na mamlaka za bajeti, ihakikishe kuwa bajeti inatolewa kulingana na mahitaji halisi ili kuwezesha matengenezo ya kutosha ya taa za kuongoza magari. Kwa kuongezeka kwa msongamano wa magari kwenye makutano, matengenezo makubwa na ukarabati huenda yakahitajika au hata ujenzi wa madaraja ya juu kwenye makutano ya barabara za Mwenge, Moroko, Magomeni na Afrikana-Mbezi Beach.**

## 15.3 Usimamizi wa Mikataba

### 15.3.1 Hali Isiyoridhisha ya Alama za Barabarani

Kifungu cha 5.2.1 (c) cha Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani ya Mwaka 2009 kinaitaka wizara inayohusika na uendelezaji wa miundombinu kuhakikisha kuwa miradi yao ya barabara inaambatana na viwango na miongozo ya usalama barabarani kwa matumizi ya barabara, makutano, alama za barabarani na mipango ya usimamizi wa magari.

Mapitio yangu na ushuhudiaji wa moja kwa moja wa miradi teule ya barabara ulibaini kutozingatiwa kikamilifu idadi inayohitajika ya alama za barabarani (alama za barabarani, taa za kuongoza magari, na taa za barabarani) dhidi ya

idadi iliyopatikana kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 49.** Nilibaini upungufu wa taa za barabarani 1,795 sawa na asilimia 73 ya taa za barabarani zinazohitajika kando ya Barabara ya Bagamoyo.

### Jedwali Na. 49: Hali ya idadi inayohitajika ya alama za barabarani

| Jina la barabara | Alama za barabarani | | Taa za Kuongozea Magari | | Taa za Barabarani | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Zinazohitajika | Zilizopo | Zinazohitajika | Zilizopo | Zinazohitajika | Zilizopo |
| Barabara ya Bagamoyo | 1710 | 934 (55%) | 28 | 24 (86%) | 2445 | 650 (27%) |
| Barabara ya Morogoro | 1635 | 1221 (75%) | 30 | 23 (77%) | 2335 | 1840 (79%) |
| Barabara ya Dodoma - Bereko | 455 | 322 (71%) | 1 | 1 100%) | 112 | 56 (50%) |
| Barabara ya Nzega - Tabora | 485 | 325 (67%) | NA | NA | 355 | 282 (79%) |
| Barabara za Mji wa Serikali | 281 | 169 (60%) | 2 | 2 (100%) | 739 | 1635 (221%) |
| Barabara ya Visiga Zegereni | 42 | 42 (100%) | NA | NA | 350 | 350 (100%) |
| Barabara ya Nyengedi-Mnara | 30 | 10 (33%) | NA | NA | 8 | 8 (100%) |
| Barabara ya eneo la viwanda Nala | 70 | 49 (70%) | NA | NA | 114 | 150 (131%) |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwa ripoti ya usanifu na michoro iliyojengwa mwaka 2024*

Kuhusu alama za barabarani, Barabara ya Visiga-Zegereni ndiyo barabara pekee yenye upatikanaji wa alama za barabarani kwa 100%, huku Barabara ya Nyengedi-Mnara ikiwa na kiwango cha chini kabisa cha upatikanaji kwa 33% kutokana na kazi ambazo hazijakamilika. Barabara ya Bagamoyo ilikuwa na 55% kutokana na ujenzi unaoendelea wa Barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Nne, ambayo ilisababisha ubomoaji wa alama za barabarani zilizopo, hivyo kuathiri usalama wa barabara na matumizi yake.

Barabara ya Bagamoyo ilikuwa na idadi ndogo ya taa za barabarani kwa 27% na taa za kuongozea magari kwa 86% kwa sababu ya ujenzi unaoendelea wa Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka. Barabara ya Visiga-Zegereni na Barabara ya Nyengedi-Mnara ilikuwa na taa za kuongozea magari kwa 100%. Hata hivyo, Barabara za Mji wa Serikali na Barabara ya Hifadhi ya Viwanda ya Nala zinaonesha asilimia kubwa kuliko kawaida, kutokana na usanifu duni ambao ulisababisha tofauti wakati wa utekelezaji.

Kutozingatia mahitaji ya alama za barabarani kulisababishwa na matengenezo duni na ufahamu katika maeneo yenye viwango vya juu vya uharibifu ambao unahatarisha uendelevu wa usalama kwa watumiaji wa barabara

Ni maoni yangu kwamba hali ya jumla ya alama za barabarani hairidhishi kama ilivyo na alama za barabarani zilizofifia zinasababisha hatari ya matumizi ya barabara, ajali, usalama wa watumiaji wa barabara, na ufanisi wa usafirishaji.

Kwa kuongezea, alama zilizoharibika au zinazokosekana, alama zilizofifia, na kuharibika kwa taa za kuongozea magari huhatarisha uwezo wa madereva kusafiri salama kwa sababu ya ukosefu wa mwongozo bayana au maonyo ya sehemu hatarishi, mipaka ya mwendokasi, au hali ya barabara. Hususani, kuwapo kwa alama za barabarani zilizofifia hupunguza mwonekano wa mwisho wa njia za magari wakati wa usiku au wakati wa hali mbaya ya hewa.

### 15.3.2 Upimaji wa Uthibiti wa Ubora Usiojitosheleza wa Rangi za Alama za Barabarani

Kifungu cha 5502 cha Viwango Mahususi vya Kazi za Barabara vya Mwaka 2000 kinataka uhakikisho wa ubora wa rangi za alama za barabarani zilizotumika kama ilivyoelezwa katika maelezo maalumu, mchanganyiko wa plastiki katika rangi za alama za barabarani zinazoyeyushwa na moto zitazingatia kiwango cha BS 3262. Uagizaji wa rangi kwa ajili ya alama za barabarani unazingatia vipimo vya kukubalika kwa bidhaa kwa idhini ya mwajiri kabla ya kuagiza vifaa ili kuangalia asili na mchanganyiko wake. Vifaa hivyo vinachukuliwa kwa ajili ya vipimo vya uthibitisho ili kuhakikisha ubora wa rangi za alama za barabarani dhidi ya mchanganyiko wake na kuimarisha ukaguzi kabla ya kuweka alama za barabarani.

Kinyume na mahitaji, nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini hazikufanya vipimo vya uthibitisho dhidi ya mchanganyiko wa rangi kutoka nje kabla ya utekelezaji wa alama za barabarani.

Ukosefu wa uhakiki wa ubora wakati wa matengenezo ya alama za barabarani ulisababishwa na usimamizi duni wa miradi ya matengenezo ya barabara kwani ilichukuliwa kama mikataba midogo ya kazi ambayo haikutengewa bajeti ya uhakiki na kupima ubora wa kazi. Hali hii huathiri uhai na ubora wa alama za barabarani, ambazo huhitaji matengenezo ya mara kwa mara na kuongeza gharama kwa serikali.

### 15.3.3 Wizi wa Alama za Barabarani zenye Thamani ya Shilingi Milioni 170.48

Kifungu cha 31(2) cha Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 kinamwona mtu yeyote atakayeharibu, kuondoa, au kuficha alama za barabarani kuwa ametenda kosa na atawajibika kutozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

Ukaguzi wangu kwa njia ya ushuhudiaji nilioufanya tarehe 1 Novemba 2024 katika Barabara ya Tabora-Nzega (Tabora) na Barabara za Mji wa Serikali Mtumba (Dodoma) ulibaini matukio ya wizi wa alama za barabarani 78 na kingo za barabara 153 katika Barabara ya Tabora-Nzega huku alama nne za barabarani zikiibwa katika Barabara za Mji wa Serikali Mtumba kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 50.**

**Jedwali Na. 50: Uchambuzi wa wizi wa alama za barabara**

| Jina la Barabara | Alama za barabarani Zilizoibwa | | Thamani ya Alama za Barabarani Zilizoibwa (Sh. milioni) |
|---|---|---|---|
| | Alama za Barabarani | Kingo za Barabara | |
| Barabara ya Tabora-Nzega | 78 | 153 | 168.00 |
| Barabara za Mji wa Serikali | 4 | - | 2.48 |
| **Jumla** | | | **170.48** |

***Chanzo***: *Uchambuzi wa wakaguzi kwa njia ya ushuhudiaji wa moja kwa moja na Ripoti ya Mkoa wa Tabora kuhusu alama za barabarani ya mwezi Mei 2018*

Kiwango kikubwa cha uharibifu katika Barabara ya Tabora-Nzega kilitokana na biashara ya vyuma chakavu vya alumini. Alama za barabarani na matumizi ya vifaa vya thamani vinavutia zaidi wizi kwa sababu vinauzika kwa matumizi ya utengenezaji wa vifaa vya chuma.

Alama za barabarani zilizoibiwa zinahitaji ukarabati na kurudishiwa hivyo kusababisha gharama za ziada za matengenezo. Katika Miaka ya Fedha 2019/2020 hadi 2022/2023, jumla ya shilingi milioni 30 zilitumika kwa ajili ya ukarabati au kurudishia alama za barabarani zilizoibwa. Kuchelewa kubadilisha alama za barabarani zilizoibwa hupunguza usalama barabarani kwa watumiaji.

**Ninapendekeza TANROADS na TARURA zihakikishe kuwa alama zote za barabarani na kingo za barabara zinawekwa vizuri kulingana na vipimo. Aidha, ziongeze ushirikiano na vyombo vingine vya usalama vya serikali ili kudhibiti kikamilifu wizi na uharibifu wa alama za barabarani na kuwawajibisha wahusika.**

## 15.4 Masuala ya Mazingira, Jamii, na Afya

### 15.4.1 Alama za barabarani kuzuiwa na miti na vichaka kutokana na ukosefu wa matunzo

Sehemu ya 4.1 ya Mwongozo wa Uwekaji wa Alama za barabarani wa Mwaka 2009 inataka alama za barabarani kuonekana kwa madereva kutoka umbali unaofaa. Hali hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa mimea, majengo, vifaa vya ujenzi, au vitu vingine havizuii alama hizo. Uonekanaji bayana wa alama za barabarani ni muhimu kwa usalama wa watumiaji wa barabara, uzingatiaji wa sheria, na upunguzaji wa hatari za ajali.

Mapitio yangu na ukaguzi kwa njia ya ushuhudiaji uliofanywa katika Barabara ya Tabora-Nzega, Barabara ya Dodoma-Bereko, na barabara za Mji wa Serikali Mtumba ulibaini kutokuwapo kwa matengenezo ya mara kwa mara ya kuhakikisha alama za barabarani zinaonekana kama inavyotakiwa. Nilibaini kuwapo kwa miti, nguzo za umeme, na vifaa vya ujenzi, vilivyokuwa zimezuia uwekaji wa alama za barabara. Vikwazo hupunguza ufanisi wa alama na kuzuia madereva kuona mipaka ya mwendokasi, mwongozo wa mwelekeo, na maonyo ya maeneo hatarishi. Kutoonekana bayana kwa alama muhimu za maonyo kama vile mipaka ya mwendokasi, alama za hatari, na vivuko vya watembea kwa miguu kunaweza kupotosha na kuongeza uwezekano wa ukiukaji wa alama, mgongano, na ajali za watembea kwa miguu na madereva.

**Ninapendekeza TANROADS na TARURA zidhibiti kwa wakati ukuaji wa nyasi zilizozidi na kuondoa vizuizi vingine vya alama za barabarani ili alama hizo ziwe zionekana wazi na kwa urahisi na watumiaji wa barabara.**



# SURA YA KUMI NA SITA

## Ukaguzi wa Kiufundi wa Ubora wa Usanifu wa Kazi wa Barabara

# UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UBORA WA USANIFU WA KAZI ZA BARABARA

## 16.1 Utangulizi

Usanifu wa barabara ni shughuli muhimu katika mradi wa ujenzi kwa utekelezaji wenye mafanikio. Nilifanya ukaguzi wa kiufundi kwenye miradi kumi ya ujenzi wa barabara inayotekelezwa na TANROADS, nikizingatia hasa ubora wa usanifu wa barabara. Ukaguzi ulitathmini iwapo michakato ya usanifu na vipimo ilizingatiwa ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi bila athari za gharama zinazotokana na mabadiliko ya usanifu.

Ukaguzi huu wa kiufundi umehusisha miaka kumi, kuanzia Mwaka wa Fedha 2013/14 hadi 2023/24, ukizingatia miradi iliyokamilika, inayoendelea, na miradi ambayo ilikuwa katika hatua ya upembuzi yakinifu. Kipindi hiki kilichaguliwa ili kuruhusu tathmini ya ufanisi wa usanifu wa barabara kuhusu muda wake uliotarajiwa na kuhakikisha uendelevu wa miundombinu ya barabara. Miradi ya barabara iliyokaguliwa inawasilishwa katika **Kiambatisho Na. VII**.

## 16.2 Ushirikishaji Usiotosheleza wa Wadau na Utambuzi Hafifu wa Viashiria Hatarishi Wakati wa Hatua ya Usanifu

Sehemu ya 3.2.2 ya Mwongozo wa Usanifu wa Muundo wa Barabara wa Mwaka 2011 inataka utafiti wa upembuzi yakinifu kufanyika ili kuhakikisha mipango shirikishi ya kutosha na kushauriana na wadau wa sekta ya umma na binafsi.

Mapitio yangu ya taarifa za usanifu wa miradi ya barabara teule ulibaini kuwa TANROADS ulihusisha wadau husika, kama vile watu walioathirika na miradi, wakurugenzi wa halmashauri, TTCL na RUWASA wakati wa hatua za upembuzi yakinifu wa miradi. Hata hivyo, ushirikishaji na uratibu haukupunguza au kuondoa changamoto za uhamishaji na fidia wakati wa utekelezaji wa miradi kutokana na kuendelea kwa changamoto hiyo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 51**.

Nilibaini kuwa si huduma zote zilizopo zilitambuliwa kwa ajili ya kuhamishwa. Pia, mchakato wa tathmini haukujumuisha mali zote na watu walioathirika na miradi hiyo kwenye barabara, kutokana na ukosefu wa michoro baada ya ujenzi ili kutambua maeneo ya miundombinu ya wamiliki ili kuhamisha matumizi.

Aidha, nilibaini kuwa hakukuwa na hatua za kupunguza vikwazo vilivyobainishwa ambavyo havikushughulikiwa kikamilifu katika usanifu wa kina na makadirio ya gharama za miradi ili kuhakikisha masuala yote ya fidia na uhamisho yanahesabiwa wakati wa utekelezaji wa miradi. Kwa mfano, nilibaini kuwa uratibu usioridhisha kati ya Wakala wa Barabara Tanzania na Shirika la

Reli Tanzania ulisababisha kukwama kwa ujenzi wa sehemu ya kilomita 1 ya barabara ya mzunguko wa nje (km 112.3) kutokana na kutojengwa kwa daraja la juu katika reli ya kisasa baina ya kilomita ya 49+200 katika Jiji la Dodoma kwa kiwango cha lami kipande cha kwanza cha Nala-Veyula-Mtumba-Ihumwa-Bandari Kavu (km 52.3). **Jedwali Na. 51** linaonesha athari za uratibu duni baina ya wadau wa miradi.

**Jedwali Na. 51: Athari za uratibu duni baina ya wadau wa miradi**

| Jina la Mradi | Hali Ilivyoonekana | Athari |
|---|---|---|
| Ujenzi wa Miundombinu ya Usafiri wa Haraka wa Mabasi Dar es Salaam - Awamu ya 3, Kipande cha Kwanza (km 23.33) | - Mapitio yangu ya barua yenye Kumb. Na. CA.463/563/71/L/99/BIM.8950 ya tarehe 2 Oktoba 2024 yalibaini ushiriki duni wa vituo vya kijamii kama vile Soko la Buguruni lililoathiriwa na mradi huo.<br>- Mapitio yangu ya barua za mawasiliano ya mradi yalibaini kuwa kulikuwa na mashauriano duni na mamlaka za huduma kama Wakala wa Barabara Tanzania, Shirika la Simu Tanzania na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam. | - Kuongezeka kwa idadi na mabadiliko ya mawanda ya mradi, ambayo yalithibitisha madai ya mkandarasi kwa upanuzi wa muda.<br>- Madai ya mkandarasi (dai Na.4, 6, 9, na 10) na kuongezeka gharama za nyaya kwa Shirika la Simu Tanzania shilingi 1,905,878,387.27 |
| Tabora-Koga-Mpanda (Mkoa wa Tabora-Mpanda km 105.389 Kipande cha 3, Kasinde-Mpanda na Uruwira Mji sehemu ya km 2.29) | - Mapitio yangu ya Ripoti ya Mwisho ya Mradi, mwezi Septemba 2023 yalibaini katika sehemu B.4.1 9 (ii) kwamba hakukuwa na tathmini ya watu walioathirika na mradi wakati wa hatua ya usanifu ili kuhakikisha kuondolewa kwao kabla ya kuanza kwa mradi. | Kuhama kwa usawa kwa mita 15 kwa sehemu ya km 2.752 (km 349 + 800 - 352 + 552.39), ambayo iliongeza mawanda wa mradi. |
| Uboreshaji wa Barabara ya Bagamoyo-Sadani-Pangani-Tanga (km 256) kwa Kiwango cha Lami, Kipande cha 1 (Pangani-Tanga, km 50) | - Mapitio yangu ya ripoti ya maendeleo ya mradi ya kila mwezi Na. 47, mwezi Agosti 2024, katika sehemu ya 16.2, yalibaini kuwa kulikuwa na utambuzi usioridhisha wa watu wote na mali zilizoathiriwa na mradi huo na utambuzi duni wa huduma ndani ya barabara wakati wa hatua ya usanifu. | - Kuchelewa kwa fidia na kuhamishwa kwa huduma ambazo zilisababisha madai ya mkandarasi kwa muda wa ziada. |
| Uboreshaji wa Barabara ya Itoni-Ludewa-Manda (km 211.4) kwa kiwango cha lami, Kipande cha 1 (Itoni-Lusitu 50 km) | - Nilibaini kuwa kulikuwa na utambuzi usioridhisha wa watu wote na mali zilizoathiriwa na mradi huo, ikiwa pamoja na makaburi na mashamba ya chai kwa sehemu ya km 3.15 (9 + 950 hadi 10+300) na utambuzi duni wa huduma ndani ya barabara wakati wa hatua ya usanifu. | - Ongezeko la gharama za uhamishaji wa huduma kwa shilingi 250,000,000<br>- Ongezeko la gharama za ununuzi wa ardhi kwa shilingi 3,007,879,357.69. |
| Ujenzi wa Barabara ya Sakina-Tengeru | - Mapitio yangu Sehemu ya 3.7 ya ripoti ya mwisho ya mradi, mwezi Aprili 2019, yalibaini kuwa usanifu | - Ongezeko la gharama za uhamishaji wa huduma kwa shilingi 504,443,890.57 |

| Jina la Mradi | Hali Ilivyoonekana | Athari |
|---|---|---|
| na Barabara ya Mchepuko Arusha | wa awali haukushirikisha vya kutosha wadau katika mradi husika katika kutambua na kukadiria gharama za uhamishaji wa huduma na upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. | - Ongezeko la gharama za ununuzi wa ardhi kwa shilingi 6,143,311,374.14. |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Usanifu na Nyaraka za majalada ya miradi, 2024*

Ni maoni yangu kwamba mashauriano na wadau wa miradi yalifanyika wakati wa utekelezaji wa miradi na si wakati wa awamu ya kupanga na usanifu ili kupunguza vikwazo vinavyoweza kujitokeza, kama vile nyumba, nguzo za umeme, mabomba ya maji, na nyaya zilizomo ndani ya mradi.

**Ninapendekeza TANROADS ahakikishe inashirikiana kikamilifu na wadau, wakiwemo wamiliki wa huduma, na kutekeleza hatua za kupunguza vikwazo kabla ya utekelezaji wa miradi ili kupunguza usumbufu.**

## 16.3 Utafiti Hafifu wa Wingi wa Magari na Watumiaji wa Barabara na Usanifu Unaosababisha Barabara Kuharibika Mapema

Sehemu ya 4.0 ya Mwongozo wa Vifaa vya Ujenzi na Usanifu wa Barabara wa Mwaka 1999 inataka usanifu wa tabaka za barabara za lami kufanyiwa utafiti wa kutosha na uchambuzi wa uzito na wingi wa magari yanayotarajiwa kupita ili kutoathiri usanifu wa tabaka la lami, hasa ukubwa wa mizigo, shinikizo katika matairi, na idadi ya kurudia uzito wa magari kwa kipindi cha usanifu.

Nilibaini kuwa TANROADS hakuhakikisha kuwa utafiti wa watumiaji wa barabara uliofanyika ulijumuisha ukuaji wa uchumi wa maeneo ya mradi, ambao uliathiri makadirio ya wingi wa magari yaliyozalishwa na kuathiri makadirio ya usanifu.

Pia, mapitio yangu ya ripoti za usanifu za miradi teule yalibaini kuwa usanifu ulifanyika ili kukidhi mahitaji kwa miaka 20 baada ya kukamilika kwa mradi wa barabara, hivyo kutarajia ongezeko la idadi ya magari yaliyotambuliwa wakati wa kipindi cha usanifu kama ilivyowasilishwa katika **Jedwali Na. 52**.

### Jedwali Na. 52: Uchambuzi wa usanifu wa uwezo wa barabara kuhimili mizigo

| Mradi wa Barabara | Maisha ya Usanifu (Miaka) | Usanifu wa Uzito wa Magari (TLC) | Athari na Hali Halisi wakati wa Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| Uboreshaji wa Barabara ya Mbeya-Makongolosi, | 20 | TLC 3 | Kwa miaka nane tangu kukamilika kwake mwezi Novemba 2015, mradi umepitia uchakavu wa mapema. |

| Mradi wa Barabara | Maisha ya Usanifu (Miaka) | Usanifu wa Uzito wa Magari (TLC) | Athari na Hali Halisi wakati wa Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| Sehemu ya I: Mbeya-Lwanjilo | | | Uchakavu huo ni kama vile mashimo na kubanduka kwa tabaka la lami ulionekana dhahiri |
| Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko ya Jiji la Dodoma (km 112.3) kiwango cha lami 1: Nala-Veyula-Mtumba-Ihumwa Bandari Kavu (km 52.3) | 20 | TLC 20 | Ripoti ya usanifu wa barabara iliyorekebishwa ya mwaka 2022 baada ya kuanza kwa mradi ilibainisha kuwa makadirio ya wingi wa magari yalikuwa magari 97,992,018, ambayo yalikuwa zaidi ya TLC 50 wakati mradi ulisanifiwa awali kwa TLC 20, lakini Wakala wa Barabara Tanzania hatimaye ulikataa pendekezo hili kutokana na vikwazo vya bajeti ambavyo havikupangwa awali kwa ajili ya usanifu huo. |
| Ukarabati wa Barabara ya Igawa-Uyole-Songwe-Tunduma na Ujenzi wa Barabara ya Mchepuko ya Uyole - Songwe | 20 | TLC 50 | Madaraja kama vile Kimani na Songwe yanahitaji hatua za ufuatiliaji na matengenezo ya mara kwa mara ili kuhakikisha yanaendana na usanifu wa masharti ya TLC 50 |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi mwaka 2024 kutoka katika Ripoti za Usanifu wa Miradi iliyochaguliwa*

Kwa kuongezea, kutozingatia usanifu wa barabara kulisababisha kupunguza uwezo wa matabaka ya barabara kuhimili mizigo. Aidha, niliona upungufu kwenye muda wa usanifu wa barabara katika Mwongozo wa Usanifu wa Muundo wa Barabara wa Mwaka 2011, ambapo huenda hadi miaka 30 huku iliyotolewa katika Mwongozo wa Vifaa vya Ujenzi na Usanifu wa Barabara wa Mwaka 1999 unaishia miaka 20.

Changamoto katika utafiti wa watumiaji wa barabara, uchambuzi, na usanifu zilihusishwa na kutotosheleza kwa miongozo ya usanifu ya Wizara ya Ujenzi, kutokuhusisha vya kutosha washauri elekezi wanaohusika kufanya utafiti wa kina wa watumiaji wa barabara, na ukaguzi duni wa usanifu kwa TANROADS ili kuhakikisha usanifu unaonesha makadirio ya hali ya watumiaji wa barabara.

**Ninapendekeza TANROADS atenge rasilimali kwa ajili ya utafiti katika mbinu za ujenzi wa ubunifu na kushirikiana na Wizara ya Ujenzi kuendeleza**

**viwango vya kazi za barabara ili kupunguza makosa kwenye usanifu wa barabara.**

## 16.4 Utafiti Usiotosheleza wa Maji na Usanifu wa Miundombinu ya Maji

Kifungu cha 5.7 cha Mwongozo wa Usanifu wa Muundo wa Barabara wa Mwaka 2011 kinataka usanifu sahihi wa mifereji ya barabara na kupanga kwa kuzingatia mambo muhimu kama vile kiwango cha maji ya mvua kubwa, kiwango cha maji ya mtiririko wa mkondo; na asili na aina ya udongo wa bonde ikiwa pamoja na uwezekano wa mmomonyoko wa udongo.

Nilibaini kuwa TANROADS hakuhakikisha kuwa usanifu wa kiwango cha maji ulionesha hali halisi ya eneo la mradi na mabadiliko ya hali ya hewa. Matokeo yake, ukaguzi uliona kuwa idadi ya usanifu wa miundombinu ya maji iliyotolewa ilikuwa na kadirio la chini, ukubwa wa miundombinu ya maji ulikuwa mdogo kuliko iliyohitajika, na miundombinu kuwekwa sehemu isiyo sahihi.

**Jedwali Na. 53** linaonesha hali na athari zilizotokana na utafiti hafifu wa usanifu wa maji na upembuzi yakinifu katika miradi husika.

**Jedwali Na. 53: Athari za utafiti na usanifu wa miundombinu ya maji**

| Jina la Mradi | Hali Iliyoonekana | Athari |
|---|---|---|
| Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam - Awamu ya 3: Kipande cha Kwanza (km 23.33) | - Ukaguzi wa Mabadiliko ya Mkataba (Nyongeza Na.1) wa tarehe 4 Aprili 2024 ulibaini kuwa kulikuwa na makadirio duni ya idadi ya mabomba na miundombinu ya mifereji ya maji. | Kuongezeka kwa gharama za miundombinu ya mifereji ya maji kwa Shilingi 488,547,433.44 |
| Barabara ya Tabora-Koga-Mpanda km 105.389 Kasinde-Mpanda na Mchepuko wa Mji wa Uruwira km 2.29) | - Mapitio ya Ripoti ya Mwisho wa Mradi, mwezi Septemba 2023 ukaguzi ulibaini katika sehemu B.4 kulikuwa na makadirio duni ya mifereji ya wazi, na upungufu wa kutosha wa nondo. | Makadirio yasiotosheleza ya kazi za mifereji ya maji yalisababisha ongezeko la zaidi ya asilimia 145 ya gharama za kazi za mifereji kwa Shilingi 6,021,608,010.23 |
| Uboreshaji wa Barabara ya Bagamoyo-Sadani-Pangani-Tanga (km 256) kwa kiwango cha Lami, Kipande cha 1 (Pangani-Tanga, km 50) | - Mapitio ya ripoti ya maendeleo ya kila mwezi Na. 47, mwezi Agosti 2024, sehemu ya 12.1 yalibaini kulikuwa na usanifu duni wa ukubwa wa miundombinu ya maji, uliosababisha mabadiliko ya ukubwa wa makalavati kipenyo | - Kuongezeka kwa idadi ya miundombinu ya zege kwa ujazo wa 950m3, sawa na ongezeko la gharama ya Shilingi 239,400,000.00.<br>- Kuongezeka kwa idadi ya nondo sawa na tani |

| Jina la Mradi | Hali Iliyoonekana | Athari |
|---|---|---|
| | cha sm 90 kuwa makalavati ya kipenyo cha boksi.<br>- Mapitio ya mabadiliko ya Mkataba (Nyongeza Na. 1), mwaka 2022 yalibaini kuwa kulikuwa na usanifu duni wa kuimarisha Daraja la Kirare, ambalo liliongezeka kwa kiasi cha kuweka mawe. | 153, sawa na ongezeko la gharama ya Shilingi 385,560,000.<br>- Kuongezeka kwa kiwango cha mawe kulisababisha gharama ya Shilingi 85,927,500 |
| Ujenzi wa Barabara ya Sakina-Tengeru na Barabara ya Mchepuko Arusha | - Mapitio ya ukaguzi Sehemu ya 3.7 ya ripoti ya mwisho ya mradi, mwezi Aprili 2019, yalibaini kuwa kulikuwa na upungufu wa miundombinu ya maji, uliosababisha kupungua kwa makadirio ya daraja. | Ongezeko la idadi ya nondo halisi kwa ujenzi wa daraja ilisababisha ongezeko la gharama ya Shilingi 6,095,905,431.65. |

***Chanzo**: Uchambuzi wa wakaguzi wa taarifa za usanifu na nyaraka za majalada ya miradi mwaka 2024*

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa usanifu duni wa miundombinu ya maji ulihusishwa na ukusanyaji wa taarifa usiotosheleza kutoka kwa washauri elekezi ili kuhakikisha eneo la bonde linasanifiwa kwa taarifa sahihi. Pia, kulikuwa na mapitio duni ya usanifu wa miundombinu wa washauri elekezi ili kuhakikisha miundombinu iliyopendekezwa inakidhi mahitaji halisi ya mradi.

Kwa kuongezea, hakukuwa na utafiti wa kitaifa wa masuala ya maji na miongozo ya usanifu ambayo inazingatia mabadiliko ya hali ya hewa ya sasa. Nilibaini kuwa tafiti za maji na usanifu wa miundombinu zilitokana na Muundo wa Mafuriko wa Afrika Mashariki (TRRL) wa Mwaka 1976, ambao haujumuishi mabadiliko makubwa katika matumizi ya ardhi na mabadiliko ya hali ya hewa ya hivi karibuni, kama vile kuongezeka kwa kiwango cha mvua.

Kulikuwa na kutozingatia usanifu unaoweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kama ilivyoelezwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania mwaka 2019 na 2020. Mamlala ya Hali ya Hewa iliripoti kuongezeka kwa wastani wa mvua wa kila mwaka kwa mm 256.5 mwaka 2019, sawa na 125% ya wastani wa muda mrefu wa kuanzia mwaka 1981 hadi 2010, na kwa mm 100 mwaka 2020, sawa na 163.6% ya wastani wa muda mrefu wa mwaka 1981 hadi 2010, ikihusishwa na kushindwa kwa miundombinu ya maji kabla ya mwisho wa muda wa usanifu.

**Ninapendekeza TANROADS afanye tafiti za kina za maji, uchambuzi wa matumizi ya barabara, na uchunguzi wa udongo wa chini ya matabaka ya barabara ili kuboresha usanifu na kuhakikisha uthabiti wa miundombinu, usalama, na ufanisi wa gharama nafuu.**

## 16.5 Utafiti Hafifu wa Udogo wenye Shida kwa Ajili ya Usanifu wa Barabara

Sehemu ya 5.0 ya Mwongozo wa Vifaa vya Ujenzi na Usanifu wa Barabara wa Mwaka 1999 inataka uchunguzi wa kina wa udongo kufanywa mapema katika miradi. Uchunguzi huu unapaswa kuanza na utafiti na upembuzi yakinifu wa taarifa kuhusu eneo la mradi. Unapaswa pia kujumuisha uchunguzi wa mstari wa katikati ya barabara, katika kina na umbali unaohitajika, pamoja na uchambuzi wa sifa za udongo wa tabaka za chini kama inavyohitajika.

Nilibaini kuwa TANROADS haikuhakikisha kuwa uchunguzi wa udongo uliofanywa ulikuwa wa kina ili kupata sifa za udongo uliopo. Pia, niliona utambuzi duni wa sehemu zenye udongo mbaya, na usanifu haukutoa suluhisho kuhusu sehemu hizo zenye udongo mbaya.

Pia, nilibaini kuwa uchunguzi duni wa udongo ulihusishwa na kutowashirikisha washauri elekezi wanaohusika kuzingatia masharti ya uchukuaji wa sampuli unaohitajika wakati wa ukusanyaji wa taarifa ya udongo. Aidha, ukaguzi usioridhisha uliofanywa na TANROADS ili kuhakikisha kuwa uchunguzi wa udongo uliofanywa ulizingatia Mwongozo wa Vifaa vya Ujenzi na Usanifu wa Barabara wa Mwaka 1999. Matokeo yaliyoripotiwa yalionesha hali halisi ya mradi katika uchunguzi wa udongo usiofaa.

Hata hivyo, TANROADS alionesha kuwa kwa wakati huo ulimshirikisha mshauri elekezi wa kuhuisha Mwongozo wa Vifaa vya Ujenzi na Usanifu wa Barabara, ambapo changamoto zilizobainishwa zitashughulikiwa kwa kutoa njia na mbinu zinazowezesha uchambuzi sahihi na michakato bora ya usanifu kushughulikia ugumu wa uhalisia wa eneo la mradi. **Jedwali Na. 54** linaonesha madhara ya uchunguzi duni wa udongo na vifaa kwa miradi husika.

**Jedwali Na. 54: Athari za uchunguzi hafifu wa udongo na vifaa**

| Jina la Mradi | Hali Iliyoonekana | Athari |
|---|---|---|
| Barabara ya Tabora-Koga-Mpanda km 105.389, Kasinde-Mpanda na Mchepuko wa Mji wa Uruwira km 2.29) | - Mapitio ya ripoti ya mwisho ya usanifu ya mwezi Juni 2016 yalibaini upungufu wa sampuli ya udongo iliyochukuliwa, ambayo ilikuwa takribani umbali wa kilomita 1 kutoka sehemu moja hadi nyingine kinyume na mita 250 kama inavyotakiwa.<br>- Mapitio ya Taarifa ya Uchunguzi wa Ufa wa Barabara (Ripoti Na. C334), | Kuongezeka kwa unene wa tabaka za barabara, na kusababisha ongezeko la makadirio na gharama<br>- Kupasuka kwa marefu kwa sehemu kati ya km 324 na km 331 juu ya tabaka la juu (CRR) na ukingo wa barabara kulisababisha kuchelewa kukamilika kwa mradi kwa miezi 8.27 na kuongezeka kwa |

| Jina la Mradi | Hali Iliyoonekana | Athari |
|---|---|---|
| | mwezi Disemba 2020 ulibaini kulikuwa na usanifu duni dhidi ya athari za unyevu kwenye udongo wa tabaka la chini kinyume na sehemu ya 2.2.0 ya Mwongozo wa Vifaa vya Ujenzi na Usanifu wa Barabara wa Mwaka 1999 | gharama ya usimamizi kwa Dola za Kimarekani 3,607,315 |
| Uboreshaji wa Barabara ya Bagamoyo-Sadani-Pangani-Tanga (km 256) kwa kiwango cha lami, Kipande cha 1 (Pangani-Tanga, km 50) | - Katika mapitio ya ripoti ya mwisho ya usanifu wa barabara, mwezi Juni 2016, nilibaini kuwa sampuli ya udongo ilichukuliwa kwa umbali wa mita 1,000 badala ya mita 250 kama inavyotakiwa na kusababisha kukutana na sehemu nyenye udongo mfinyanzi mweusi kwa sehemu ya km4.15 (km 182 + 200-km, 218 + 500), wakati wa utekelezaji ambayo ilihusishwa na ongezeko la gharama kama ilivyoripotiwa kwenye taarifa ya maendeleo ya kila mwezi Na. 47. | Kuongeza kiasi cha kuondoa udongo wa mfinyanzi mweusi kwa ujazo wa 910,347$m^3$, sawa na Shilingi 16,854,246,000.00.<br>- Ongezeko la ujazo wa kujaza udongo mzuri wa matabaka ya barabara kwa ujazo wa 660,882$m^3$, sawa na Shilingi 4,097,470,725. |
| Uboreshaji wa Barabara ya Itoni-Ludewa-Manda (km 211.4) kwa kiwango cha lami, Kipande 1 (Itoni-Lusitu km 50) | - Nilipitia sehemu ya 3.7 ya ripoti ya madai ya ongezeko la muda ya mkandarasi ya mwezi Juni 2024, ambayo ilionesha kuwapo kwa udongo dhaifu kwa umbali wa kilomita 2.35. (km 30+375-32+600 & 35+375-35+500) | - Kuongezeka kwa udongo imara ili kufidia sehemu zilizojazwa baada ya kuondolewa kwa udongo dhaifu hadi kina cha mita 1, ambayo iliongeza gharama na kuchelewesha maendeleo ya mradi. |

***Chanzo**: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Usanifu na Nyaraka za majalada ya miradi, 2024*

**Ninapendekeza TANROADS atekeleze mchakato wa ukaguzi ili kuhakikisha ubora wa usanifu, ikiwa pamoja na ukaguzi wa taarifa na kuzingatia taratibu za ubora, kushughulikia masuala ya kawaida ya usanifu na kuboresha matokeo ya mradi.**



# SURA YA KUMI NA SABA

## Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi

# UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA DARAJA LA KIGONGO - BUSISI

## 17.1 Utangulizi

Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi ni miongoni mwa nguzo muhimu katika utekelezaji wa mpango wa miaka mitano wa maendeleo nchini. Daraja hili linatarajiwa kuwa kiungo muhimu kati ya Mkoa wa Mwanza na nchi jirani za Rwanda, Burundi na Uganda, na kuwa kichocheo cha kukuza uchumi na kupunguza umaskini katika eneo hilo kubwa. Ukaguzi huu wa kiufundi kuhusu ujenzi wa Daraja la Kigogo – Busisi ili kujiridhisha iwapo Wakala wa Barabara Tanzania umetekeleza ipasavyo mradi huo kwa kuzingatia gharama, muda, ubora na mawanda ili kuwezesha kufikia malengo ya mradi yaliyokusudiwa. Taarifa ya mkataba imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. VIII.**

## 17.2 Usimamizi wa Mkataba

### 17.2.1 Kuchelewa Kukamilika kwa Mradi kwa Siku 310

Kifungu cha 1.1 cha Masharti Maalumu ya Mikataba kinataka mradi kutekelezwa kwa miezi 48 kuanzia tarehe ya kuanza ikiwa pamoja na miezi 3 ya maandalizi ya ujenzi. Tarehe iliyotarajiwa ya kukamilika kwa mradi ilikuwa 25 Februari 2024.

Mapitio yangu na ziara ya moja kwa moja kwenye mradi ilibaini kuwa tarehe ya kukamilika kwa mradi iliongezwa mbele kwa siku 310 hadi tarehe 31 Disemba 2024 kutokana na sababu mbalimbali kama vile kuchelewa kwa maandalizi ya ujenzi, kuchelewa kwa malipo ya awali, na kuchelewa kwa uamuzi wa urefu wa nguzo za chini ya daraja kama ilivyoelezwa katika **Kiambatisho Na. IX.** Nilibaini zaidi kwamba hapo awali mkandarasi aliomba kuongezewa siku 444, ikiwa pamoja na sababu zingine kama vile kuchelewa kwa malipo ya kazi, hali isiyotarajiwa ya miamba, na viwango vya maji wakati wa ujenzi wa nguzo. Baada ya mshauri kuchambua madai, siku 311 tu zilikuwa halali, na mwajiri alitoa siku 310.

Hata hivyo, ninahusisha upungufu huo na kuchelewa kwa siku 72 kwa mwajiri kulipa malipo ya awali na idhini ya mabadiliko ya usanifu kwenye urefu wa nguzo za chini za daraja. Pia, Janga la UVIKO-19 linahusishwa na sababu za kuchelewa kwa mradi.

Athari za kuchelewa kukamilika kwa mradi huo ni pamoja na kuongezeka kwa kiasi cha shilingi milioni 696.03 za gharama za ziada zisizo za moja kwa moja za matengenezo, utoaji wa elimu ya VVU/UKIMWI, n.k. Pia, kiasi cha ziada cha Shilingi bilioni 1.79 kiliongezeka kwa ajili ya usimamizi wa mshauri elekezi.

**Ninapendekeza TANROADS aimarishe mchakato wa malipo ili kuhakikisha uchambuzi na idhini ya mabadiliko ya muundo yanafanyika kwa wakati ili utekelezaji wa mradi uendelee kwa ufanisi bila kuchelewa zaidi.**

### 17.2.2 Riba ya Shilingi Bilioni 4.5 kama Adhabu kwa Kuchelewa Kulipa Hati ya Malipo Ya Kazi

Kifungu cha 16 cha Masharti Maalumu ya Mikataba na Kifungu kidogo cha 51.1 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba kinamtaka mwajiri kumlipa mkandarasi kiasi kilichothibitishwa na mshauri elekezi ndani ya siku 28 kuanzia tarehe ya kila hati.

Mapitio yangu ya hati za malipo yalibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania ilicheleweshaa malipo kwa mkandarasi zaidi ya tarehe inayostahili kwa kipindi cha hadi siku 131 kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. X**. Malipo hayo yalichelewa kwa siku 13 kwa Hati Na. 23, wakati ucheleweshaji wa juu ulikuwa wa siku 137 (miezi 4.6) kwa Hati Na. 16, hivyo kufanya ucheleweshaji kuwa wa wastani wa siku 60 kwa hati ya malipo. Hivyo, kwa mujibu wa masharti ya mkataba, kiasi cha shilingi bilioni 4.5 kilidaiwa na mkandarasi kama riba ya kuchelewa kwa hati za malipo kuanzia namba 1 hadi 23.

Kukosekana kwa fedha hizo kulisababishwa na utaratibu usioridhisha wa utoaji wa fedha wa Wizara ya Ujenzi kwenda TANROADS, ambapo ilichukua muda usiopungua siku 41 hadi siku 193 kutoa fedha zilizoombwa na TANROADS, hivyo kuchelewesha uchakataji wa hati za malipo, ambapo ilichukua takribani siku saba kufanya malipo ya stahiki za mkandarasi baada ya kupokea fedha kutoka Wizara ya Fedha kupitia Wizara ya Ujenzi.

**Ninapendekeza TANROADS ashirikiane na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha kuandaa utaratibu utakaohakikisha hati za malipo zinalipwa kwa wakati ili kuepuka adhabu zitokanazo na tozo za riba. Utaratibu unapaswa kuwezesha ombi la wakati, utoaji, na muafaka wa hati za malipo zilizoombwa na mkandarasi na Mshauri Elekezi.**

### 17.2.3 Malipo ya Ziada ya Shilingi Bilioni 16.4 Kutokana na Marekebisho ya Bei kwa Vifaa Vyenye Viwango Vipya

Kifungu cha 55.3 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba kinazuia marekebisho ya bei kutumika kwa kazi zinazothaminiwa kulingana na gharama au bei za sasa, mabadiliko, na kazi za siku.

Mapitio yangu ya Hati za Madai ya wakandarasi yalionesha kuwa wakandarasi walikabidhi Hati zao za Madai zikiwa na marekebisho ya bei kwa kazi zilizo thaminishwa kwa viwango vipya vilivyowekwa baada ya kusaini mkataba. Viwango vipya vilisababisha malipo ya ziada ya Shilingi bilioni 16.4 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 55**.

**Jedwali Na. 55: Marekebisho ya bei kwa vifaa vipya**

| Marejeo ya Nukuu | Maelezo ya Vifaa | Gharama (Sh.) |
|---|---|---|
| SS64.02 b.iv | Uzio wa kuzuia maji kwa ajili ya ujenzi wa nguzo za juu (Pier) 3-30, Pier 36-64 | 2,539,230,708.63 |
| SS64.02 b.vi | Uzio wa kuzuia maji kwa ajili ya ujenzi wa nguzo za juu (Pier) 32, 33 and 34 | 470,632,494.68 |
| SS64.02 b.v | Uzio wa kuzuia maji kwa ajili ya ujenzi wa nguzo za juu (Pier) 31,35 | 189,273,321.85 |
| 61.27 c | Nguzo za kudumu za chini ya daraja zenye kipenyo cha mita 2.5 | 3,251,701,306.78 |
| 61.27 d | Nguzo za kudumu za chini ya daraja zenye kipenyo cha mita 1.5 | 9,948,017,206.46 |
| SS67.06 | Usanifu wa taa za LED | 10,928,791.97 |
| **Jumla** | | **16,409,783,830.38** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa wakaguzi kutoka hati namba 6 hadi 24 mwaka 2024*

Pia, nilibaini kuwa maoni ya Mshauri Elekezi yaliyomo kwenye barua yenye Kumbukumbu Na. YS-TZ-KBS-202305127-27 yalifichua kuwa mkandarasi alitakiwa kutojumuisha viwango vipya kwa vipengele vya marekebisho ya bei kwa ajili ya kuweka mashimo na nguzo za zege.

Taratibu zisizokuwa bora za usimamizi wa mkataba wa mradi uliofanywa na TANROADS zilileta kasoro hii. Hii ilisababisha gharama za ziada kwa mradi ambazo zilileta upotevu wa fedha kwa serikali.

**Ninapendekeza TANROADS aimarishe usimamizi wa mikataba wakati wa utekelezaji wa mradi na udhibiti wa gharama ili kuepuka mabadiliko ya viwango baada ya kusaini mkataba. Pia, kurejesha kiasi cha fedha kilicholipwa zaidi kwa wakandarasi.**

### 17.2.4 Malipo ya Ziada ya Shilingi Milioni 181.72 Kutokana na Tathmini Hafifu ya Hati za Malipo ya Kazi Zilizofanywa

Kanuni ya 243 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inataka taasisi inayofanya ununuzi kuidhinisha hati za malipo kwa tathmini na vipimo kwa vipindi au hatua zilizotajwa katika mkataba. Aidha, Kifungu cha 50.3 cha

Masharti ya Jumla ya Mikataba kinamtaka meneja mradi kufanya tathmini ya thamani ya kazi zinazotekelezwa.

Mapitio yangu ya hati za malipo ya vifaa vilivyolipwa na ukaguzi wa mradi yalibaini kuwa TANROADS alilipa ziada ya jumla ya Shilingi 181,720,066.77 kwa kazi zilizopimwa ambazo ni pamoja na kusafisha eneo la mradi, kuondoa udongo wa juu katika eneo la barabara iliyojengwa, mbao za kumwaga zege kwenye nguzo ya awali za daraja, na nguzo za kati za zege za daraja kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 56**.

### Jedwali Na. 56: Malipo ya kazi zilizopimwa

| Marejeo ya nukuu | Maelezo ya Vifaa | Kipimo | Kiasi Kilicholipwa | Kiasi cha Kazi Zilizofanyika | Kiwango cha Kazi (Sh.) | Kiasi za Hati za Malipo (Sh. Milioni) | Kiasi Kilichohesabiwa na Mkaguzi (Sh. Milioni) | Tofauti (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 31.1 a.i | Kusafisha eneo la mradi | ha | 10.2 | 5.91 | 14,575,847 | 148.67 | 86.13 | 62.55 |
| 31.1.b.i | Kuondoa udongo wa juu eneo la mradi | $M^3$ | 12,146 | 8863.15 | 7,288 | 88.52 | 64.59 | 23.93 |
| 62.01b. iv | Kumalizia msingi wa nguzo ya awali kwa daraja F3 | $M^2$ | 441.28 | 287.6 | 23,124 | 10.20 | 6.65 | 3.55 |
| 64.01 -b (ii) | Nguo za katikati za daraja (Pier1-31), (Pier 35-65) | $M^3$ | 71,732.74 | 71532.47 | 457,839 | 32,842.05 | 32,750.35 | 91.69 |
| Jumla | | | | | | 33,089.44 | 32,907.72 | 181.72 |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa mkaguzi wa hati za malipo na vipimo vilivyopatikana kwenye ukaguzi wa mradi mwaka 2024*

Ninahusisha malipo ya ziada ya kazi zilizofanyika na tathmini hafifu ya vipimo iliyotekelezwa na mshauri, kutokuwapo kwa njia ya kawaida ya mwongozo wa kipimo kwa kazi za ujenzi na kutohakiki usahihi wa viwango vya kazi na TANROADS.

**Ninapendekeza TANROADS ahakikishe kuwa malipo yaliyoongezeka kwenye bei yaliyofanywa kwa Mshauri Elekezi na mkandarasi yanarejeshwa kulingana na bei halisi. Vilevile, marekebisho yote yaliyofanywa kwa vifaa na viwango vipya baada ya kusainiwa kwa mkataba yawe yanalipwa ili kupunguza athari za riba kwenye malipo yaliyocheleweshwa.**

### 17.2.5 Faini ya Shilingi Milioni 627.19 Ambayo Haikudaiwa Kutokana na Mabadiliko ya Wafanyakazi Waandamizi

Kifungu cha 14 Sehemu ya II ya Masharti Maalumu ya Mikataba kinamtaka mwajiri kupunguza asilimia 10 ya malipo ya usimamizi wa kazi wakati wa mabadiliko ya wafanyakazi muhimu, kutoka asilimia 25 hadi asilimia 50 ya jumla ya miezi ya kazi kwa sababu nyingine isipokuwa kifo au sababu za kiafya.

Mapitio yangu ya Ankara Na. 22 yalibaini mabadiliko ya wafanyakazi watatu muhimu, sawa na jumla ya miezi 63.74 ya kazi. Mapitio zaidi ya fomu 5B2 ya muhtasari wa gharama yanaonesha kuwa Shilingi bilioni 6.27 zilitengwa kwa ajili ya malipo ya wafanyakazi waandamizi. Hivyo, mabadiliko ya wafanyakazi waandamizi bila kuzingatia masharti ya mkataba yalimfanya mshauri huyo aadhibiwe kwa kutozwa faini ya kiasi cha Shilingi milioni 627.19.

Hata hivyo, nilithibitisha kuwa Wakala wa Barabara Tanzania haikudai faini hiyo hadi Ankara Na. 23 ilipotolewa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 57**.

**Jedwali Na. 57: Adhabu kwa mabadiliko ya wafanyakazi waandamizi**

| Nafasi | Hali ya Mabadiliko | Miezi ya Kazi | Miezi ya Mabadiliko | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Meneja wa Mradi | Imebadilisha | 48 | 5.27 | 2.43 |
| Mhandisi wa Daraja | Imebadilisha | 48 | 10.47 | 4.82 |
| Mtafiti wa Topografia | Imebadilisha | 48 | 48.00 | 22.12 |
